ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe.Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim — **Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 21 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, naomba kuwasilisha hati mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 173

Chumba cha Mizigo Bandarini Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kuna jengo liliopo Bandarini Zanzibar ambalo lilijengwa kwa ajili ya kuweka biashara (*Duty Free Shop*). Jengo hilo halikuwahi kutumika.

(a) Je, Mhe. Waziri serikali ina mpango gani na jengo hili?

(b) Je, serikali haioni kuwa jengo hilo kuendelea kubakia kama lilivyo ni kupoteza nguvu za wananchi?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 173 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Jengo lililopo Bandarini Malindi lilikusudiwa kuwa "*Duty Free Shop*", ambalo kwa bahati mbaya halikuwahi kutumika kutokana na muhusika (Mwekezaji) kufunguliwa kesi Mahakamani. Jengo hilo lilikuwa chini ya amri ya Mahakama kwa muda mrefu. Hivyo, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ilichukuwa juhudi kuomba idhini ya kulitumia, ambapo hivi karibuni tu Shirika la Bandari liliruhusiwa kulitumia.

Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari inakusudia kulijenga upya jengo hilo kwani limeharibika sana, ili kuweza kuzihamishia afisi zake za bandarini na kutoa nafasi kwa ajili ya kuengeza eneo la kuhifadhia makontena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ni mtu aliyesoma sheria tena anavyo vyeti vyake, basi anaweza kutuambia kesi hiyo iko Mahakamani na idhini hiyo ameipatia wapi au ameiomba vipi?

(a) Mhe. Spika, kesi iko Mahakamani hiyo idhini umeiomba wapi?

(b) Kwa sababu kesi iko Mahakamani maamuzi ya mwisho yatakapotokewa kinyume na serikali atafanya nini?

(c) Lile eneo wananchi wanaokwenda Pemba wanapata tabu sana wakati wa mvua pamoja na watoto wao wadogo. Hivi atakuwa tayari kutafutiwa mwekezaji kwa ajili ya kuwastiri wananchi wanaokwenda Pemba kutokana na eneo lile wanavyopata shida, kwa sababu tuwachukulie wale wananchi ni wa Jimbo la Chwaka. Sasa atawafikiria vipi, ili kuweza kuwasaidia?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika.

(a) Mwekezaji huyu alikuja kuwekeza Zanzíbar na waliofungua kesi hii ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar kupitia Wizara ya Fedha. Kwa kweli kesi hii imechukua muda mrefu tokea mwaka 1997/1998 hadi leo hii.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, yaani Serikali Kuu ndio tuliowaomba idhini kwa kupitia mawasiliano yaliyofanywa na Idara ya Mahakama, baada ya kwisha jengo hili kutolewa ushahidi, basi Idara ya Mahakama ilituruhusu kutumia.

(b) Mategemeo yetu ni kwamba Idara ya Mahakama inatambua vizuri sheria na maamuzi hayo yaliyofanywa kwa niaba ya serikali

yalikwisha kupimwa na kuona kwamba hakuna athari zozote za kisheria zitakazopatikana pindi maamuzi hayo yakiwa kinyume.

(c) Mhe. Spika, katika jibu mama nimeeleza kwamba madhumuni na malengo ya Shirika la Bandari kwa jengo hili ni kulivunja na kulifanyia ukarabati na kujenga jengo jipía litakaloweza kutumika kwa shughuli za afisi kwa baadhi ya afisi ya Shirika la Bandari. Sambamba na hilo kuondoa baadhi ya majengo yaliopo katikati ya eneo, kwa ajili ya kuongeza eneo la kuweka makontena na jengo hili liweze kutumika kwa shughuli za kiofisi za Shirika la Bandari.

Mhe. Machano Othman Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nataka kuongezea tu kidogo. Mwaka 2010 mwanzoni Mhe. Rais wa Zanzíbar alitembelea Bandari na Shirika la Bandari waliomba kwamba ile sehemu waruhusiwe, ili wapajengwa kwa ajili yakutumia kwa shughuli zao za Bandari.

Kwa kuwa inasemekana huyu ambaye anayeshtakiwa huko aliko tayari ameshafungwa nchi za Ghuba, basi Mhe. Rais aliagizwa kwamba Wizara ya Fedha wafute kesi, ili watoe fursa kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wajenge pale. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nadhani kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba Bandari wanao mpango mzuri wa kujenga katika eneo lile baadaye ya Wizara ya Fedha kumalizana na Mahakama. *(Makofi)*

Nam. 209

Watoto Kupatiwa Huduma ya Chanjo

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Tunaipongeza Wizara ya Afya kwa jitihada kubwa wanayochukua ya kuwahamasisha wazazi, kuhusu umuhimu wa kuwafikisha watoto wao hospitali, kwa ajili ya kupata chanjo kila pale wanapotakiwa kufanya hivyo. Hata hivyo, ni asilimia ndogo ya wananchi wanaoitikia wito huo.

Kwa kuwa mtoto kutokupatiwa huduma hiyo muhimu hutoa mwanya wa kupata maambukizo mbali mbali. Je, Mhe. Waziri jitihada gani za makusudi zitachukuliwa ili kutatua tatizo hilo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 209 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inampongeza Mhe. Mjumbe kwa kutambua jitihada zetu kuhusu chanjo. Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Chanjo imekuwa ikifanya juhudi kuhakikisha kwamba kiwango cha chanjo Zanzibar kinaongezeka na kila mtoto mwenye umri wa kupata chanjo anazipata bila ya usumbufu wowote.

Hata hivyo, tathmini ya mwisho imeonesha kwamba Wilaya ya Kaskazini "A" na "B" kwa Unguja na Mkoani na Micheweni kwa Pemba zilikuwa na kiwango kidogo cha chanjo kwa mwaka 2009. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

- Kukutana na watendaji wa Afya wa Wilaya ya Kaskazini "A" na "B", Mkoani na Micheweni na kuitathmini hali hiyo kwa pamoja na Wakuu wa Wilaya na watendaaji wao.

- Kwa kushirikiana na Timu za Afya, tumewapatia mafunzo ya uhamasishaji juu ya chanjo watu mashuhuri kutoka kila Shehia wakiwemo Masheikh, Maimamu, Walimu wa Madrasa, Wakunga wa Kienyeji nakadhalika.

- Tumeongeza idadi ya vituo vinavyotoa chanjo katika maeneo yasiyo na vituo vya afya kwa kila wilaya.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Naibu Waziri hatua gani nyengine ambazo zilizochukuliwa kwa hopitali nyengine kuhusu suala zima la asilimia ndogo ya chanjo kwenye maeneo mengine katika kipindi hiki cha mwaka huu?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, katika vituo vya afya hakuna tatizo. Kwa hivyo, tatizo liliopo ni kwamba watu hawafiki kule, kwa sababu vituo vya afya vimetayarishwa na chanjo zipo, sasa pale ambapo tumehisi vituo vya afya havitoshi ndio maana tumeamua kufungua hata sehemu nyengine, ili watu waweze kufikia chanjo.

Kwa maana hiyo, kuna *outreach* points nyingi kwa sehemu ambazo hakuna vituo karibu, ili watu waweze kupata huduma kwa ukaribu kama tatizo ni kuvifuatilia mbali.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza naishukuru sana Wizara ya Afya kwa jitihada yake ya kuwapatia watoto chanjo. Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna baadhi ya sehemu muamko wa kuwapeleka watoto kupata chanjo ni mdogo.

Sasa je, moja ya sababu ambayo kuwa wanadai watu, yaani wanasema kwamba mtoto anapopata chanjo hasa ikiwa ni sindano ya paja inasababisha pengine kuleta athari ya maumivu au mtoto kulemaa?

Je, suala hili lina ukweli na kama ni kweli ikitokezea mtoto kupigwa sindano na kupelekea kupata matatizo ni hatua gani wizara yake inachukua kwa ajili ya kumsaidia mtoto huyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna sindano ambazo zinapigwa mapajani katika sindano hizo zinazotumika kama chanjo. Lakini anavyoiunganisha chanjo ya paja na kulemaa mguu sio kweli, kwa sababu kinacholemaza mguu ni sindano ambao inapigwa takoni tena katika sehemu ile iliyoainishwa.

Hivyo, sindano ya paja mara nyingi watoto wanakuwa wanapata homa, lakini wazazi wanatahadharishwa kwamba mtoto kwa siku ya leo na kesho atakuwa na homa kwa hiyo tumpe dawa ya kupunguza homa.

Kwa kweli hakuna chanjo hata moja inayopigwa sehemu ambayo inaweza ikamlemaza mtoto. Kwa maana hiyo, msiwe na wasi wasi na watu wenu wafahamisheni, ili waje wawape watoto chanjo, kwa sababu kuna umuhimu wa kukinga maradhi na njia moja ya kukinga maradhi wasipate matatizo watoto ni kuwapa chanjo.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe ambapo majimbo yenu pamoja na wilaya zenu hazifanyi vizuri, basi wahamasisheni watu kwani Wizara ya Afya tumejipanga vizuri chanjo zipo na serikali inajitahidi kwa asilimia kwa mia kununua chanjo na wala hatupewi na wafadhili. Kwa hiyo, wahamasisheni watu waje kwenye chanjo. *(Makofi)*

Nam. 221

Wanafunzi wa Elimu Mbadala Kukoseshwa
Fursa ya Kujiendeleza zaidi

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa makusudi imeamua kuanzisha Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, ili kuwasaidia na kuwarejesha skuli vijana waliocha skuli kwa sababu mbali mbali. Vile vile serikali imeanzisha Vyuo vya Amali Mkokotoni na Vitongoji, ili wale vijana wanaomaliza Kituo cha Elimu Mbadala wapate fursa zaidi ya kujiendeleza. Hata hivyo, kuna malalamiko kwamba vijana hao kutoka Elimu Mbadala hawapatiwi nafasi hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri ni kwa nini vijana hao wa Elimu Mbadala hawapatiwi fursa ya kuendelea na elimu katika Vituo vya Amali Mkokotoni na Vitongoji?

(b) Tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Elimu Mbadala ni vijana wangapi waliomaliza na kupewa fursa ya kuendelea na Vyuo vya Mkokotoni na Vitongoji?

(c) Kwa nini serkali haiwapatii msaada wa fedha na zana za ufundi vijana wanaomaliza Elimu Mbadala na Elimu ya Amali, ili waweze kujiajiri wenyewe na kupunguza umasikini wa kipato.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam.221 lenye vifungu (a), (b) na (c).

Mhe. Spika, ni kweli kuwa Kituo cha Elimu Mbadala, Rahaleo kimesaidia sana katika kuwapatia elimu na ujuzi vijana waliacha masomo njiani kwa sababu mbali mbali. Pia serikali, imeanzisha Vituo vya Mafunzo ya Amali, huko Mkokotoni Unguja na Vitongoji Pemba kwa dhamira ya kuwaendeleza zaidi vijana wanaokamilisha mafunzo katika Kituo cha Elimu Mbadala, ili wapate ujuzi wa kazi za amali na waweze kujitegemea wenyewe.

Baadhi ya vijana waliomaliza Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, waliwahi kujiunga katika Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

(a) Vijana waliomaliza mafunzo katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo wamepatiwa nafasi za mafunzo katika Kituo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni. Kuhusu Kituo cha Mafunzo ya Amali ya Vitongoji, ni kweli kuwa hakuna vijana waliomaliza Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo waliojiunga na kituo hicho kwa vile vijana wa Rahaleo ni wakaazi wa Unguja, hivyo isingekuwa rahisi kwa wao kuishi Vitongoji kutokana na shughuli zao za kimaisha.

(b) Vijana 20 kutoka Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo walichaguliwa kujiunga na Kituo cha Mafunzo ya Amali, Mkokotoni katika mwaka wa kwanza. Kwa bahati mbaya, vijana hao waliacha masomo njiani kwa sababu mbali mbali, zikiwemo umbali wa Kituo Mkokotoni na maeneo wanayoishi mjini hasa kwa vile vijana hao wanajitegemea wenyewe kimaisha.

Pia wengi wao walishindwa kuendelea kwa vile wanahitaji muda wa kufanya kazi na wasingeweza kukaa darasani kwa muda wote wa masomo. Pamoja na kushindwa kuendelea na mafunzo ya kazi za Amali huko Mkokotoni. Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo kimeanzisha mafunzo ya awali ya kazi za amali kwa vijana wanaosoma katika kituo hicho. Baadhi ya vijana hao wameweza kujiajiri baada ya kukamilisha mafunzo yao.

(c) Vijana watakaomaliza mafunzo katika Vituo vya Mafunzo ya Amali vya Mkokotoni na watapenda kujiajiri wenyewe badala ya kuajiriwa watapatiwa mikopo ya fedha na vifaa. Hadi sasa hakuna vijana waliomaliza mafunzo hayo na hivyo hakuna wahitimu waliopatiwa mikopo hiyo. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa nini Pemba hakuna Kituo kama hiki cha Mbadala?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo tulikijenga kwanza kwa majaribio, sasa baada ya kuona kwamba kituo kile kinafanya uzuri. Kwa hivyo, sasa vituo hivyo tunavieneza na kwa upande wa Pemba tayari tumeshaanza kujenga kituo hicho Wingwi Mtemani na kimefikia hatua kubwa tu. Vile vile tutajenga vituo

vyengine kwa upande wa Pemba kama vile Ungi – Konde, Makombeni – Mkoani pia tutajenga kituo kama hicho katika Jimbo la Mtambwe. *(Makofi)*

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza. Lini Vyuo vya Amali vitajengwa Mkoa wa Kusini Unguja?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, vituo hivi tunatarajia kujenga kwa kila Mkoa wa Zanzibar. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe awe mstahamilivu na kituo hicho kitamfikia. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa kama alivyojibu katika swali la pili la nyongeza kwamba Kituo cha Amali Pemba kiko Wingwi pamoja na Mtambwe. Lakini naona vituo hivi ni vya kimajimbo inavyoelekea.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kujenga kituo kikubwa kama kilichopo hapa au nusu yake hususani ukiangalia *geography* ya Pemba Chakechake ni eneo la katikati linalokusanya njia zote. Kwa hivyo, kwa nini hakuna utaratibu wa kujengwa Chakechake ambacho kitakusanya kila anayetoka.

(b) Kwa kuwa tunavyo Vituo vya Amali na taarifa zilizopo ni kwamba vituo vile zana zilizokwisha kupelekwa ndio zimeshapelekwa. Je, Wizara ya Elimu ina mpango gani wa kuongeza nyenzo ya kufanyiakazi wale vijana katika Vituo vya Amali, hususan tukitizama vinahitaji kupata kujiandikisha katika *NECTA*, ili vionekane kwamba vina jarada lililosawa na vyuo vyengine.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, hiki kituo ambacho nilisema ni cha Wingwi – Mtambani, hiki ndio kitakuwa *centre* kwa pemba kama ambavyo kiko katika Jimbo la Rahaleo na ni Kituo chambo tunakiita cha Rahaleo. Kwa hivyo, sidhani kama tutakijenga ambapo hapana jimbo, yaani popote ambapo tutajenga ni sehemu ambayo ni jimbo la uchaguzi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kwa Unguja *centre* ni Rahaleo na kwa upande wa Pemba itakuwa ni Wingwi – Mtemani ndio itakuwa *centre* katika vituo vyetu hivi vya Elimu Mbadala. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kuhusu nyenzo kama ambavyo tuliahidi kwenye bajeti yetu, kwamba tutajitahidi kuhakikisha kuwa wanapata nyenzo bora za kisasa za kufanyiakazi. Nakushukuru Mhe. Spika, *(Makofi)*

Nam. 208

Wananchi wa Konde Kununuliwa Tangi Jipya

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Tangi la Kuhifadhia Maji Safi na Salama lilioko vilima vitatu Konde haliko katika hali inayostahili kwa shughuli za kuhifadhia maji safi na salama. Hii ni kutokana na kuwa pleti za chini za tangi zinaendelea kukatika vipande na kuchafua maji na kuwa hayafai kwa matumizi ya binadamu. Pia tangi hilo halikupata mnyanyuko jambo ambalo linachangia kudhoofisha msukumo wa maji.

Kwa kuwa tangi hilo limeshatengenezwa mara kadhaa bila ya mafanikio. Je, Mhe. Waziri, serikali ina mpango gani wa kuwapatia wananchi wa Konde tangi jipya, ili waondokane na maji machafu?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 208 kama ifuatavyo:-

Ni kweli tangi la kuhifadhia maji liliopo vilima vitatu Konde ni kongwe, halikupata mnyanyuko na ni dogo likilinganishwa na mahitaji ya maji ya Mji wa Konde kutokana na kasi kubwa ya utanukaji wa mji huo. Tangi hilo kwa muda mrefu sasa halina uvujaji wowote wa maji kutokana na matengenezo makubwa yaliyofanywa na iliyokuwa Idara ya Maji wakati huo.

Pamoja na ukongwe wake, tangi hilo ni salama kwa shughuli zote za kuhifadhia maji kwa matumizi ya binaadamu na ukweli kwamba tako la tangi hilo ni la zege wala si la chuma kama inavyofikiriwa.

Aidha, Mamlaka ya Maji inakiri kwamba kuna haja ya kujenga tangi kubwa la juu la zege, ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia eneo kubwa zaidi kadri hali ya fedha itakaporuhudu.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri lakini naombani muulize swali moja la nyogeza.

Kwa kuwa amekiri yeye mwenyewe kutokana na idadi ya watu katika Jimbo la Konde wamezidi kuongezeka na amekiri kwamba atakuwa tayari kujenga tangi hilo. Kwa hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri ni lini hasa kwa kuwa hiki ni kipindi cha bajeti na fedha ipo tayari, basi ni lini Mhe. Waziri atatuhakikishia tangi hili litajengwa?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina lengo la kuboresha na kutengeneza matangi mapya kwa yale maeneo yote yenye matatizo ya maji na hususani katika eneo hilo. Kwa hiyo, ni kweli hiki ni kipindi cha bajeti na tunategemea tutakapoingiziwa fedha basi tutaanza kulishughulikia suala hili.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Hivi sasa ni mwaka watatu huu baada ya kujengwa tangi jipya katika kijiji cha Bahanasa kwenye Jimbo la Mtambwe na kutokezea matatizo likapasuka tena, basi halikushughukiwa mpaka leo.

Sasa Mhe. Naibu Waziri anasema mkakati wake mara baada ya Baraza hili atashughulikia hayo matangi mabovu na pale ambapo pametokezea matatizo kama hayo.

Je, katika huo utaratibu aliuweka hilo tangi la Bahanasa limo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, kama nilivyoeleza ni kwamba wizara yangu kupitia Mamlaka ya Maji ina lengo la kulishughulikia suala la tatizo la maji, kuyaboresha matangi pamoja na kujenga matangi mapya. Hivyo, kwa vile na wao wamo katika mlolongo huo, basi tutalishughulikia tangi lao. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa alipokuwa akijibu swali mama amekiri kwamba tangi la Konge lilioko Vilima Vitatu ni bovu na limeharibika na limetengenezwa zaidi ya mara tatu, lakini bado tangi hilo ni bovu na kuna wajibu au nia ya kujenga tangi jengine.

Kwa hivyo, namuuliza Mhe. Waziri kwa sababu tangi hilo wamelitengeneza zaidi ya matatu ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kutengeneza tangi hilo kwa mara tatu?

Je, hizo fedha zilizotumika mara tatu hawaoni kama ni bora kujenga tangi jengine wakati huo kabla ya kuziharibu?

Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa na wizara yake kwa ajili ya kujengea matangi wakati huu, ambapo wananchi wa Konde wanamatatizo?

Je, kama fedha tayari kwa sababu bajeti tayari tumeshaipitisha ya fedha, yaani Bajeti Kuu ya Serikali. Kwa hivyo, ni lini hasa ni mwezi gani wataanza kujenga matangi hayo kwa ajili ya kuwaondoshea usumbufu wananchi wa Konde waliowengi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante Mhe. Spika, wakati nilipojibu swali mama nilisema kwamba tangi hilo kwa hivi sasa halina uvujaji wa aina yoyote ya maji.

Kwa hivyo, tangi hilo ni zima.

Vile vile nilisema tutajenga tangi jengine kuboresha kutokana na udogo wa tangi hilo.

Kuhusu fedha za matengenezo yaliyofanyiwa tangi hilo suala hili nitakujibu kwa maandishi. *(Makofi)*

Nam. 210

Kukosekana Huduma ya Umeme Shehia ya Msuka

Mhe. Suleiman Hemed Khamis – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wananchi wa Shehia ya Msuka na Konde wamekosa huduma ya umeme, jambo ambalo husababisha usumbufu mkubwa.

Je, Mhe. Waziri ni lini vijiji vifuatavyo vitaweza kufaidika na huduma ya umeme na kuonja matunda ya Mapinduzi: Gombani – Dodea – Ungi – Kivumoni – Mnarani na Mkia wa Ng'ombe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 210 kama ifuatavyo:-

Napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kuwa vijiji vya Gombani, Ungi, Kivumoni, Mnarani na Mkia wa Ng'ombe vinaweza kufaidika na huduma ya umeme

iwapo Mhe. Mwakilishi atashirikiana na Shirika pamoja na wanavijiji, ili kuchangia upelekaji wa umeme katika vijiji hivyo, hapo awali vijiji vingi vilifaidika na huduma ya umeme kutokana na Mradi wa Umeme vijijini, ambao umemalizika tokea mwaka 2009, hivyo wakati huu kuvipatia umeme vijiji hivyo inahitaji mashirikiano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suali moja dogo la nyongeza.

Watu wa vijiji hivi wamekosa umeme kwa muda mrefu hawaoni kwamba wamekosa raha za Kimapinduzi tangu kipindi hicho mpaka leo, kwa kuwa wenziwao wanafaidika na umeme kusema tu muwakilishi anashirikiana nao katika kuvipatia umeme si rahisi, lakini hapa ni suala la serikali vijiji ni vingi Gombani, Dodea, Uungi, Kivumoni na Mnarani hawana umeme.

Je huoni kwamba hao watu si rahisi kwa muwakilishi kuweza kuwapatia faida hiyo?.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati: Kwanza naomba Mhe. Muwakilishi akumbuke kwamba serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi kirefu imesambaza umeme katika vijiji vingi vya Zanzibar kwa hivyo vijiji hivyo ambavyo havijabahatika si lengo la serikali kutowapelekea umeme, lengo la serikali ni kuwapelekea umeme. Lakini kutokana na miradi ambayo ilikuwa tunaitegemea kwa muda huu imemalizika muda wake kwa hivyo ili kupata wepesi shirika langu kuwapeleka umeme vijiji hivyo basi lazima tujenge mashirikiano katika Shirika pamoja na Muwakilishi na wananchi kwa jumla.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mashirikiano ni jambo muhimu sana na kwa msingi huo ndio maana wananchi wa jimbo la Kiwani kwa misingi ile walikubali kuchangia nguzo 40, Chwaka nguzo 25, Kilindongo 6 na Kidutani nguzo 10. Hadi hii leo shirika lake limeshindwa kuwasaidia wananchi wale hata kuwapimia pamoja na kuwasaidia waya. Sasa anakusudia kutwambia mashirikiano yepi ambayo shirika lake litatoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati: Mimi ningesema tu kwamba hao wananchi ambao wamekusanya hizo nguzo basi kama bado shughuli zao hazijashughulikiwa, basi warudi tena na waje kwangu mimi ikisha tutashirikiana pamoja na shirika langu la umeme kwa kuziangalia nguzo hizo, kama itakuwa ni nguzo ambazo zina kiwango basi tutazitumia nguzo hizo,

kama itakuwa hazina kiwango basi tutapeana ushauri mzuri pamoja na kusaidiana kwa ajili ya kuiendeleza hali hiyo ya kupelekea umeme vijijini wananchi wetu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Spika, ninavyofahamu katika kumbu kumbu zangu juzi tulipokuwa tukichangia kwenye hotuba ya bajeti ya wizara hii katika sehemu ya umeme vijijini, hotuba ilieleza kuwa wale wote ambao hawajapatiwa umeme vijijini watapatiwa wote.

a) Je, Mhe. Waziri anakwenda kinyume na maelezo yaliyomo kwenye hotuba yake ya bajeti ya mwaka huu.

b) Kwa kuondolea matatizo haya ya umeme niliita kama kisio tu ya kijiji kimoja cha Jimbo langu kinaitwa Chanjaani na gharama zilikuwa ni shilingi milioni 22 na vijiji vyenyewe ni vingi. Hivyo kweli Mhe. Mwakilishi ana uwezo wa kueneza umeme katika vijiji ambavyo havina kwa kutumia nguvu zake mwenyewe.

c) Ilani yetu ya CCM inaeleza nini huduma hii ya umeme kwa wananchi.

Mhe. Spika: Hili la ilani ya CCM nafikiri sio la wizara hii, kwa hivyo jibu haya mengine.

UTARATIBU

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, tunavyofahamu serikali hii ya moja wa kitaifa inaongozwa na ilani ya uchaguzi ya CCM, halafu inavyoelewa hutuba zote zinazotolewa hapa zinalenga kwenye ilani hiyo kwa hivyo haiwezekani mtu aongoze bila ya kwenda kwenye ilani hiyo, ndio nasema kwa sababu imo shughuli ya umeme katika ilani ya CCM inamueleza nini Mhe. Waziri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa nakubaliana nawe unavyosema lakini sina hakika kama anaweze kuinukuu hiyo ilani kwa urahisi, kama anaweza basi atusaidie lakini kama hakuiweza nadhani kidogo tumsamehe hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Mazingira na Nishati: Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuongozwa na Rais Mhe. Doctor Ali Mohammed Shein lengo na madhumuni ni kuhakikisha kwamba kuwaondolea wananchi

matatizo ya aina zote ikiwemo na masuala haya ya umeme, ni kweli serikali inaendeshwa katika ilani ya chama cha Mapinduzi kwa kufuata ilani hii lengo ni kujenga nchi na kuwatumikia wananchi vile ipasavyo.

Kwa hivyo kilichoahidiwa na serikali hii kwa kupitia ilani hii ya Chama cha Mapinduzi basi chote kitatekelezwa kwa mujibu wa vile kilivyoahidiwa.

Mhe. Spika: Waheshimwa wajumbe kabla ya kuendelea nimepokea maombi mawili matatu na nafikiri mengine yatakuwa yapo kwa baadhi ya wenzetu waheshimiwa kuhitaji kwenda mazikoni. Kuna mwenzetu mmoja Mungu amuweke pahala pema lakini tukitoa ruhusa saa hizi kwa ajili ya shughuli hiyo tunaweza kuwa na upungufu mkubwa wa Koram ya kumaliza shughuli yetu hii itakayofuata muda mfupi hivi punde.

Hivyo niwaombe basi waheshimiwa wajumbe tustahamili na tupitishe masuala ya wizara hii halafu baadae sio kwamba wote tunakwenda huko, nafikiri mnadhim wa Chama cha Mapinduzi mjumbe wa Kamati Kuu Mhe. Salmin Awadh Salmin atafanya utaratibu na hatimae anaweza kuniambia wachache waweze kushirikia lakini wengine tuendelee na shughuli yetu hii. Ahsanteni sana.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

(Majadiliano yaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe tulikubaliana jana kwamba leo tuwasikilize baadhi ya Mawaziri walioomba ili kusaidia ufafanuzi kwa kumsaidia Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, nimesimama kuomba muongozo wako kuhusiana na kauli ambayo umeitoa hivi punde, kuhusiana na mwenzetu amabae amefariki na wengine tungependa kwenda mazikoni, lakini agizo ulilolitoa umelitoa kwa upande mmoja. Sasa sijui kwa upande huu wa pili nani atakuwa *responsible. (Makofi)*

Mhe. Spika: Nashukuru sana kwamba serikali ya umoja wa kitaifa inafanya kazi nzuri sana na kumekuwa na mwelekeo wa mashirikiano makubwa mno, nilifikiri kwa sababu ya maombi yaliyonifikia yote yametoka upande mmoja kwamba labda wanaohitaji kwenda ni hao peke yao. Lakini kama kuna na

wengine wanaohitaji kwenda basi Mnadhim Mhe. Rashid Seif Suleiman nae anaweza kufanya kazi hiyo hiyo lakini baada ya kukamilisha kazi hii nao wataniarifu wachache waweze kwenda lakini wengi tubaki kuendelea na kazi iliyobakia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea na shughuli zetu hizi za Baraza na kutuweka katika hali ya afya na uzima, aidha nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza asubuhi hii kuchangia hoja hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na Michezo.

Aidha nimshukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa namna ambavyo wamewasilisha vizuri hotuba hii ya bajeti, pia napenda niseme kwamba naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba hii ya bajeti.

Mhe. Spika, katika michango waliyotoa waheshimiwa wajumbe kwanza nichukue fursa hii niwapongeze sana kwa michangoa mizuri ambayo lengo lake ni lilelile lengo la serikali la kuendeleza sekta zetu hizi za habari utamaduni Utalii na Michezo, kwa hivyo walichokieleza ni yale yale ambayo serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya muundo wa Umoja wa Kitaifa imekusudia kuyatekeleza, kwa hivyo niwapongeze sana waheshimiwa kwa mwelekeo huu.

Mhe. Spika, katika michango ya wajumbe yako mambo pia yamegusa kwa kiasi fulani wizara yangu na moja nataka niwashukuru sana sana waheshimiwa, kwa kusema kwamba wametoa ushauri kuhusu malipo ya madeni yanayodaiwa taasisi mbali mbali za serikali kwa kiwanda chetu hichi cha upigaji chapa, ushauri huu tunaupokea na tutaufanyia kazi na nataka niwahakikishie waheshimiwa wajumbe kwamba tayari wahusika tumeshawaandikia barua kuwaelekeza ushauri ambao waheshimiwa mmetupa ili kuhakikisha kwamba malipo haya yanafanyika ili kiwanda chetu hichi cha upigaji chapa kiweze kufanya kazi zake kwa vizuri zaidi.

Lakini Mhe. Spika, vile vile serikali inachukua hatua ya kukiimarisha kiwanda hiki katika hatua zetu za awali kwanza kihamisha hiki kiwanda kutoka mahala ambapo kipo sasa kule Saateni kutokana na mazingira ya pale, nia ni kwamba tukihamishe kiwanda hiki na kiweze kuhamia Maruhubi pale kilipokuwepo kiwanda cha sigara ili kiweze kufanya kazi zake vizuri zaidi katika mazingira yaliyo mazuri zaidi. Hivi sasa serikali inachukua hatua ya kutafuta mitambo mipya kwa ajili ya kukiimarisha kiwanda hiki, tayari tumeanza mazungumzo na wafadhili mbali mbali ikiwemo Serikali ya Oman na imeonyesha nia njema ya kutusaidia ili kiwanda hiki kiwe cha kisasa kabisa, nathubutu kusema baada ya kupokea hiyo mitambo itakuwa ni kimoja katika kiwanda kizuri sio kwa Zanzibar na Tanzania, lakini kwa Afrika ya Mashariki Nzima.

Kwa hivyo tutaweza kuwa na ushindani ulio mzuri katika kukamilisha wajibu wetu wa uchapishaji, lakini ningependa kutoa wito Mhe. Spika, kwa taasisi za serikali kukitumia kiwanja hiki kwa sababu bila ya kupeleka kazi zetu ambazo zitasaidia sana kukisaidia kiwanda hicho kufanya kazi zake vizuri itakuwa hatukukitendea haki kiwanda hicho. Kwa hivyo naomba nitoe wito kwa taasisi zote za serikali kwamba kazi zao wazipeleke pale na sisi tunawahakikishia kwamba sasa hivi kiwanda kimeanza kujipanga upya na kinafanya kazi zake vizuri zaidi.

Mhe. Spika, wajumbe pia walielezea sana suala la utalii hasa suala la *package tour* na wengine wetu hapa tulizungumzia kusema kwamba utaratibu huu sio mzuri ni utaratibu ambao unaikosesha serikali mapato, Mhe. Spika, na waheshimiwa wajumbe nia ya serikali ni kuwa na utalii wenye hadhi, utalii wa daraja la juu tokea awali hiyo ndio ilikuwa nia yetu, lakini lazima tuanze na katika kuanza kuna ugumu wakekatika safari yetu hatukuanza moja kwa moja tukafikia ile hatua tuliyokusudia, lakini hatua zimechukuliwa na hivi sasa zipo hoteli mbali mbali za daraja la juu zimejengwa hapa Zanzibar na zinatoa huduma hizo za hadhi ya juu kabisa.

Kutokana na hali hiyo hivi sasa kwa kiasi fulani ule utaratibu wa *package tour* unapungua hatua kwa hatua, tulipoanzia Mhe. Spika, zaidi ya asilimia 95 ndio ilikuwa tunatumia utaratibu huu wa *package tour* lakini sasa ni kati ya asilimia sitini na sitini na tano, kwa maana hiyo zaidi ya asilimia 35 ni wale watalii wanaokuja nje ya utaratibu huu kwa vyovyote vile kadiri ya siku zinavyokwenda utaratibu huu utapungua, lakini juu ya hali hiyo ambayo waheshimiwa wawakilishi wamesema kwamba utaratibu huu wanaikosesha mapato serikali. Ni kweli inaipunguzia mapato sio kuikosesha mapato moja kwa moja, kwa sasa hivi kwa utaratibu huu tuliokuwa nao mchango wa sekta ya utalii katika pato la taifa ni karibu asilimia 27 msingi wake ni kwamba unachangia vizuri katika pato la taifa.

Lakini vile vile Mhe. Spika, sekta hii ya utalii inatoa ajira za moja kwa moja zaidi ya watu 12,500 wameajiriwa katika sekta hii, lakini wale ambao hawakuajiriwa moja kwa moja ni wengi sana ni zaidi ya watu elfu 45 wameajiriwa sio moja kwa moja lakini ajira zao zinatokana na sekta hii ya utalii. Kwa hivyo kwanza ni kichocheo kikubwa cha uchumi wetu lakini pia inachukua sehemu kuba ha ajira katika nchi yetu lakini asilimia 70 ya mapato ya fedha za kigeni yanatokana na sekta hii ya utalii kwa utaratibu huu ambao sasa tunao.

Sasa kazi iliyopo mbele yetu ni kuzidi kuimarisha kuvutia wawekezaji wakubwa waje kujitokeza, changamoto yetu kubwa ni kwamba ni lazima

tuanze kujipanga vizuri kuisaidia wizara hii kupitia kamisheni yake ya utalii ili waweze kujitangaza zaidi. Mhe. Spika, ukiangalia wenzetu majirani hapo Kenya tu wanatumia zidi ya dola milioni 6.3 kwa mwaka katika kujitangaza. Tanzania Bara wao wanatumia zaidi ya dola milioni 1.50 katika kujitanga. Syshel kisiwa kidogo tu Mhe. Spika, wanatumia zaidi ya dola milioni 6.7 katika kujitangaza. Moritious wanatumia zaidi ya dola milioni 15 kwa mwaka katika kujitangaza, Afrika ya Kusini wanatumia zaidi ya dola milioni 90 kwa mwaka katika kujitangaza.

Kwa hivyo ukiangalia wenzetu hawa wanachukua hatua kubwa sana sasa moja katika wajibu wetu mkubwa ni kuhakikisha kwamba sekta hii tunaisaidia kifedha kuhakikisha kwamba inapata nafasi nzuri ya kujitangaza lili iweze kutoa ushindani mkubwa zaidi. Kwa sasa hii *package tour* bado inaendelea kutusaidia, kama nilivyosema hatua kwa hatua kadri tutakavyozidisha uwezekezaji wa utalii wenye hadhi ndio vile vambavyo na hii itapungua.

Lakini Mhe. Spika, nini kinafanyika ni kwamba sio kwamba hakuna mapato yanayopatikana kutokana na utaratibu huu, utaratibu huu ni kwamba mtalii analipa mwanzo kule anakotoka na anavyofika hapa anapata huduma zote, lakini si kwamba zile fedha haziji hapa kwetu zile fedha lazima zije kwasababu hawa watalii wanahitaji malazi, wanahitaji kula, wanahitaji usafiri, kunywa n.k. Kwa hivyo hulipa zile fedha kule lakini kwa taratibu zao ndio fedha zile huletwa hapa nchini na zikatumika. Mfano mzuri ni sisi tunapokwenda Makka inabidi tulipie hapa Zanzibar lakini unapokwenda kule zile huduma muhimu zote unazipata sio kwamba hivi fedha hazitoki hapa kwenda kule, hivi fedha zinatoka hapa na zinakwenda kule.

Kwa hivyo utaratibu huu unatusaidia na unaweza kuondoka kama tukiweza kuzimaliza changamoto kubwa zilioko mbele yetu, kwanza ni kuwa na Air line yetu wenyewe itakayoweza kuleta watalii moja kwa moja hapa, hiyo ni moja katika changamoto kubwa sana na moja katika eneo ambalo linaingizwa fedha ambazo zinaingizwa katika usafiri kwa maana ya tiketi za watalii kuja hapa nchini. Mhe. Spika, tungekuwa na shirika letu la ndege basi mapato hayo yangaingia mfukoni mwetu.

Lakini vile vile tungalikuwa na ndege zinazokuja moja kwa moja kwa maana ya *direct flight* ingesaidia sana kuondokana na utaratibu huu, kwa hivyo jitihada za serikali zinazochukuliwa hivi sasa katika kuimarisha kiwanja cha ndege, kuimarisha jengo la kiwanja cha ndege, kuimarisha *rain way* hiyo itavutia sana ndege za mashirika mbali mbali mbali makubwa ulimwenguni kuja Zanzibar, kwa misingi hiyo basi utasaidia kuongeza kuleta watalii wenye hadhi.

Mhe. Spika, nataka nichukue fursa hii kuwapongeza sana sana ndugu zetu wa Oman kwa kuanzisha ndege ile ya Shirika la Oman kuja moja kwa moja Zanzibar, jambo hili nalo linasaidia sana katika kuimarisha sekta yetu ya utalii, vile vile niwapongeze ndugu zetu wa Kenya kwa ndege yao ya *Kenya Air ways* kufanya kazi hiyo. Lakini kadiri tutakavyoimarisha uwanja wetu wa ndege Mhe. Spika, ndivyo ambavyo tutaweza kuimarisha zaidi watalii wetu kuja hapa Zanzibar.

Kwa hivyo mfumo huu au utaratibu huu ambao Mhe. Spika tunaendelea nao mimi ningeomba Waheshimiwa wenzangu wajumbe wa Baraza hili tukufu tuendelee nao mpaka pale tutakapokuwa tuna uwezo kikamilifu tukiwa na mashirika yetu ya Ndege, ama kupata ndege za moja kwa moja pamoja na kuimarisha mahoteli yetu ili yawe ya hadhi ya juu na hapo ndio kipato kikubwa zaidi kitapatikana.

Mhe. Spika, utalii huu unatupa soko kubwa sana unatupa fursa za soko njia ya kujiongezea mapato ni pamoja na kulitumia kikamilifu hilo soko la utalii, kwa sababu Mhe. Spika, hata tukipata fedha zinazotokana na utalii kwa kiasi kikubwa watalii hawa fedha zao nazo wanazitumia kwenye chakula, kama tutaweza kuhakikisha kwamba tunazalisha chakula ambacho kitatumika katika mahoteli yetu hususan mboga mboga na matunda ambayo kwa kiasi kikubwa tungeweza kuwauzia wawekezaji wetu wenye mahotali ingesaidia kuongeza mapato yetu ya utalii wa ndani. Lakini pia yanasaidia kuimarisha ajira zetu za ndani kwa hivyo msingi mkubwa ni kutoa wito kwa wananchi wetu kujiendekeza katika kulitumia vizuri soko hilo ili mapato yanayotokana na utalii yote tuweze kupata wenyewe ikiwemo masuala ya kuimairisha mifugo na serikali inachukua hatua hiyo ya kujenga mazingira mazuri ili mifugo iwe ya kisasa. Kwa hivyo, wananchi wanatakiwa hapa wajielekeze katika ufugaji, wajielekeze katika kilimo cha mboga mboga ili tuweze kuimarisha mapato yanayotokana na utalii.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi ningewaomba Waheshimiwa Wajumbe tuunge mkono hoja hii ipite ili tuwawezeshe wizara hii iweze kufanya vizuri, na kwa sababu Waziri aliyeko ni mahiri, Naibu Waziri wake pia ni mahiri na watendaji wake mahiri. Mhe. Spika, mimi sina shaka yoyote tukiwawezesha hawa basi naamini wataweza kufanya vizuri zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru na mimi naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Mhe. Spika, baada ya kukushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri na watendaji wao kwanza kwa kusimamia

majukumu yao na pia kuandaa hotuba hii ya bajeti ambayo inaeleza mwelekeo katika mwaka huu tunaokwenda nao wa fedha.

Mhe. Spika, mimi naomba nichangie katika maeneo mawili. Mhe. Spika, katika michango mingi iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hapa imegusia suala la kulinda utamaduni wetu. Mimi naomba niungane nao katika *concern* hiyo kwa sababu ni jambo muhimu. Kama walivyosema baadhi yao kwamba hii ni roho ya taifa, kama haitokuw ana afya nzuri basi na taifa zima nalo litaumwa.

Mhe. Spika, labda kilichonipa wasi wasi tu ni kwamba ule mwelekeo wa kuona kuwa suala hili zaidi liko mikononi mwa serikali. Mhe. Spika, mimi nadhani suala la kulinda utamaduni wetu, silka na mila zetu kwanza linaanzia na sisi wenyewe katika ngazi ya familia.

Mhe. Spika, mimi nadhani suala hili linahitaji zaidi kumjenga mtu nafsi yake na akaamini na akaona fahari na utamaduni wake, mila yake na silka zake. Bila ya kumjenga mtu katika ngazi hiyo basi hakuna sheria ambayo inaweza ikamuongoza. Mhe. Spika, nafikiria tuna mifano mingi sana kama mtu hakujengwa katika nganzi pengine tokea mtoto kujua utamaduni wake, kuuthamini na kuweza kuuendeleza, basi nadhani kama hakuharibika utotoni anaweza kuharibika hata ukubwani kwa sababu atakuwa nafsi yake haikujengwa katika kuamini yeye ni nani. Mhe. Spika, kwa sababu utamaduni ndio unaomjenga ajitambue kwamba mimi ni nani napaswa nifuate utaratibu gani, napaswa nifuate njia gani za maisha.

Mhe. Spika, mifano iko mingi kwa sababu kuna watu pengine ya kutokujengwa katika misingi imara ya utamaduni wake, ya dini yake ambayo ni sehemu ya utamaduni, ya silka zake na mila zake. Mhe. Spika, akitoka hapa pengine akivuka bahari tu watu wakichubua na yeye basi atachubua. Kuna watu pengine wakivuuka bahari akenda kwenye utamaduni ambao watu hawavai nguo kwa staha kama anavovaa kuwa kwao, basi na yeye kama ni mtandio ama kama ni mavazi mengine ya staha anaweza akayaondoa, na mifano hii iko mingi kweli kweli. Lakini kwa watu ambao wamejengwa kwenye misingi ya kiutamaduni yakuamini ama imani yake ya dini, ama silka yake au utamaduni wake basi nafikiri hata akenda popote duniani hawzi kubadilika kwa sababu kenda pahala pengine. Kwa hivyo, mimi nasema huku tunakokwenda kwa kweli ni kugumu zaidi.

Mhe. Spika, ningeomba sana kwamba hili jukumu tulichukue kuwa ni la kwetu sote kwa sababu waheshimiwa sio tu ni walezi wa taifa letu, lakini ni walezi katika ngazi hata ya familia. Kwa hivyo, tulihimize jambo hili na sidhani kuwa ni wajibu ambao tunaweza tukaukasimu au tukaukodisha au tukauacha kwa kweli.

Mhe. Spika, labda katika kuthibitisha hili mimi niseme kama ni sheria wengi tumesahau kwamba nchi yetu mwaka 1973 ilipitisha sheria Nam. 1, hii sheria inaitwa sheria ya kulinda utamaduni wa taifa. Chini ya sheria hii ukisoma hasa kifungu cha 2 kinakataza mambo mengi sana. Kinakataza kuvaa nguo za kubana, na imetafsiriwa humu nguo ya kubana ni ile inayoonesha maumbile yale ya mtu mwenyewe hasa kwa wanawake. Pia kimekataza kuvaa nguo fupi, kuvaa nguo inayoonesha kifua wazi, lakini kwa wanaume pia imekatazwa kusuka, imekataza hata kuvaa wigi. Kwa hivyo, tujiulize suala kwamba sheria hii imeachwa leo? Mimi nasema imeachwa siku nyingi kwa sababu wengi sio rahisi kujua kwamba tuna sheria hii, au sheria hii bahati nzuri haikuwahi kufutwa bado ni sheria na iko katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sheria hii haitekelezwi kwa sababu kwa mazingira yake ya sasa hivi tukiangalia tunakuta kwamba kuitekeleza kwake inabidi tujenge labda magereza mapya na pengine tuwe na Mahakama mpya ya kusikiliza kesi hizi. Mhe. Spika, itabidi tuwe na polisi maalum ya kushughulikia kesi za utamaduni kwa sababu kwa Mahakama zilizopo itakuwa hazina nafasi kwa sababu sheria hii kama ni kuvunjwa ndio inayovunjwa sana, pengine tukitoka hapo nje tu tutaanza kukamata watu wanaovunja sheria hii.

Mhe. Spika, hiki ni kielelezo cha kuwa suala la kulinda utamaduni ni suala ambalo msingi wake linaanzia katika ngazi ya familia. Maana wengi wao wanaovaa hizo nguo ambazo hazistahiki ni watoto wetu, ni ndugu zetu, ni majirani zetu ni waumini wenzetu ambao tokea sheria ya mama ya dini yetu basi imekataza jambo hili.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa tunafuata sheria yetu wengi tuliokuwa waislamu katika nchi hii basi nafikiri tusingehitaji sheria nyengine. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba wito wangu kwa wenzangu na kwa wananchi kwa ujumla ni kwamba tumeacha majukumu yetu kama walezi wa familia, kama wasisimamizi wa familia tumeacha majukumu yetu na haya ndio matokeo yake. Mhe. Spika, kwa sababu leo ukitunga sheria iendane na mfumo wa wakati ule uliokuwepo, tulikuwa na sheria inayokataza watu kusafiri mpaka uwe na *visa* ya kuondokea. Mhe. Spika, sio unakokwenda, chini ya sheria ya *Migration control Nam. 9 ya 1969* ulikuwa unahitaji uwe na *visa* hata ya kuondokea hapa lazima uwe na *exist visa* vile vile. Kwa hivyo, mchanganyiko zamani ulikuwa mdogo, lakini leo mtu anakwenda anapotaka pengine anakunywa chai China anakuja kula chakula cha usiku hapa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, yale maingiliano baina ya jamii yetu na jamii ya dunia kwa ujumla kwa kweli imekuwa kubwa sana.

Mhe. Spika, kitu peke yake kitakachotuokoa, kitakacholinda silka na utamaduni wetu ni kurudi katika misingi ya dini yetu na kurudi katika misingi ya utamaduni wetu pamoja na silka zetu na kusimamia katika ngazi ya familia. Mhe. Spika, hiyo ndio itakuwa sheria kubwa na hakuna mtu ambaye anaweza akaivunja.

Mhe. Spika, la pili ambalo ni dogo nimesema nijaribu kuliweka sawa ni suala hili la kuanzishwa kwa Shirika la Utangazaji. Mhe. Spika, nakubaliana na michango iliyotolewa na wajumbe wengi hapa kwamba inaonekana huu utaratibu wa kuanzishwa kwake haukwenda sawa sawa. Kwa sababu ilitangulia kuteuliwa kiongozi wa hii taasisi kabla shirika lenyewe halijaanzishwa rasmi.

Mhe. Spika, mimi naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wajumbe kwamba kuanzishwa kwa taasisi hii kwa mfano hata ya Mamlaka ya Anga ilikuwa ni katika kuweka sawa mtiririko wa uanzishwaji wa viwanja hivi katika mwelekeo mpya wa serikali hii ya awamu ya saba. Pia zilianzishwa mamlaka hizi ile ya anga na hili Shirika la Utangazaji kwa kutumia Mamlaka ya Rais chini ya kifungu cha 53 cha Katiba ambacho kinampa uwezo wa kuanzisha ofisi yoyote hapa Zanzibar na kuwateuwa viongozi wa ofisi hizo.

Mhe. Spika, huo ulikuwa ni utaratibu wa dharura lakini kwa upande wa Mamlaka ya Anga kama tulivyoona miswada tumepata kwa sababu mamlaka itanzishwa chini ya sheria. Lakini kwa upande wa Shirika hili la Utangazaji tuna sheria ya *Public Investment Act Nam.4 ya 2002*.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kinachofanyika sasa hivi ni kuandaa tangazo la kisheria ambalo liko ofisini kwangu tunategemea ndani ya wiki hii na inayokuja hatua hizo zitakamilika kuandaa tangazo rasmi la kisheria la kuanzisha Shirika hili la Utangazaji. Litakapoanzishwa kwa sababu ile sheria ya *Public Investment Act* inaeleza utaratibu, muundo wa shirika na uendeshaji wake na pia baada ya kuanzishwa huko chini ya sheria hii ambayo inahusu uanzishaji wa Mashirika ya Umma, baadae inaweza kuja ikaangaliwa. Kwa hivyo, kwa mujibu wa kazi zake Shirika hili la Utangazaji je kuna haja ya kulianzisha kwa sheria mahsusi?

Mhe. Spika, kwa kawaida shirika linaanzishwa kwa sheria kama litakuwa lina kazi zaidi ya kuendesha shughuli zake litakapokuwa lile shirika lina kazi nyengine zaidi kama za *regulation* kwa mfano kama Shirika la Bandari. Mhe. Spika, Shirika la Bandari halifanyi kazi ya kibiashara, lakini linafanyakazi pia ya kusimamia mambo mengine ya masuala ya usimamizi wa bandari ambao una mambo mengi ya kusimamia utaratibu wake, kulinda na mambo yanayohusiana na bandari.

Kwa hivyo, lile ndio maana likaanzishwa kwa sheria, lakini hatua ya mwanzo ni kulianzisha kwa kupitia sheria ya *Public Investment Act* naomba niwahakikishie kwamba hatua hizo ziko katika hatua za mwisho katika kulikamilisha na baada ya hapo tutazingatia kama kuna haja ya shirika hili kulianzisha kisheria. Mhe. Spika, kama kutakuwa na haja hiyo baada ya kuona muundo wake na kazi zake, basi hatua hiyo itachukuliwa na serikali bila ya tatizo lolote.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo naomba kuunga mkono hoja na kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi wote waunge mkono hoja hii ili tuweze kupitisha hii bajeti ili wenzetu waanze kufanya kazi kwa mwelekeo huu ambao tumejipangia katika awamu hii ya saba ya serikali hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia. Mhe. Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha leo hii nikaweza kusimama hapa kuchangia Wizara yangu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Pia nikipongeze Chama changu ya Mapinduzi kwa kushirikiana na Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa kuweza kunichagua nikawa mwakilishi na mimi nikatekeleza wajibu wangu kwenye Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba. Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa mashirikiano tangu tulipoteuliwa kwa mashirikiano ya pamoja kuweza kufanya kazi zetu siku hadi siku.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo pamoja na Naibu Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote na wafanyakazi wa wizara hii kwa kuweza kushirikiana pamoja siku hadi siku kwa maslahi ya nchi yetu. Mhe. Spika, kwa kweli michangio mingi iliyochangiwa ni kuhusu kwenye mila na desturi, kama alivyoeleza Mwanasheria Mkuu wa Serikali sina haja ya kuharibu utamu aliyoueleza Mhe. Mwanasheria Mkuu, lakini na mimi nichangie kidogo kuhusu mila na desturi.
Mhe. Spika, jana Mhe. Panya alizungumza kwa unyenyekevu na masikitiko makubwa, kwa kweli mheshimiwa nakupongeza sana kujua kwamba ni utekelezaji ambao ni wetu sisi wazazi. Mhe. Spika, pia alizungumza kuhusu mavazi na kuhusu utekelezaji ambao ni wa maumbile kwenye binadamu, kwa kweli vijana wetu ni kweli wanakiuka maadili yetu na silka zetu za Kizanzibari. Mhe. Spika, jambo hilo lipo lakini nawaomba waheshimiwa tushirikiane pamoja na wizara na serikali ili kuwatoa vijana wetu kwenye mwelekeo ambao uliokuwa sio.

Vile vile na Mhe. Mtumwa Kheri Mbaraka na yeye alichangia kuhusu mavazi na utamaduni wetu, kwa kweli mimi nampongeza sana mheshimiwa kwa kulichangia hilo kwa sababu ni mwanamke ambaye ni ustadh mkubwa kwenye Baraza letu hili la Wawakilishi anatuelekeza mambo mbali mbali yanayohusu mavazi na kuhusu maendeleo ya jamii zetu. Pia alizungumzia kuhusu safari niliyokwenda na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Makamo wa Pili wa Rais tulikwenda kwenye tamasha ambalo lilifanyika Iran. Mhe. Spika, ni kweli tuliona mambo mbali mbali kwenye tamasha lile na niliona hali ambayo ni nzuri ya kuiga na kuileta hapa Zanzibar hii.

Mhe. Spika, nilipofika hapa nikawazungumzia Waheshimiwa wenzangu hasa wanawake niliwaambia nilipokwenda Iran nilikutia kitu ambacho ni kizuri kwa maadili yetu ya Kiislamu na maadili ya Mzanzibari. Mhe. Spika, niliwaeleza vizuri na waheshimiwa walinifahamu juu ya mambo mbali mbali yaliyoko kule.

Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Mgeni yeye pia alichangia kuhusu mila na desturi na vipindi vyetu vya televisheni vilivyoanzishwa mwanzo tangu wakati wa Rais wetu wa mwanzo. Kwa kweli mimi mwenyewe binafsi Mhe. Spika, nimesoma hapa kuanzia mwaka 1970 niliviona vipindi hivyo na vipindi hivyo vilikuwa vinaelimisha sana jamii. Mimi nilikuwa ni mdogo lakini historia yangu naijua sana na nampongeza Mhe. Mgeni kulikumbusha suala hilo, lakini tunamuahidi Mhe. Mgeni suala hili tutalifuatilia na tutaandaa vipindi mbali mbali kwenye wizara yetu ili kuelimisha jamii na watoto wetu.

Mhe. Spika, sasa niende kwa Mhe. Subeit Khamis Faki mwakilishi wa Jimbo la Micheweni. Mhe. Spika, Mhe. Subeit aliipongeza sana wizara yetu kwa kujenga redio jamii Micheweni, redio hii jamii imeleta faraja kubwa sana kwa jamii ya Micheweni kwa kuelimisha na kutoa taarifa muhimu zilizokuwa zinaigusa jamii ya Micheweni. Mhe. Spika, pia alizungumzia kuhusu wafanyakazi walioko katika kituo cha redio jamii.

Mhe. Spika, namwambia Mhe. Mwakilishi kuwa wizara yangu imejipanga kutekeleza majukumu yaliyoko katika kituo cha redio jamii kwa kuwasomesha wafanyakazi walioko pale. Pia tunategemea mwezi ujao yuko kijana wetu mwanamke anatoka Jimbo la Micheweni na anazungumza lahaja ya Kimicheweni, atakuja kusoma kwenye Chuo cha Habari ili awe na upeo zaidi wa kuweza kuzungumza ile lahaja ya Kimicheweni sahihi.

Mhe. Spika, sasa nije kwa Mhe. Mtando yeye aligusia kuhusu jengo letu la wizara, alizungumza mambo mengi kama alikwenda kwenye jengo letu kulikuwa kuna *function* akakutia mambo ambayo hayaridhishi. Mhe. Spika,

jengo lile tulipopewa tulipewa jengo ambalo lilikuwa ni bovu sana na mimi mwenyewe ni shahidi, kwani miaka mitano iliyopita nilikuwa ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, hivyo tumefanya juhudi mtu sifa yake apewe pale anapofanya vizuri.

Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe watupe sifa kuhusu jengo lile jinsi tulivyolifanyia ukarabati. Mhe. Mtando alisema kwenye ukumbi na eneo ambalo alikuwa akifikia Mhe. Spika, eneo lile hatukukabidhiwa, tulikabidhiwa lile jengo lakini sasa hivi Mwenyezi Mungu akitujaalia serikali ikitukabidhi ukumbi na lile eneo alilokuwa akifikia Mhe. Spika, tutalifanyia ukarabati ili tuweze kutekeleza mahitaji yetu ya wizara. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Mwakiliishi mambo yatakuwa mazuri na wewe ukiwa na *function* zako pale utakuja pale pale.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia pia nawaomba Waheshimiwa Wakilishi ng'ombe hamli mtoto wake huwa anamramba tu. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwaombe basi wakati mwengine makofi huwa yanaingiliana na majibu anayotoa Mhe. Waziri inafika pahala wakati wa kupitisha vifungu tunarudia yale yale ambayo Mhe. Waziri alijibu kwa utulivu mkubwa na ikawa mjumbe hakusikia kwa sababu ya makofi mengi. Makofi kama nilivyokuwa naelekeza mara kwa mara tuyapige kwa nidhamu ili tuweze kumsikia waziri akitoa majibu yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwanza kabisa natoa shukurani zangu za dhati kwako pamoja na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu na hasa kwa wale waliochangia kwa namna moja au nyengine katika bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sina budi kutoa shukurani hizo kwa michango yao mizuri waliyoitoa nasaha, busara zao pamoja na ushauri wao muafaka. Mhe. Spika, jumla ya waheshimiwa 30 wametoa michango yao ambao nitawataja nao ni:-

1. Mhe. Asha Bakari Makame.
2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
3. Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa
4. Mhe. Nassor Salim Ali
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Omar Ali Shehe
7. Mhe. Rashid Seif Suleiman
8. Mhe. Mbarouk Wadi Mtando

9. Mhe. Salmin Awadh Salmin
10. Mhe. Hija Hassan Hija
11. Mhe. Mohammed Said Mohammed
12. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
13. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
14. Mhe. Mussa Khamis Silima
15. Mhe. Subeit Khamis Faki
16. Mhe. Mgeni Hassan Juma
17. Mhe. Fatma Mbarouk Said
18. Mhe. Saleh Nassor Juma
19. Mhe. Mohammed Haji Khalid
20. Mhe. Raya Suleiman Ali
21. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed
22. Mhe. Haji Faki Shaali
23. Mhe. Othman Masoud Othman
24. Mhe. Bihindi Hamad Khamis

Pia kuna Waheshimiwa wengine ambao walichangia kwa maandishi pia nao sina budi kuwataja nao ni:-

1. Mhe. Thuwayba Edington Kissasi
2. Mhe. Salim Amour Mtondoo
3. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo
7. Mhe. Ashura Sharif Ali
8. Mhe. Bikame Yussuf Hamad
9. Mhe. Mussa Ali Hassan
10. Mhe. Suleiman Hemed Khamis na
11. Mhe. Salim Abdalla Hamad

Mhe. Spika, hao wote ni Wajumbe ambao walichangia katika hoja hii kwa hiyo Mhe. Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ambao wamechangia hoja hii.
Kwa hivyo, Mhe. Spika, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kunisaidia kwa kiwango kikubwa kuzitolea ufafanuzi baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe. Ufafanuzi wa mawaziri umenisaidia na hivyo kuifanya kazi yangu kutoa ufafanuzi kwa wepesi kabisa.

Mhe. Spika, napenda nikiri kwamba michango yote iliyotolewa ilikuwa ya msingi kwani kuna waliotoa ushauri, walioiuliza, kupongeza na wengine kutaka kufahamu baadhi ya mambo yaliyomo ndani ya wizara yangu. Kwa wote waliopongeza tunazipokea pongezi zao, ninachoweza kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba ushauri wote walioutoa tumeupokea na tutaufanyia kazi kwa ajili ya kuendeleza mafanikio ya wizara na maslahi ya taifa.

Kwa kuwa sitoweza kujibu hoja zote zaidi ya 200 zilizotolewa, nataka niwahakikishie wajumbe wote ambao hoja zao zimetolewa maelezo waelewe kwamba wizara yangu itazifanyia kazi hoja hizo. Katika kugusia maelezo ya hapa na pale Mhe. Spika, naomba nianze na Sekta ya Michezo.

Kwa kuzungumzia kiwanja cha michezo ni kweli hali ya viwanja vyetu ni mbaya, Kiwanja cha Mao-Tse- Tung, Kiwanja cha Gombani na Kiwanja cha Amani. Kiwanja cha Amani kilikabidhiwa wizara tarehe 19 Julai, 2010 na kilianza kutumika kwa shughuli mbali mbali za kitaifa kama ifuatavyo:-

1. Gwaride la kuapishwa Mhe. Rais wa Zanzibar
2. Gwaride la Maazimisho ya Sherehe za Miaka 47 ya Mapinduzi ya Zanzibar
3. Gwaride la Maazimisho ya Miaka 47 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Ninachotaka kusema na kuwafahamisha wajumbe ni kwamba, baada ya kufanyika mashindano mawili yaliyoandaliwa na *ZFA* majuani yote yaliyokuwa yamepandwa yalikauka na kufa na baadae kuanza kuchipuka na kuota majani ya asili. Pia uwanja ulifanyika mashimo na kupelekea kutochezeka kabisa.

Mhe. Spika, miongoni mwa sababu zilizopelekea majani kukauka na kufa kabisa ni:

1. Matumizi ya uwanja kwa gwaride
2. Ukosefu wa maji katika Uwanja wa Amani
3. Kampuni ya Fujian ya Kichina ilitoa *tender* kwa mkandarasi mdogo ambaye hana taaluma ya matengenezo ya uwanja.
4. Udongo uliorejeshwa uwanjani ulikuwa umechoka na ni ule wa miaka 41 iliyopita. Wahandisi wa Kichina walichukua zaidi ya miezi sita kuotesha majani hayo.

Hatua ambazo zinatarajiwa kuchukuliwa na uongozi wa uwanja ni:-

1. Kuchimbua uwanja na kuondosha majani yote yaliyoota baada ya yale yaliyopandwa na wataalamu wa kichina kukauka.
2. Kuongeza udongo mwengine wenye sifa za kuotesha majani katika uwanja wa mpira. Namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili anisaidie kwa hili kwani maafisa wetu wamekataliwa kuchimba udongo katika eneo husika, eneo la Kitembweni Wilaya ya Kati Unguja.
3. Kuweka *level* nakupanda majani ya asili.

Kuhusu Uwanja wa Mao-Tse-Tung Mhe. Spika, ni kweli hali yake sio yakuridhisha ingawaje bado unaendelea kutoa huduma kwa timu zetu mbali mbali kupitia Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*). Uwanja huu hivi sasa umeakabidhiwa *ZFA* na azma ya kuwapatia *ZFA* uwanja huo ni njeme tu katika kufikia malengo ya kujiunga na *FIFA*, hiyo ni moja ya masharti ya *FIFA* ni lazima chama cha mpira cha nchi kiwe na uwanja wake.

Ni kweli *ZFA* uwezo wao wa kuhudumia kiwanja hicho ni mdogo sana na tayari kamati ya Mhe. Mama Asha Bakari Makame imetushauri juu ya haja ya kukaa pamoja na kutafuta njia ya kuunusuru uwanja huu. Tayari tumeshaanza kufanyia kazi agizo hilo kwani uongozi wa wizaa yetu Kamisheni ya Utamaduni na Michezo, yaani Baraza la Michezo na Uongozi wa Taifa wa *ZFA* tumeshakutana kwa hatua ya awali. Napenda nimtoe wasiwasi Mhe. Saleh Nassor Juma pamoja na wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwamba, kazi hiyo itasimamiwa kwa karibu sana na ufanisi mkubwa ili tuweze kubadilisha mandhari ya uwanja huo muhimu katika kuleta maendeleo ya michezo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kuhusu uongozi wa *ZFA*, Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar lina wajibu wa kuvisimamia vyama vyote vya michezo na kuhakikisha kwamba vinafuata taratibu za kisheria kwa mujibu wa katiba zao na sheria Nam. 5 ya mwaka 2010 ya Baraza la Taifa la Michezo. Kila chama kinasimamiwa na katiba yake na kanuni zake na endapo ikitokea chama hicho kimekiuka taratibu zake ni haki na wajibu wa wajumbe au wanachama wake kuwasilisha malalamiko yao kwa kamati ya usuluhishi na rufaa ya chama hicho kwa mujibu wa Ibara ya 5 ya Sheria Nam. 5 ya mwaka 2010 ya Baraza la Michezo la Zanzibar.

Aidha, endapo maamuzi hayatomridhisha mlalamikaji hatua za kuwasilisha malalamiko hayo zinaweza kuwasilishwa katika kamati tendaji ya chama na hatua ya mwisho ni mkutano mkuu wa chama hicho. Na kama bado shauri hilo

halijafikiwa muwafaka, huo utakuwa ni mgogoro mkubwa na litawasilishwa BTMZ kwa kulifuatilia na kulihakikisha kwamba haki inatendeka.

Sheria hii mpya ya BTMZ inavipa vyama vyote vya michezo nafasi zaidi yakutatua migogoro au rufaa zinazohusu vyama vyao badala ya kutumika mkono wa moja kwa moja wa serikali jambo ambalo hapo awali vyama vya michezo vililalamika sana.

Aidha, suala la kuanzishwa kwa *junior academy* wizara tunalipa umuhimu mkubwa na vile vile lina nafasi kubwa ya kupatikana vipaji vya Zanzibar. Kwa sasa tunaendelea na ujenzi wa kituo cha academia ya michezo huko Dole kwa mashirikiano na Taasisi ya *Olympa Africa*. Aidha, kwa upande wa Pemba tumetenga eneo ambalo ni Gombani kwa ajili ya kujenga kituo cha kisasa kabisa kwa mashirikiano na wadau mbali mbali. Vituo hivi pia vitawezesha makocha na walimu wetu wa michezo yote kupata mafunzo na kuwa wafanisi zaidi kwa maendeleo ya michezo Zanzibar.

Kuhusu maduka ya vifaa vya michezo Mhe. Spika, ni kweli vifaa vya michezo ni ghali na kwa sasa biashara hiyo inamilikiwa na watu binafsi. Hii ni kwa mujibu wa mabadiliko ya sera za mwelekeo wa kibiashara kuelekea katika soko huria. Hata hivyo, wizara yangu inakaa na wafanyabiashawa wa vifaa hivi vya michezo na kuangalia ni kwa kiasi gani tunaweza kuwasaidia wanamichezo wetu kuvipa vifaa hivi kwa wepesi na kwa bei nafuu zaidi. Aidha tutaangalia zaidi njia nyengine ambazo zinaweza kutupatia vifaa hivyo ili kuwe na unafuu na upatikanaji wake.

Kuhusu michuano ya Kombe la Kagame ni kweli Shirikisho la Afrika Mashariki na Kati lilitupa nafasi au heshima ya kuandaa michuano hiyo, lakini kwa bahati mbaya halikufanyika Zanzibar na yamefanyika Dar-es-Salaam. Sababu kubwa ni kwamba kiwanja chetu cha Amani hakikuwa katika hali nzuri na kwa sasa tunaendelea na utengenezaji ili tuweze kukitumia kiwanja hicho kwa mashindano mengine katika muda mfupi ujao.

Mhe. Spika, kuhusu kushindwa kwa Timu ya *Basket* kushiriki ligi Dar-es Salaam, Mhe. Spika, timu hii imeshindwa kwa vile ligi ambayo ingeweza kutoa wachezaji kujiunga na Timu ya Taifa haikufanyika kutokana na vipabu kutoa pendekezo la kufanyika kwa uchaguzi kwanza wapate viongozi wapya na hatimaye washiriki katika ligi kuu na kupata timu ya taifa. Suala la uchaguzi la chama hicho pamoja na vyama vyengine nina imani linashughulikiwa vyema na kwa karibu sana na BTMZ ili kuzijengea timu hizo mazingira mazuri sana ya kujiendesha na kuendesha shughuli zao.

Mhe. Spika, nakubali kwamba Zanzibar bado kuna vipaji vingi sana vya michezo ya riadha. Chama cha Riadha Zanzibar kinaendelea na jitihada zake za kusaka vipaji vya vijana hao. Ni kweli vipaji vingi vinatoka skulini, jitihada za pamoja na BTMZ, Kamisheni ya Utamaduni wa Michezo na Chama cha Riadha, Wizara ya Elimu na wadau wengine zinahitajika katika kufanikisha suala hilo.

Katika muundo wa Baraza la Michezo Zanzibar kwa makusudi kabisa tumeweka nafasi moja ya mjumbe kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na kwa bahati nzuri nimemchagua Mkuu wa Kitengo cha Michezo cha Wizara ya Elimu kuwa Mjumbe wa Baraza kwa lengo la kupata ushiriki wa vijana wetu walioko katika skuli ambapo ndipo vipaji vya michezo vingi vinapatikana.

Kuhusu suala la mapato yanayoingia kwa *TFF* ni kweli kabisa kuwa hakuna sehemu ya fedha hizo zinazoingia katika Chama cha *ZFA* bado, muundo na katiba ya *TFF* bado hawajaonekana kuwa katika sura ya Tanzania. Uongozi wa *TFF* pamojana uongozi wa *ZFA* wanalielewa hilo. *ZFA* na BTMZ kwa busara kabisa wanaendelea na jitihada kubwa ili kuhakikisha kwamba kasoro hizo zinatoweka.

Mhe. Spika, aidha suala la *ZFA* kujiunga na *FIFA* bado limo katika mchakato mwelekeo. Jitihada za pamoja kati ya *ZFA*, *TFF* na wizara yetu bado zinaendelea. *TFF,* yaani Chama cha Soka cha Tanzania kwa mashirikiano ya *ZFA* hivi karibuni kulifanyika mawasiliano na shirikisho hilo la mpira ulimwenguni *FIFA* juu ya nafasi ya Zanzibar kupata uanachama. Kwa ihvyo, napenda niseme kwamba jitihada za makusudi kabisa bado zinaendelea na si busara kusema ama tutapata au hatupati kwa vile maamuzi hayo yanatoka *FIFA.* Niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar tuendelee kuwa na subira juu ya jambo hilo. Mimi mwenyewe binafsi kama waziri ninalifuatilia kwa karibu sana na vile vile nimeweka ahadi na Rais wa *FIFA* ili nikutane naye ili nipate ufasaha zaidi juu ya suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu suala la academia ya michezo ya Dole limefikia katika hatua nzuri tu na ya kuridhisha. Hadi sasa viwanja vya michezo mdogo midogo tayari limekwishakukamilika na kwa sasa shughuli za utandikaji njia kwa udongo inaendelea, ambapo kwa sasa tumo katika hatua ya kuwasilisha picha za vielelezo kwa wafadhili yaani *Olympa* ya *Africa* kwa ajili ya kupatiwa fedha nyengine za kuendeleza ujenzi wa jengo la ofisi.

Aidha, suala la ununuzi wa magoli kwa viwanja vyote vidogo vidogo litakuwa ni jukumu la serikali kugharamia kwani si sehemu ya makubaliano na wafadhili hao.

Kuhusu sababu za Uwanja wa Gombani kuchelewa kumalizika kwa wakati na lini utakuwa tayari. Kuchelewa kumalizika kwa *base* ya kuweka nyasi bandia kwa sababu ya mvua, mashine zilikuwa haziwezi kuchimba uwanja na kuondoa udongo na ugumu wa upatikanaji wa kokoto. Pili upatikanaji wa kokoto za kuweka kwenye *base* ya uwanja sababu mashine za kuzalisha kokoto ziliharibika katika kware zote mbili za Micheweni na Vitongoji. Kokoto zilizohitajika ni za iana tatu, nusu inchi, inchi moja na robo inchi. Baada ya matengenezo ya mashine hizo kukamilika na uzalishaji wa kokoto kwanza mambo yalikwenda vizuri na hivi sasa *base* ya kuweka nyasi bandia imeshakamilika.

Vile vile kinachosubiriwa kwa sasa ni kuwasili kwa nyasi bandia, kwa tarifa zilizotolewa na *ZFA, TFF* na Mwakilishi wa Kampuni ya HIBA Ltd. meli iliyobeba nyasi hizo tayari imeshaondoka tarehe 13 Julai, 2011 yaani kutoka Netherlands kuja Zanzibar na inategemea kuwasili mapema tarehe 1 Septemba, 2011. Kampuni inayohusika na uwekaji wa hizo nyasi hizo ni Kampuni ya Green Falts ya Netherlands.

Mhe. Spika, kuhusu uwekaji wa taa katika minara ya Uwanja wa Gombani kwana taa tayari zimeshafungwa katika minara yote minne kila mnara zimefungwa taa 40 na zote zinafanya kazi. Kuhusu eneo la kujenga hoteli eneo hilo bado lipo na halijavamiwa, bado wizara imo mmbioni kutafuta ama wawekezaji na wafadhili wa kujenga hoteli hiyo.

Kuhusu suala la ufungaji wa mtambo wa FM Pemba kazi hii imefanyika kwa mashirikiano baina ya Mkurugenzi wa STZ na Afisa Mkuu Pemba kwa vile kazi zao hufanyika kwa mashirikiano na ni kweli kuwa ofisi ya Pemba ni ofisi kiunganishi.

Mhe. Spika, Sekta ya Utamaduni imeelezwa kwamba sanaa za Kizanzibari hazionekani katika maeneo ya kihistoria. Ninachoweza kusema ni kwamba suala la kuimarisha utamaduni wa Zanzibar katika maeneo ya kihistoria hasa katika eneo la Ngomekongwe linapewa umuhimu mkubwa mno. Wizara yangu kupitia Idara ya Makumbusho imeshaamuru kuwa asilimia 50 ya vitu vya kitalii vinavyouzwa viwe vya Kizanzibari ili vitusaidie kasoro hiyo.

Mhe. Spika, kuhusu jengo la Makumbusho ya Kasri, *Palace Museum* ni kwamba kila mwaka huwa linapakwa rangi nyeupe lakini tatizo la kufutika kwa rangi hiyo kwa kipindi kifupi baada ya matengenezo halijapatiwa ufumbuzi na mamlka husika zinazofanya ukarabati huo.

Kuhusu Jengo la Makumbusho ya Mnazi Mmoja. Hivi sasa jengo hilo liko katika hatua ya kuanza kufanyiwa ukarabati na Kampuni ya *Lucky Construction Ltd* ya Dar es Salaam chini ya ufadhili wa *MACEMP*. Jumla ya shilingi 78,811,600/- zitatumika kwa ukarabati huo.

Kuhusu eneo la Unguja Ukuu jengo lilioko pale ni kwa ajili ya Makumbusho kuweka vitu vya kihistoria vilivyopatikana eneo hilo wakati wa uchimbaji. Hivi karibuni baada ya kufanyiwa ukarabati litaanza kutumika tena kwa shughuli za kimakumbusho.

Mhe. Spika, kuhusu suala la Msikiti wa Mtoni, msikiti uko chini ya milki ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale pamoja na Gofu lote la Mtoni. Hawajazuiliwa waumini kwenda kusali na wanaendelea kama kawaida.

Kuhusu suala la ukarabati wa magofu idara iko mbioni kuyakarabati magofu yake kila watakapopatiwa fedha na serikali. Mhe. Spika, katika kusimamia na kulinda maadili, Bodi ya Sensa imechukua hatua za kukutana na wenye vyombo vya habari pamoja na Tume ya Utangazaji kwa lengo la kurekebisha kasoro zilizojitokeza za mmong'onyoko wa maadili, hatua ambayo imeanza kupata mafanikio kwa kweli. Sambamba na hatua hiyo Bodi ya Sensa imeandaa ukarabati kwa kuvifanyia semina vyombo hivyo ili kutoa taaluma juu ya maadili.

Mhe. Spika, kuhusu kuhusika kwa Bodi ya Sensa katika usimamizi au utumiaji wa intaneti, bodi imeandaa utaratibu wa kukutana na taasisi inayohusika na mawasiliano hayo hapa Zanzibar kwa lengo la kulitafutia ufumbuzi tatizo hilo.

Mhe. Spika, kuhusu matamasha mbali mbali yanayofanyika Zanzibar pamoja na vikundi kutoka nje ya Zanzibar, hatua ya kuikagua sanaa zinazotumika katika matamasha hayo na vikundi hivyo zinachukuliwa na sanaa zinazobainika kutofaa kimaadili zinazuiliwa kama inavyoonekana katika kiambatisho Nam. 8 cha kitabu changu cha Bajeti.

Kuhusu matumizi ya lugha inayokiuka maadili katika Vyombo vya Habari na hasa katika redio, Bodi ya Sensa kwa kushirikiana na Tume ya Utangazaji imeanza na hatua ya kukutana na vyombo hivyo na kutoa miongozi ya jinsi ya kuondoa kasoro hizo ikiwa ni pamoja na kutotumia nafasi hizo kwa kuwazalilisha wengine. Aidha, ni hivi karibuni tu mimi binafsi pamoja na watendaji wangu nimekuwa na mazungumzo ya pamoja na *NGOs* ya Maimamu kujadili na kuweka mikakati ya kupunguza na kuondosha kabisa kasoro hizo.

Mhe. Spika, kuhusu Kamusi la Kiswahili sasa kuingizwa katika mtaala wa elimu. Kamati maalum ya Wajumbe wa Baraza la Kiswahili la Zanzibar

imekwenda kuonana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kuomba rasmi kuliingiza Kamusi la Kiswahili hasa katika mtaala wa elimu ili lipate nguvu ya kuelimisha jamii iliyokusudiwa wakiwemo vijana. Aidha, kamusi hili pamoja na vitabu vyengine vilivyoandikwa na Wazanzibari vimepelekwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa lengo la kufanyiwa tathmini ili kuona uwezekano wa kuviingiza katika mtaala wa elimu.

Mhe. Spika, kuhusu upotoshaji wa lugha ya Kiswahili unaofanywa na vyombo vya habari katika kukabiliana na suala hili, Baraza linaandaa vipindi vya kuelimisha kupitia televisheni na Sauti ya Tanzania Zanzibar. Aidha, mara kwa mara Baraza linawashauri watendaji wa vyombo hivi juu ya usahihi wa lugha wanayoitumia.

Kuhusu uendelezaji na utunzaji wa Lugha ya Kiswahili, Baraza katika kukabiliana na suala hili linaandika na kuchapisha vitabu ambavyo vimehifadhi hazina kubwa ya lugha yetu. Vimechapisha kamusi vitabu vinavyozungumzia utamaduni wa Mzanzibari, tunafanya mashindano ya uandishi na fani mbali mbali nakuandika kumbukumbu za wasanii na kazi zao. Hivi sasa kamusi la Kiswahili fasaha limeshafika sehemu mbali mbali ndani na nje ya Zanzibar na juhudi zaidi ya kulisambaza zinaendelea.

Mhe. Spika, ukodishaji wa ukumbi wa Bwawani. Zabuni za ukodishaji wa ukumbi huo ulitangazwa kwenye Gazeti la Zanzibar Leo katika matoleo yake ya Disemba 23, 24 na 25, 2010. Kampuni zilizojitokeza katika *tender* hiyo ni nne ambazo ni: *Star Time Promotion, Zanzibar Media Co-operation, National Marketing Ltd na Prime Time Promotion.* Katika kinyang'anyiro hicho kampuni ya *National Marketing Limited* ndio iliyoshinda kwa kukodishwa ukumbi huo kwa shilingi 15 milioni kwa kila mwezi.

Uchambuzi. *Star Time Promotion,* tathmini iliyofanywa ilionesha kwamba kampuni hii imesajiliwa Zanzibar tarehe 15 Julai 2010 na ina leseni ya biashara iliyotolewa tarehe 27/12/2010. Vile vile kampuni imejisajili kulipa kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *TRA* yenye *TIN* Nam. 110-533-349. ni kweli kampuni iliweka kiwango cha zabuni ya shilingi 35 milioni kwa mwezi lakini ilishindwa kutokana na kwamba haikuweza kuwasilisha uwezo wake wa kifedha. Aidha, ilionekana leseni yake na usajili wake ni wa karibuni kabisa kiasi ya kuonekana wazi kwamba, kampuni hiyo iliundwa kwa ajili ya kuingia kwenye zabuni tu.

Zanzibar Media Co-operation, kampuni iliweka kiwango cha zabuni ambacho ni shilingi 17 milioni, kampuni hii ilionekana kuwa imesajiliwa Zanzibar mnamo tarehe 13/07/2005 na imesajiliwa kama ni mlipa kodi wa Bodi ya Mapato Tanzania yenye *TIN* Nam. 106-436-533 tarehe 13/02/2008. Aidha,

imesajiliwa kama ni mlipa kodi wa *Zanzibar Revenue Board* yenye Nam.07000933000 iliyotolewa tarehe 8/09/2008. pia kampuni imeonesha uzoefu wenye kufanya kazi kuhusisha na upigaji wa disko mafano, *Zanzibar Tigo Music*. Hata hivyo, kampuni iliyowasilisha ripoti ya ukaguzi wa mahesabu ya kampuni ambao ulionesha wazi kwamba haina uwezo wa kumudu kulipa fedha hizo yaani shilingi 17 milioni.

National Marketing Limited. Kampuni hii iliweka kiwango cha zabuni hii ni shilingi 15 milioni kwa mwezi. Kampuni ilionesha kuwa imesajiliwa Zanzibar tarehe 6/05/2006, imewasilishwa kuwa ni mlipa kodi halali kwa Bodi ya Mapato Tanzania (*TRA*) yenye *TIN* Nam. 165-645-546 tarehe yake ni 1/06/2007. Vile vile imethibitishwa na kupewa leseni ya biashara ya vileo na Mahkama tarehe 4/8/2010. kampuni iliwasilisha uzoefu wa miaka 10 wa kupiga disko katika ukumbi wa *Komba Disco*, Swimming Pool, Fuji na kadhalika. Kampuni hii ilionesha kuwa na uwezo wa kulipa shilingi 15 milioni kwa kuwa na rasilimali nyingi ikiwemo umiliki wa *Amani Bungalow*.

Prime Time Promotion. Kampuni hii nayo iliweka zabuni ya shilingi 15 milioni, iliwasilisha vyeti vya kuwa amesajiliwa kibiashara Tanzania Bara tarehe 25/04/2002, imesajiliwa kama ni mlipa kodi halali wa Bodi ya Mapato Tanzania (*TRA*) mwenye *TN* Nam. 100-676-230 na *VAT* 10-013988-2 tarehe 1/1/2001 pamoja na kuwasilisha wadhamini wa benki kama vile *SBL* lakini haikuonesha uwezo wake wa kifedha.

Hivyo Bodi ya Zabuni ilifikia uamuzi wa kukodishwa ukumbi huo *National Marketing Ltd* kwa kuweza kutimiza vigezo vyote vilivyotolewa katika zabuni hiyo. Katika ukodishaji huo ilibainika kwamba sehemu zote zilikuwa katika hali mbaya kuanzia kuta, milango, madirisha *tiles* na hata kwenye kuta za kuzuaia sauti isitoke nje. Mkodishwaji alikadiriwa matengenezo makubwa yafanyike katika sehemu hiyo. Kitathmini gharama za matengenezo hayo zilikadiriwa kufikia shilingi 60 milioni, hivyo katika kukubaliana na mkodishaji huyo wa ukumbu kwa mujibu wa mkataba ilifikiwa kodi ya kila mwezi iwe ni shilingi 15 milioni ambapo kiasi cha shilingi 40 milioni zilipaswa kulipwa kwa kipindi cha miaka mine na shilingi 20 milioni zitumike kwa ajili ya gharama za ujenzi kwenye ukumbi husika.

Aidha, malipo mengine yalifanyika kwa kipindi cha miezi mine kwa mpango kama huo katika awamu ya pili na ya tatu kwa kuhusisha pia ujenzi kwenye *swimming pool*. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba kazi ya matengenezo hayo itaanza mwezi ujao wakati wa kipindi cha Mfungo wa Mwenzi wa Ramadhani.

Kuhusu suala la *Legal Status*, hadi sasa Serikali ya Awamu ya Saba haina mpango wa kuifanya Hoteli ya Bwawani kuwa ni shirika, bali ina mpango wa kuimarisha hoteli hiyo pamoja na eneo lote lililopo Bwawani chini ya nadharia ya mradi utakaoleta tija zaidi kwa serikali yaani *Intergrated Resort Project System*. Tayari kamati maalum ya kusimamia utekelezaji wa dhana hiyo imeundwa chini ya uongozi wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kimsingi ndio maana watumishi wa hoteli hiyo wakaamuliwa kuajiriwa chini ya Idara ya Utumishi na Uendeshaji ya wizara. Aidha, nadharia ya kuunganisha Chuo cha Maendeleo ya Utalii na Bwawani limesitishwa kutokana na ukweli kuwa yapo matumaini makubwa kujitegemea kwa choo baada ya ufadhili wa *ADB* kukubalika rasmi kama hotuba yangu ilivyobainisha.

Kuhusu suala la hoteli kuwa na hatimiliki ya eneo lake, tayari shauri hilo lmeshawasilishwa kwa Mamlaka husika ya Idara ya Upimaji na Mipangomiji. Tumefuatilia na taratibu zinaendelea kufanyiwa kazi.

Kuhusu suala la wadaiwa sugu wa kodi za ofisi. Hoteli imechukua hatua za makusudi za kuwaandikia barua za ukumbusho na tayari wengi wao wameshaanza kulipa madeni yao. Wadaiwa wote ni 13 lakini wadaiwa sugu kwa tafsiri kuwa hawajafikia kulipa angalau asilimia 50 ni watano ambao nitawataja ni:-

1.	OSAJU COMPOUND ambao wanadaiwa	shilingi	3,750,000
2.	ZANZIBAR SAFARI ambao wanadaiwa	shilingi	2,600,000
3.	BREAK ENTERPRISES wanadaiwa	shilingi	2,750,000
4.	MODESTY TOUR wanadaiwa	shilingi	2,650,000
5.	ZFA ambao wanadaiwa	shilingi	2,400,000

Kuhusu suala la kodi ya kampuni ya *Rock Cafe.* Ni kweli kodi iliyolipwa kwa sasa ni ndogo lakini hata hivyo, hoteli imejipanga kuongeza kodi hiyo katika mkataba mwengine utakaofungwa ambao unamalizika mwezi wa Oktoba mwaka 2011.

Kuhusu athari za mmong'onyoko wa ardhi Hoteli ya Bwawani tayari taasisi yangu imechukua hatua za kuwasilisna na Shirika la Bandari kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi suala hilo.

Mhe. Spika, katika Hoteli ya Bwawani Baraza lako tukufu limeomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 8,000,000/-. Matumizi haya yanatokana na makusanyo ya shilingi milioni milioni 890 yanayopatikana katika hoteli hiyo.
Kuhusu Shirika la Utalii linalipwa kodi ya dola 3,500 kwa mwezi kwa Kisiwa cha Changuu badala ya dola 8,000 walizokuwa wakikusanya kabla ya kukodisha kisiwa hicho. Mhe. Spika, ninachotaka kueleza hapa ni kuwa

ukodishwaji wa Kisiwa cha Changuu ni miongoni mwa miradi mikubwa ya uwekezaji kwa Zanzibar ambayo inaidhinishwa na Mamlaka ya Uwekezaji *(ZIPA).* Kinacholipwa shirika ni dola 3,500 kwa mwezi lakini ziko kodi nyengine zinazolipwa kutoka kwa mwekezaji zikiwemo kodi ya ardhi, ongezeko la thamani na kuchangia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kutokana na uajiri wa wafanyakazi. Malipo hayo ya ziada yanalipwa kwa taasisi nyengine zinazohusika.

Hivyo, wazo la kukirejesha kisiwa hicho mikononi mwa shirika kwa sasa haliwezi kutekelezwa kutokana na mkataba uliofungwa wa muda mrefu wa miaka 33 kati ya serikali na mwekezaji.

Mhe. Spika, kuhusu ukarabati wa jengo la Livingstone kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 44 wa kitabu cha bajeti ilikuja Kampuni ya *Royal Institution of Charter Survey* ya Uingereza kwa nia ya kusaidia ukarabati wa jengo hili na kuahidi kwa hatua za mwanzo kuleta mtaalam wao kwa ajili ya kufanya utafiti. Kama tujuavyo jengo hili ni la *gazetted monument.*

Halikadhalika Mamlaka ya Uendelezaji Mji Mkongwe ni Mshauri Mkuu kwa vile moja ya vigezo vinavyofanywa Zanzibar kupata hadhi ya kuwa *World Heritage Site* ni pamoja na jengo hili ambalo lilitumiwa na mvumbuzi huyu maarufu kwa kuanzia misafara yake ya uvumbuzi. Hivyo, ukarabati wake ni lazima uwe wa kitaalam. Hata hivyo, wizara ina nia ya kutafuta mbia ili kulikarabati jengo hilo na kulitumia kibiashara kama ilivyoelezwa.

Mhe. Spika, kuhusu shirika kutokuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Mhe. Spika, ni kweli shirika halina bodi tangu kumalizika kwa mwaka 2007 mwezi Oktoba kwa kuwa serikali ilikuwa na maamuzi ya kulifunga shirika hilo. Kuanzia muda huo shirika limekuwa likipokea maamuzi kutoka wizara mama na kama nilivyoeleza katika hotuba yangu kwamba hivi sasa utafiti wa kitaalam wa kuendelea na kufutwa kwa shirika hilo umefanyika na *research* yake iko wizarani kwa hatua zinazofuata.

Kuhusu mali za shirika kuchukuliwa. Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza kwamba mmiliki wa mali zote za serikali na mitaji ya umma maamuzi ya kuhaulisha mali hizo hutolewa na taasisi hiyo na lazima itekelezwe. Hoja hii inakwenda sambamba na suala la uuzwaji wa magari ya shirika basi na *hiace* ambayo yameuzwa kwa mujibu wa maelekezo ya Ofisi ya Mitaji ya Umma na Uhakiki wa Mali.

Nyumba za Chwaka. Kwa mujibu wa hati za mmiliki nyumba hizi mbili zilizopo Chwaka zinamilikiwa na Shirika la Utalii, hivyo kufuatia agizo la

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mwaka 1997 aliamuru nyumba hizi zikabidhiwe Serikali ya Mkoa wa Kusini Unguja.

Kuhusu deni la *Royal Star* shirika limewasiliana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kwenda kulifuatilia deni hilo na hivi karibuni wanasheria watakwenda kutekeleza kazi hiyo.

Shirika la Utalii limekusudia kukusanya kiasi gani. Mhe. Spika, shirika limekusudia kukusanya kiasi cha shilingi milioni 275,280,000 kwa mwaka wa fedha 2011/12 na limeomba kupatiwa idhini ya kutumia kiasi cha shilingi milioni 245,440,000 ili kuendeleza shughuli zake.

Kuhusu hadhi ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni ya kitaifa au kimataifa. Mhe. Spika, chuo hichi kiko kitaifa kwa sababu kimeanzishwa kisheria kwa mujibu wa Sheria Nam. 7 ya mwaka 2008 ya Baraza la Wawakilishi na wahitimu wake wanafanya kazi katika taasisi mbali mbali za kitalii zilizomo nchini kwa kutumia vyeti walivyopata chuoni.

Pia chuo kinatambulika na *Matrix* ambayo ndicho chombo kikuu cha taifa chenye kutathmini taaluma za Vyuo vya Ufundi Tanzania. Chuo kinafanya matayarisho ya kutambulika kimataifa, matayarisho hayo yanahusiana na mashirikiano na Shirika la Utalii na ukarimu la Uingereza yaani *Confederation of Tourism and Hospitality.*

Mhe. Spika, *CTH* ni shirika linalosimamia mafunzo ya utalii na ukarimu katika vyuo vinavyoendesha fani hiyo duniani. Kwa hivyo, hii ni daraja ya diploma ya juu inafundishwa kwa mwaka mmoja tu. Chuo kinaendelea na kozi hizi kwa majaribio na mkupuo wa mwanzo wa wanafunzi kumi ulifanya mitihani ya *CTH* mwezi wa Juni mwaka 2001 na hivi sasa wanaendelea na utafiti. Wahitimu wa kozi hii wataweza kupata ajira kwa nafasi za uongozi katika taasisi za utalii. Pia chuo kitafanya mapitio ya mihutasari yake katika mwaka huu wa fedha chini ya mtaalam kutoka Nertherland ili kuiweka mihutasari hiyo katika hadhi ya kikanda na ya kimataifa.

Kuhusu mwelekeo wa chuo, hivi sasa chuo kinatoa mafunzo ya cheti na stashahada. Mwelekeo ni kutoa mafunzo ya juu zaidi ya stashahada ya Uzalishaji Mali pamoja na Uzamili, pia shahada ya Uzamivu na kufanya tafiti mbali mbali zinazolenga kuikuza sekta ya utalii. Malengo hayo yataelekezwa kadri nyenzo zitakavyokuwa zinapatikana.

Kuhusu hali ya wafanyakazi, chuo hivi sasa kina walimu wa kutosha katika kufundisha ngazi ya cheti lakini kina upungufu wa walimu wa kufundisha ngazi ya stashahada. Ili kuziba pengo hili chuo kinawatumia walimu wa muda

(part time) kutoka katika vyuo vikuu vya hapa Zanzibar. Chuo kina mpango wa kuwaendeleza walimu na wafanyakazi wake kwa kupitia nyenzo za chuo chini ya mradi wa *ADB* unaotarajiwa kuanza mwaka ujao wa fedha 2012 na Mradi wa Lishe unaotarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha 2011.

Mhe. Spika, hoja ya chuo kuwa katika hali mbaya na wanafunzi kusoma chini ya miti. Ni kweli tatizo hilo lilikuwepo kabla lakini sasa limerekebishwa chini ya kauli mbiu ya kuleta mabadiliko. Tunamuomba Mhe. Mwakilishi atembelee vyuo hivi na aone hali halisi ya vyuo.

Kuhusu mikakati juu ya wahitimu wa chuo. Tunadhania kuwa hoja hii jawabu yake iko katika Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Kuhusu uvamizi wa eneo mbali na mazungumzo ya mdomo, chuo kilimuandikia barua rasmi mwekezaji kumtaka aondoe mabaki ya boti mbovu aliyoyatupa maeneo ya chuo na kurejesha eneo la chuo alilovamia katika hali yake ya kawaida. Mwekezaji alijibu barua hiyo baada ya muda mrefu. Baada ya barua hiyo Kamati ya Uongozi ya Chuo ilifanya kikao cha dharura tarehe 12 Julai, 2011 saa 3:00 asubuhi ili kujadili barua iliyojibiwa na mwekezaji wa *Maruhubi Beach Village*. Baada ya majadiliano chuo kilikuja na maamuzi na msimamo wa kumtaka mwekezaji aondoe mabaki ya maboti mabovu aliyoyatupa katika eneo hili la chuo.

Kufuatia zaidi katika Idara ya Mazingira kuhusiana na suala la kifusi na udongo aliomwaga eneo la ufukwe wa chuo, ili kwanza kujua iwapo eneo la fukwe si la mtu yeyote kama ilivyodaiwa na mwekezaji. Kifusi na udongo aliomwaga hauleti madhara yoyote ila unahifadhi mmong'onyoko.

Sehemu ya usawa ya gofu lililomo ndani ya chuo kwa sheria ni mali ya chuo au ni mali ya Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale. Mhe. Spika, shinikizo la kumtaka mwekezaji aondoe mabaki yake ya boti mbovu aliyotupa katika eneo la chuo limefanyika na tayari mabaki hayo yameshaondolewa.

Ufuatiliaji wa suala la kifusi na udongo katika ufukwe unafanyika na umeanza na Idara ya Mazingira. Mhe. Spika, chuo kilipeleka ombi katika idara hiyo kuomba wataalam waje waliangalie eneo la pwani la chuo. Idara ya Mazingira imeleta ripoti yake ambayo imegusia athari za kitendo cha umwagaji wa udongo na kifusi katika eneo la ufukwe. Kinachoonekana hivi sasa ni mwekezaji huyu kuondoa kidogo kidogo kifusi na udongo alioujaza sehemu ya ufukwe iliyopo katika eneo la chuo. Mhe. Spika, chuo kinaangalia kuona hatima ya kazi hiyo inayofanyika.

Msimamo baada ya kuona hatima ya uondoaji wa udongo huo chuo kinatafuta ushauri wa kitaalam wa jinsi ya kulihami eneo lake kwa njia ambayo haitaleta madhara.

Kuhusu mapato ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii. Mhe. Spika, chuo hichi licha ya kupatiwa ruzuku na serikali pia kinakusanya mapato kutoka vyanzo vyake mfano ada za wanafunzi, huduma za jamii na shughuli mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 chuo kimetarajia kukusanya jumla ya shilingi milioni 211 kutoka katika vyanzo vyake.

Kuhusu unyanyasaji wa wafanyakazi wa Kizanzibari na uongozi wa mahoteli. Mhe. Spika, ni kweli kwamba kuna malalamiko ya wafanyakazi yanayotokana na *PO* kutoka nje ya Zanzibar. Hata hivyo, suala hili linatakiwa lishughulikiwe zaidi na Kamisheni ya Kazi kuwa ndio wenye mamlaka ya kisheria. Aidha, wizara yangu iko katika kuyafanyia kazi malalamiko hayo kwa kushirikiana na wizara hiyo iliyohusika.

Suala la ajira kwa Wazanzibari katika Sekta ya Utalii. Mhe. Spika, suala hili limeonekana na linafanyiwa kazi kwa kufanya mapitio ya kisera ya utalii. Sambamba na hilo, kwa nia ya kuwajengea uwezo vijana wetu Chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii tayari kinatoa mafunzo katika ngazi ya stashahada yaani diploma, ili kuondokana na kisingizio cha uwekezaji kuwa Wazanzibari hawana sifa na uzoefu wa kuajiriwa na kushika nafasi za utawala. Aidha, suala hili pia lilizungumzwa vyema na Mhe. Haroun Ali Suleiman wakati wa hotuba yake.

Kuhusu hoteli ya *Blue Bay* kuwa na wafanyakazi wengi wa kigeni. Mhe. Spika, suala la kuajiriwa katika mahoteli tunaendelea kulifanyia kazi kwa kushirikiana na wizara inayohusika na mambo ya ajira.

Kuhusu suala la kupatikana kwa wawekezaji wengine wa hoteli ya *Venta Club.* Mhe. Spika, naomba Waheshimiwa Wajumbe wawe na subira kwani suala hili limeundiwa kamati maalum kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais na linafanyiwa kazi ipasavyo.

Kuhusu kupotosha historia kwa watembezaji wageni kwa watalii. Mhe. Spika, watembezaji watalii wanaopewa vibali na Kamisheni ya Utalii kabla ya kutoa kibali hicho watembezaji hao hupatiwa mafunzo maalum ya utembezaji watalii kutoka katika Chuo chetu cha Maendeleo ya Utalii. Mafunzo hayo hujumuisha miongozo ya utembezaji, historia na maadili. Tunaamini kwamba watembezaji hao wanapata maadili ya kazi zao ambayo ni pamoja na kutoa historia sahihi ya Zanzibar.

Aidha, limejitokeza kundi la watembezaji watalii wasio rasmi maarufu kama ni mapaparazi. Hawa hawana elimu ya utembezaji wala vibali vya kufanyia kazi hiyo. Hivyo, kundi hili ndilo linalopotosha historia ya Zanzibar. Kwa hivyo, wizara itaendelea kukabiliana na kundi hili kwa lengo la kubadilisha mwelekeo wake.

Kuhusu faida ya utalii wa makundi *(package tour)* naomba kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba utalii wa makundi ni mfumo unaotumika duniani kote. Hapa Zanzibar juhudi kubwa zimetumika kupunguza utalii wa aina hiyo kulinganisha na miaka ya 90 ambapo kwa Zanzibar ilikuwa ni asilimia 90 wakati Tanzania Bara ilikuwa asilimia 85. Hivi sasa utalii wa makundi umeshuka na kufikia asilimia 65 kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

Aidha, tafiti zinaonesha kwamba bado utalii wa makundi matumizi yao yako juu kiasi cha wastani wa dola za Kimarekani 209 kwa siku, wakati watalii wa kujitegemea matumizi yao ni wastani wa dola 190 za Kimarekani kwa siku. Utafiti huu pia husaidia wakati wa majanga kubakisha hadhi ya nchi *(country image)* kama ilivyotokezea wakati wa kuporomoka kwa uchumi wa mwaka 2009, mripuko wa maradhi ya mafua ya ndege mwaka 2004, tukio la ugaidi la kuripuliwa Balozi za Marekani mwaka 1998 na kuripuliwa kwa majengo ya kibiashara nchini Marekani mwaka 2001. Safari hizi ambazo zinatayarishwa na mawakala husaidia sana kuitangaza nchi yetu kiutalii.

Mhe. Spika, pamoja na faida hizo aina hii ya utalii huipatia nchi mapato ya viza, mapato yatokanayo na uegeshaji wa ndege, mapato yanayotokana na utoaji wa ndege, ajira kwa mawakala, biashara za huduma mbali mbali za ndani na husaidia mzunguko wa ndani wa fedha kwa wananchi.

Kuhusu hoja ya kufanya *tour* na wageni. Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Sheria ya Utalii ya mwaka 2009 imekataza kazi za uongozaji wageni kufanywa na wageni. Hata hivyo, kadhia hiyo ilikuwepo na ilizungumzwa katika kikao cha pili cha Baraza la Biashara la Zanzibar na kupewa jukumu Kamisheni ya Utalii, Jumuiya ya Utembezaji Watalii na Jumuiya ya Wawekezaji Watalii kulifanyia kazi.

Katika kulifanyia kazi suala hilo jumla ya vikao vinne vilifanyika na kukubaliwa kwamba kazi hiyo ifanywe na *tour operators* tu. Ili kuhakikisha hilo hatua za kuweka katazo katika leseni za mahoteli limefanyika na kutoruhusu kufanya kazi hiyo na kutoa onyo na adhabu kali kwa wanaokwenda kinyume na hatua hiyo.

Kuhusu utozwaji wa vibali kwa *tour operators.* Mhe. Spika, kamisheni inatoa leseni na vibali kwa waongozaji watalii. Leseni ni kwa ajili ya mradi

kuruhusiwa kufanya biashara ya utalii kwa mujibu wa Sheria ya Utalii ya mwaka 2009 na kibali hutolewa kwa gari inayotoa huduma kwa watalii, lakini kibali pia husaidia katika usalama wa wageni.

Kuhusu suala la uvujaji wa mapato ya watalii kutoka Uwanja wa Ndege na Bandarini. Mhe. Spika, napenda kueleza kwamba suala la mapato katika maeneo hayo linahusiana na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na Wizara ya Mambo ya Ndani kupitia Idara ya Uhamiaji.

Kuhusu hoja ya uporomokaji wa maadili. Mhe. Spika, napenda kueleza kwamba hakuna utafiti uliofanywa unaoonesha utalii unachangia kwa kiasi kikubwa kumong'onyoka kwa maadili. Suala la kumong'onyoka kwa maadili halihusiani moja kwa moja na utalii, kwani kuna mambo mengi yanayosababisha kumong'onyoka kwa maadili ikiwemo suala la utandawazi na kukua kwa sayansi na teknolojia.

Matumizi mabaya ya mtandao, kupatikana kwa *channel* mbali mbali za televisheni ambazo baadhi yake hazifai kwa maadili yetu, matumizi mabaya ya simu za mikononi na hata baadhi ya magazeti. Hata hivyo, wizara yangu kupitia Kamisheni ya Utalii huwa inatoa muongozo kwa mawakala wa safari, watembezaji watalii mahotelini na watalii wenyewe kuhusu kivazi na yale yote ambayo hayastahiki kufanywa na wageni wanapokuwepo nchini.

Kuhusu kufanyika utafiti wa vitu vinavyozalishwa Zanzibar na kutumika mahotelini. Mhe. Spika, napenda kueleza kuwa ufadhili wa Ubalozi wa Norway kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii ilifanya utafiti wa kutathmini mnyonyoro wa tathmini ya utalii *(very thin analysis).* Hii ilikuja nani anafaidika vipi na utalii na ilibainika kuwa bidhaa za matunda, mboga mboga na samaki ndizo zinazotumiwa kwa wingi katika mahoteli ambazo kwa asilimia kubwa zinatoka ndani ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Sekta ya Habari nianze na mada ya kuchelewa kufika vipaza sauti. Mhe. Spika, Idara ya Habari Maelezo haijawahi kuchelewa kupeleka vipaza sauti katika shughuli yoyote labda iwe taarifa hiyo imechelewa kutufikia.

Mhe. Spika, kuhusu hatimiliki ya picha ya Rais, Idara ya Habari Maelezo haijapiga picha inayotumika hivi sasa ya Mhe. Rais kwa hivyo haina hatimiliki wala mamlaka ya picha hiyo. Kwa mujibu wa sheria za hatimiliki mwenye mamlaka ya hatimiliki ni yule tu aliyefanya kazi hiyo.

Kuhusu juhudi zilizochukuliwa kuanzisha magazeti ya binafsi. Mhe. Spika, sheria iko wazi kwa mtu yeyote anayetaka kuanzisha gazeti la binafsi na

hakuna anayezuiliwa ili mradi afuate sheria. Mhe. Spika, kupitia Baraza hili nawaomba wananchi wanaotaka kuanzisha gazeti waombe.

Mhe. Spika, katika kuliweka wazi suala hili napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa wapo watu binafsi walioanzisha magazeti binafsi kama vile gazeti la Nipe Habari ambalo limesajiliwa Zanzibar.

Kuhusiana na wafanyakazi wa Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa kazi za uchapaji wa gazeti la Zanzibar Leo. Mhe. Spika, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wajumbe kwamba shirika limefanya malipo yote katika uongozi wa Kiwanda cha Upigaji Chapa na haina deni lolote linalotokana na wakati ambao magazeti ya shirika yalipokuwa yakichapishwa kwa *black and white* kwenye kiwanda hicho kabla ya kuanza kuchapishwa Dar es Salaam kuanzia Septemba 1, 2010.

Mhe. Spika, hoja ya uchakavu na kutokuwa na haiba ya kuvutia kwa jengo la ofisi ya Shirika la Magazeti ya Serikali ambalo ni jengo la zamani la STZ. Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mjumbe katika kutekeleza hayo fedha za ukarabati mkubwa wa jengo hilo zimetengwa tayari kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2011/2012. Katika kuhakikisha hilo tayari hatua zimechukuliwa na kampuni kadhaa zimeshawasilisha zabuni zake za kuomba kufanya kazi ya ukarabati huo ambapo baada ya bajeti kupitishwa bodi itaendelea na taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, napenda kukubaliana pia na hoja ya Mhe. Mjumbe kwamba kutokuwepo mtambo wa kuchapisha magazeti yake hapa Zanzibar ni changamoto kubwa kwa Shirika la Magazeti ya Serikali kufikia lengo la kujitegemea.

Mhe. Spika, magazeti ya shirika kwa sasa yanalazimika kuchapishwa Dar es Salaam kutokana na kutokuwepo mitambo ya kusafishia magazeti hapa Zanzibar hadi sasa. Gharama za uchapishaji magazeti hayo kwa sasa ni shilingi 693,521,000 kwa siku sawa na shilingi 20,805,642,000 kwa mwezi ambazo ni shilingi 249,667,704 kwa mwaka ambazo ni fedha nyingi.

Wizara yangu imeliona tatizo hilo na imechukua hatua mbali mbali za kuandika miradi ya kuomba kusaidiwa mitambo ya uchapishaji, pamoja na kuandika mradi wa shilingi milioni 800 na kuuwasilisha Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ili iingizwe katika miradi ya wizara yangu kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2011/2012 ambapo tungeweza kununua mtambo wa *recondition* kuchapisha magazeti. Lakini kutokana na uhaba wa fedha mradi huo haukuweza kupatiwa fedha. Hivyo, matarajio ni kuomba tena katika

mwaka ujao wa fedha iwapo kipindi hicho kutakuwa bado hakujapatikana mtambo mwengine.

Katika suala la madeni ya Shirika la Magazeti Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Mwakilishi kwa kuonesha kuwa kweli ni Mjumbe wa Bodi ya Shirika hili la Magazeti ya Serikali. Nakubaliana na ushauri wake kwamba umefika wakati madeni ya taasisi za SMZ kwa shirika hili kulipwa moja kwa moja na wizara inayohusika na Fedha kupitia bajeti yao, ikiwa ni hatua ya kulisaidia shirika hili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi ambapo mbali ya kuwa bado ni changa linahitaji fedha hizo kwa ajili ya kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Kuhusu suala la maslahi ya wafanyazi wia Sekta ya Habari hasa waandishi na wapiga picha wanaokuwepo wakati wa Baraza lako tukufu likiendesha vikao vyake. Wizara yangu inathamini sana juhudi za wafanyakazi wake hasa wakati wa urushaji wa matangazo wakati Baraza lako tukufu likiendelea na vikao vyake. Hata hivyo, suala la maslahi kwa wafanyakazi haliko kwa waandishi na watangazaji tu bali liko kwa wafanyakazi wote wa serikali. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kulijua hili hivi sasa liko katika utaratibu wa kufanya mapitio na kuweka muundo mpya wa maslahi *(scheme of service)*, kazi hiyo imeshaanza kupitia Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, hata hivyo, wizara kwa kuthamini nguvu za wafanyakazi wake hasa wanapokuwepo hapa Barazani huwalipa shilingi elfu tano kwa siku kwa kila mfanyakazi. Kiwango hichi ni kikubwa zaidi ya kile wanachostahiki kwa mujibu wa kanuni za utumishi. Kulingana na taratibu za utumishi wafanyakazi hawa wanapaswa kulipwa shilingi elfu tatu kama malipo baada ya saa za kazi. Vyenginevyo walipaswa kulipwa shilingi elfu kumi kama ni posho la kazi maalum ambapo kwa mujibu wa kazi wanazozifanya hapa Barazani kiwango hicho kilipaswa kulipwa na Baraza la Wawakilishi ambapo kwa bahati mbaya limeeleza halina kifungu cha kufanya malipo hayo.

Mhe. Spika, mbali na posho hilo la shilingi elfu tano kwa siku linalotolewa, wizara hupatiwa huduma za nguo rasmi kwa wafanyakazi wanaoshiriki kurusha matangazo katika kipindi cha shughuli za Baraza.

Kuhusu kupungua kwa kodi za minara. Mhe. Spika, hali hii imetokana na wateja wengi wa zamani kujenga minara yao wenyewe na kupunguza mapato ya shirika.

Mhe. Spika, kuhusu tenda ya ununuzi wa mitambo ya *digital*. Mhe. Spika, mitambo ya urushaji wa matangazo ya TV ambayo imeagizwa imenunuliwa na

fedha zinazotokana na msamaha wa madeni kwa Tanzania. Utumiaji wa fedha hiyo unasimamiwa na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pekee. Mhe. Spika, pamoja na hali hiyo, wizara yangu imeshirikishwa kikamilifu katika kutoa aina ya vifaa na vigezo vya kitaalam vinavyohitajika.

Kuhusu ubora wa vipindi vyetu. Mhe. Spika, ni kweli kwamba ubora wa vyombo vyetu TVZ na STZ unatokana na vipindi na uendeshaji wake yaani *constant presentation.* Kwa kuzingatia umuhimu huo Shirika la Utangazaji limeunda kamati maalum kupitia upya vipindi vyote kulingana na matakwa ya wadau, pia utamaduni na silka za nchi. Kazi hiyo bado inaendelea kwa kufuata taratibu na kwa uangalifu.

Hoja ya uchache wa idadi ya vipindi vinavyotengenezwa. Mhe. Spika, idadi ya vipindi vilivyotengenezwa ukilinganisha na nyenzo zilizopo sio mbaya. Hata hivyo, muhimu zaidi ni ubora wa vipindi badala ya kuvitafutia tu vibali.
Kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili fasaha. Mhe. Spika, wizara kupitia Shirika la Utangazaji itatoa kipaumbele juu ya utumiaji wa lugha fasaha ili kuwa mfano mzuri wa kuigwa na vyombo vyengine. Wizara inasisitiza ushirikiano zaidi na Baraza la Kiswahili la Zanzibar.

Kuhusu uteuzi wa viongozi wastaafu. Mhe. Spika, shirika linaamini kwamba uteuzi huo umefanywa kwa makusudi hasa ukizingatia uzoefu na elimu za wateule. Kiwango cha umri wa kustaafu kwa miaka 55 ni ya hiari na miaka 60 ni ya lazima bado inamuwezesha mteule kufanya kazi kwa ufanisi.

Kuhusu TVZ kutokuzingatia maadili kuwepo mambo hadharani. Mhe. Spika, shirika litazidi kuzingatia maadili, silka, mila na utamaduni wa Mzanzibari na pale hali hiyo itakapojitokeza hufanyika kutokana na hitilafu za mitambo.

Mhe. Spika, kuhusu kutokuwepo huduma za uhakika suala hili linatokana na kukatika mara kwa mara kwa umeme na uchakavu wa mitambo pamoja na vitendea kazi vyengine.

Mhe. Spika, shirika litakapopata mitambo mipya litajitahidi na litajidhatiti kwenda sambamba na taaluma za mitambo hiyo. Katika kuzingatia hilo, Shirika la Utangazaji linatoa kipaumbele kwa mambo yafuatayo:

(a) Kutafuta na kutayarisha mafunzo ya muda mfupi na mrefu juu ya usalama wa teknolojia ya kisasa *(digital).*
(b) Kuomba wataalam watakaofundisha na kusimamia matumizi ya teknolojia mpya kutoka nchi zinazoendelea.
(c) Kuwatumia mafundi kutoka kampuni zinazotoa vifaa.

(d) Kufunga mitambo mipya na kutoa elimu kwa wafanyakazi kama itakavyofanyika katika mitambo iliyonunuliwa.

Kuhusu hoja ya kutokuwepo kwa majenereta. Mhe. Spika, bahati nzuri shirika lina majenereta katika vituo vyake vyote ili wakati hukosa mafuta ya kuendeshea jenereta hizo.

Mhe. Spika, kuhusu kutokuwepo sheria ya kuanzisha shirika. Mhe. Spika, uundwaji wa taasisi mbali mbali za serikali upo katika mamlaka ya madaraka ya Mhe. Rais, Shirika la Utangazaji lilitangazwa na Mhe. Rais alipounda Idara katika Wizara mbali mbali, baada ya kuundwa huku, kilichopaswa kufanyika ima kuletwa mswada katika Baraza la Wawakilishi au kuanzishwa kwa kutumia na kutengeneza kwa *legal notes*, hatua iliyofanyika ni kuliunda shirika hilo kwa kutumia *legal notes* ambayo ipo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mazingatio ya mwisho.

Mhe. Spika, shirika linategemea kufunga mitambo hiyo kuanzia tarehe 25/07/2011 kama ilivyopangwa. Hata hivyo ufungaji wa huo unategemea ukamilishaji wa vifaa vyote vinavyohusika. Hadi sasa shirika limeshapokea mitambo ya urushwaji wa matangazo na linaendelea kukamilisha utaratibu wa utowaji wa mitambo ya kudhibiti umeme yaani AR vilivyopo bandarini Unguja kwa mashirikiano ya Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ya Zanzibar. Pia inasubiri kupokea a*ntennal* na *fader* ambavyo hivi sasa bado vipo bandarini Mombasa.

Mhe. Spika, kuhusu hoja ya kutokuwa na taaluma ya kutosha ya mpangilio wa vipindi shirika linawapangiliaji wa vipindi wenye taaluma. Hata hivyo, shirika litaendelea litaendelea kuwapatia taaluma zaidi wafanyakazi hao.

Vile vile kutokuwepo vipindi vya tamthilia. Shirika linatarajia kununua vipindi hivyo kulingana na bajeti. Kuhusu kutokuwepo mkalimani wa walemavu wasiosikia. Shirika limekusudia kulipatia ufumbuzi tatizo hilo. Kuhusu kutokuelewana kwa viongozi wa shirika. Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba ndani ya Shirika la Utangazaji Zanzibar hakuna ugomvi wa aina yoyote miongoni mwa viongozi wake, kwani shirika limetayarishwa na kupitisha muundo yaani *organization chart* ambayo imegawa majukumu kwa wahusika wote bila kuwepo kwa migongano kati ya viongozi na wahusika wenyewe.

Mhe. Spika, kuhusu kuwepo kwa taarifa za habari ambazo ni fupi. Shirika limekusudia kuongeza taarifa za habari hizo mara tu mitambo itakapokuwa mizuri. Kuhusu *roving reporter*. Kwa sasa tuna upungufu mkubwa wa vitendea kazi, ikiwemo usafiri. Tutarudisha kipindi hicho mara tu

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, naona waziri anakaribia kumaliza baada ya muda mchache sana. Kwa hivyo, tumpe nafasi ya kumsikiliza kwa makini ili tuweze kumaliza shughuli hii kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika. Kuhusu *roving reporter* kwa sasa tuna upungufu mkubwa wa vitendea kazi, ikiwemo usafiri. Tutarudisha kipindi hicho mara tu hali itakapokuwa nzuri. Mhe. Spika, kuhusu vyuo vya serikali vya Zanzibar kuwa na sauti moja. Mhe. Spika, napenda kumfahamisha Mhe. Mohammed pamoja na Baraza lako tukufu kuwa hivi karibuni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imeunda kamati ya kuangalia uwezekano wa kuviunganisha vyuo vya serikali kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Zanzibar yaani *SUZA*, baada ya hapo kamati itapendekeza vyuo ambavyo vipo tayari na vimetimiza vigezo vilivyowekwa kuunganishwa kuwa sehemu ya chuo hicho. Hali hiyo itasaidia vyuo hivyo kuwa na sauti kama alivyopendekeza Mhe. Mohammed.

Mhe. Spika, kuhusu Chuo cha Uandishi wa Habari kufundisha lugha za kigeni. Mhe. Spika, pendekezo la kufundisha lugha za kigeni limezingatiwa na litafanyiwa kazi hatua baada ya hatua, kutegemeana na ukuaji wa chuo na upatikanaji wa walimu wanaoweza kufundisha vizuri lugha hizo. Hata hivyo, tumeamua kuanza na lugha ya Kichina kutokana na umuhimu wake kwa sasa kama ilivyoelezwa kabla.

Mhe. Spika, kuhusu utaratibu wa vyuo vya Uandishi wa Habari. Chuo chetu cha Habari ni mdau kama wadau wengine katika tathmini ya utoaji wa taaluma, nacho kinapaswa kuratibiwa kama vingine na kamwe hakina jukumu la kuratibu shughuli za vyuo. Suala la kuratibu ubora wa vyuo halihusiki na chuo chetu wala Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Utaratibu wa vyuo vyote kwa hapa Zanzibar uko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, Mhe. Subeit Khamis Faki, alizungumzia kuhusu uhusiano kati ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *TCRA* na Wizara yetu ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ndio yenye jukumu la kusimamia masuala yote ya mawasiliano ya *electronic* ikiwemo simu, posta na utangazaji. Kwa kuwa utangazaji sio katika mambo ya Muungano, Tume ya Utangazaji Zanzibar ndio iliyopewa jukumu la kusimamia sekta ya utangazaji kwa upande wa Zanzibar. Mamlaka ya Tanzania ina mahusiano mazuri na wizara yangu kwa kupitia Tume ya Utangazaji Zanzibar na imekuwa ikishirikiana vyema na watendaji wa tume katika kuendeleza sekta

ya utangazaji ikiwemo kushirikishwa katika upangaji wa mawimbi ya kutangazia.

Mhe. Spika, kuhusu mapato ya *TCRA*. *TCRA* inakusanya mapato kutokana na ada ya leseni za wanaotoa huduma za mawasiliano katika Tanzania nzima. Mapato yanayokusanywana *TCRA* Zanzibar yanatumika kuendeshea shughuli za mamlaka hii kwa nchi nzima. Suala hili la mapato linapaswa kushughulikiwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Kwa upande wa Zanzibar mapato yanayopatikana kutokana na matumizi ya mawimbi ya kutangazia yanakusanywa na Tume ya Utangazaji Zanzibar. Napenda kulijulisha Baraza lako tukufu hili kwamba Zanzibar ina mamlaka kamili kwa mawimbi yake ya kutangazia na hakuna malipo yoyote yanayokwenda *TCRA* kwa matumizi ya mawimbi ya utangazaji.

Mhe Spika, Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kupitia Sauti ya Tanzania Zanzibar, swali la Mhe. Fatma Mbarouk alitaka kuelewa hali ya rangi na gugu mbele ya Kituo cha STZ Rahaleo. Jibu ni kwamba jengo tayari limekwishawekwa rangi na linapendeza na hali ya gugu tayari imeshashughulikiwa. Swali la kuwepo kwa vipindi vyenye kuhamasisha na kuendeleza Serikali ya Mapinduzi yenye Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Jibu ni kwamba vipindi tayari vipo vinaendeshwa chini ya ufadhili wa Marekabi katika programu inayoitwa *Search Common Ground* na hivi sasa vimekuwa vikiendelea kwa muda wa zaidi ya ya miezi mitatu na hususan katika utayarishaji wa taarifa ya habari.

Mhe. Spika, fedha zilizotolewa na Wachina kwa kodi ya Uwanjani Hoteli zilitumika kufanya ukarabati mkubwa wa hoteli hiyo pamoja na ununuzi wa samani zilizomo ndani ya hoteli hiyo. Mhe. Spika, kuhusu suala la uwekaji nyasi bandia katika uwanja wa amani, limepokelewa na litafanyiwa kazi. Mhe.Spika, msaada huu wa nyasi bandia umeletwa na *FIFA* kwa Tanzania ndipo *TFF* ukaleta Zanzibar na unathamani ya dola laki 450,000 za Marekani na Zanzibar tulichangia bilioni 1.8. Mhe. Spika, ushauri tumeupokea na kuwapa mafunzo wafanyakazi wa redio ya Micheweni na tayari mfanyakazi mmoja tumempeleka Chuo cha Uandishi wa Habari Unguja.

Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alitaka maelezo juu ya taarifa ya kuwepo fedha za Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar. Jumla ya bilioni 92 ambazo zimechukuliwa na wizara katika mwezi wa Disemba 2010. Mhe. Spika, wizara haifahamu kuwepo kwa kiwango hicho cha fedha za chuo ambacho kimechukuliwa, ikizingatiwa kwamba bajeti nzima ya chuo kwa mwaka uliopita ni milioni 120 ambayo ni ruzuku kutoka serikalini. Aidha, fedha za maendeleo zilikuwa ni milioni 30. Kuchukuliwa kwa fedha nyingi kama hizo, kungemaanisha kuzuwia kwa harakati za utendaji chuoni hapo, ikizingatiwa

kwamba chuo bado ni kichanga. Hata hivyo, katika mwezi huo wa Disemba mwaka 2010 ruzuku ya milioni 10 ya chuo hicho ilichelewa kutolewa, lakini baadae iliwasilishwa na kutumiwa kwa utaratibu uliopangwa.

Mhe. Spika, natumai huo ndio mwisho wa majibu yangu. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, sasa Waheshimiwa Wajumbe niwahoji, wale wanaokubaliana na hoja ya makadirio haya anyanywe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu utaratibu kidogo. Miongoni mwa taasisi za Wizara hii ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo ni Shirika la Utalii. Lakini kwenye hiki kitabu kikubwa hakuna kifungu kinachohusiana na matumizi ya shirika hili. Je, Mhe. Mwenyekiti, kama sikuridhika na maelezo au majibu ya Mhe. Waziri naweza kumbana kwa kutumia kifungu gani. Naomba muongozo wako.

Mhe. Spika: Inavyotokea masuala ya mashirika kama hayo na unataka uweke hoja. Nenda kwenye lile eneo ambalo na mshahara wake Mhe. Waziri.

FUNGU 31 KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201	Utawala Unguja	842,000,000
	Jumla ya Fungu	**842,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0501	Sauti ya Tanzania Zanzibar	30,000,000
Kifungu 0601	Idara ya Televisheni Zanzibar	80,000,000

Mhe. Mjumbe Fulani: Mjumbe fulani, alipiga buti hapa lakini alichelewa kidogo kupiga buti wala hakutajwa jina lake.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe ulisahau kidogo, lakini kuna maeneo mengine utayatafuta huko, maana hii ni mapato tu tunayakusanya.

Kifungu 0701	Idara ya Habari Maelezo	23,800,000
Kifungu 1001	Idara ya Utamaduni	17,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho	170,000,000
	Jumla ya Fungu	**370,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 31 KAMISHENI YA UTALII

Kifungu 0201	Utawala Unguja	671,989,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	137,011,000
	Jumla ya Fungu	**809,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, UTALII NA MICHEZO

Kifungu 0201

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba katika uendeshaji wa wizara kuna wakurugenzi, yaani kuna idara na kuna wakurugenzi. Sasa hizi idara na mkurugenzi wake anakuwa ameenea baina ya Unguja na Pemba kwa Zanzibar nzima. Sasa wizara ilionesha kwamba Sauti ya Tanzania Zanzibar, utekelezaji wake umefanywa na afisi kuu Pemba. Sasa ndio nikataka Mhe. Waziri aeleze. Alitoa maelezo hapa lakini hakueleza ni kwa nini kifungu kile basi kikawekwa chini ya Afisi Kuu Pemba, kama alivyoeleza katika *paragraph* yake kwamba Afisi Kuu Pemba ni ofisi ya uratibu. Kwa hivyo, jambo hili linaweza kama halikutekelezwa basi linaweza likawaondoshea dhamana wale wakurugenzi wakajiona wao ni wafanyakazi wa sehemu ya Unguja tu, lakini sehemu ya Pemba kuanzia uendeshaji, utekezaji

wa nafasi za kazi za wale watu walioko chini yao yaani *human resource development* yote ikaondolewa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atupe ufafanuzi kidogo hili lilikuwa ni koseo na halitarejewa au ilikuwa ni kitu gani hasa. Kwa sababu matumizi ya Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar, ilikuwa yaoneshwe kwenye Sauti ya Tanzania Zanzibar, yaani katika Shirika la Utangazaji. Naomba tupate ufafanuzi wa Mhe. Waziri kidogo.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri kila idara inakuwa na matumizi yake. Kwa hivyo, tulivyoeleza achukuwe hivyo, asichukuwe tafsiri nyengine yoyote kila idara inakuwa na matumizi yake kama kawaida. Naomba nimjibu hivyo tu.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi sijamfahamu Mhe. Waziri. Kwa sababu hizi idara zinapotangaziwa zinatangaziwa na mkurugenzi na mkurugenzi anakuwa ni wote kutoka Unguja mpaka Pemba. Sasa yuko Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar ameenea na idara yake, sasa matumizi ya idara yakafanywa popote hayaonekani chini ya ile idara ambapo wizara zote ndivyo zinavyofanya. Haioneshi kuwa Ofisi Kuu ya Pemba kazi yake ni *coordination*, kwa hivyo kutakuwa na fungu lile linalohusu mambo ya utawala na mambo mengineyo. Sasa tunamuomba Mhe Waziri awe *clear* kidogo hapa.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri pamoja na kwamba mkurugenzi anakuwa anaenea kwa Unguja na Pemba, lakini yale mafungu huwa tunayagawa, haya ni ya Pemba na haya ni ya Unguja. Kwa hivyo, Pemba wanakuwa wana matumizi yao mbali na Unguja wanakuwa na matumizi yao, pamoja na kwamba mkurugenzi anaenea, lakini tumeyagawa makusudi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe asiwe na wasi wasi kuhusiana na matumizi haya. Tumefanya hivyo kwa kuelewa nini tunachokifanya. Aelewe kwamba Pemba wana matumizi yao na Unguja wana matumizi yao, wala hakutokuwa na maingiliano yoyote pamoja na kwamba mkurugenzi anaenea kotekote, lakini tumeyagawa hivyo. Namuomba Mhe. Mjumbe alielewe hivyo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana naye kwamba matumizi yanafanywa mbali mbali kwa mujibu wa ule mradi unavyokwenda. Lakini lile fungu huwa liko chini ya ile idara inayohusika ndio utakapoweza kujua. Sasa namuomba sana Mhe. Waziri aende akakae tena na timu yake, bajeti inayokuja basi aturekebishie mambo haya, bila ya hivyo, tunastawi upya wake tu. Lakini Mhe. Spika, mimi nisingekubali kabisa

maelezo yake, kwa sababu hayatoshelezi hasa. Lakini ajuwe kwamba tunaendelea lakini mimi sikutoshelezeka kabisa na maelezo yake. Nawaomba sana timu yake ikakae tena kitako ifikirie ni njia gani za kuwasilisha bajeti katika bajeti ijayo, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilihoji suala zima la uagizishaji wa vifaa vile vya mitambo ile ya *digital* kwa ajili ya TVZ na nikasema katika maswali ambayo tuliwahi kuuliza humu humu Barazani. Mhe. Waziri mwenyewe aliwahi kutuambia na akalithibitishia Baraza kwamba iliagizwa kwa jina la mtu binafsi na sio kwa jina la taasisi ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilimtaka Mhe. Waziri atutajie hilo jina la Afisa huyo. Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako ndio linalosimamia matumizi ya fedha za walipa kodi, kwa msingi ule wa no *taxation without representation*. Sasa haiwezekani fedha za walipa kodi zikawa zinachezewa kama hivi kwa kiukwa taratibu za fedha na kanuni zake halafu tukawa hatupati majibu. Nilikuwa namuomba Mhe. Waziri atutajie, huyu Afisa ambaye mitambo hii aliiagizishia kwa jina lake, ili Baraza hili zima la kusimamia fedha za walipa kodi lipate kujua na baadae liona linaweza kuchukua hatua gani. Naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimueleze tu kwamba katika ununuzi wa vifaa hivi kwa kweli tulishirikishwa kikamilifu na tulitekeleza wajibu wetu. Sisi tulichotakiwa ni kutaja vifaa gani tunavihitaji na *specification* ya vile vifaa vyenyewe. Tunajua kwamba mamlaka ya ununuzi wa masuala hayo yote yanahusiana na Wizara ya Fedha na tunajua aliyehusika na hili ni Afisa kutoka Wizara ya Fedha. Nani anaitwa siwezi kumjua kwa kweli kwa sababu yalifanywa na Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mjumbe labda apeleke madai yake haya kwa Wizara ya Fedha ili kutaka kujua ni nani hasa. Sisi tumeutekeleza ule wajibu wetu, ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, siridhiki kabisa na majibu ya Mhe. Waziri. Wizara ya Fedha inaweza kuwa imechukua jukumu hilo, lakini tungeyafahamu kama ingekuwa ni Wizara ya Fedha iliyonunua. Yeye mwenyewe Mhe. Waziri. Nafikiri hata katika Hansard ataiona. Alitujibu humu ndani kwamba ni kweli, akithibitisha madai yetu kwamba ni kweli imenunuliwa kwa jina la mtu binafsi hata kama ni mfanyakazi wa Wizara ya Fedha, huo sio utaratibu Mhe. Mwenyekiti, wa kiserikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu yake haya kwamba yeye hamjui, itanipa mashaka juu ya usimamizi mzima wa shughuli zilizokuwa katika wizara yake.

Kwa sababu mitambo hii ilikuwa imeletwa kwa ajili ya matumizi ya Idara ya Televisheni na ilikwama uwanja wa ndege kwa muda mrefu, na Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Asha Bakari alituthibitishia humu ndani, kwamba ilibidi mpaka kukwamua na gharama baadae, ililetwa kwa jina la mtu binafsi lakini gharama zikaambiwa ni za serikali za kubakia pale uwanja wa ndege.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, huu utaratibu wa kuwalinda na kuwaficha watu wanaokiuka taratibu za fedha za walipa kodi katika nchi yetu utaendelea mpaka lini. Tutajiwe Mhe. Mwenyekiti hilo jina vyenginevyo bajeti hii tutaikwamisha. Naomba sana tutajiwe jina la mtu huyu ili tutakapokuja tena ikiwa ni kwa wizara hii au Wizara ya Fedha tutajua nini cha kufanya kama wawakilishi wa wananchi. Lakini pasiwe na taratibu za kulindana kabisa Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, vifaa hivi vya Televisheni Zanzibar, vilinunuliwa na serikali kwa njia za kutumia pesa za misamaha zile za MDRI. Kiutaratibu sisi pesa ile hatuigusi, sio Afisa wa Wizara wala sio Afisa wa Wizara ya Fedha, sisi tunakamilisha taratibu na serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha ilishirikiana bega kwa bega na Mkurugenzi aliyekuwa wa Televisheni na wizara yenyewe wakatafuta *specification*, kila kitu na tukapeleka Wizara ya Fedha Dar es Salaam, kisha Benki Kuu ndio wakalipa hizo fedha. Kwa hivyo, sio ofisi aliyeshughulika kwa jina labda fulani, labda waliyoshughulika pale ni yale mabarua tu yale kule na huku. Lakini pesa sisi hatukuigusa. Kwa hivyo, pesa zile zimenunuliwa na kutumia pesa zile za *MDRI*, huo ndio utaratibu uliotumika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mengi yaliyotolewa, bado hayajajibu hoja yangu. Inawezekana kabisa fedha zikawa zimetoka na msamaha wa madeni. Nazungumzia kwamba uthibitisho ambao umetolewa na kamati yako. Vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, tuambiwe kwamba kamati ilidanganya na kama ilidanganya na Baraza hili likaridhika na serikali na mawaziri wakaridhika kwa sababu wakati ule hawakuikanusha.

Kama nilivyosema iko Hansard, Mhe. Waziri mwenyewe wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo alituambia kwamba ni kweli ililetwa kwa jina la mtu na ni Afisa wa Wizara ya Fedha, alituambia yeye humu ndani. Lakini jina alituambia hamjui.na hata kwenye majibu yake mimi sifikiri kama alishirikishwa na wala kwenye mchango wangu sikusema kama alishirikishwa au vipi, isipokuwa nilichokizungumza ni kuhusu suala zima la utaratibu kufuatwa kwamba haiwezekani mali ya serikali kuagizwa kwa jina la mtu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, twende katika hiyo *point* na wala tusizunguke, kwamba fedha za misamaha ya madeni kuna utaratibu wake na anashirikishwa, kwa sababu sizungumzi ushirikishwaji wala chanzo cha fedha hizi. Kwa hivyo, jambo nilinalolizungumza ni kuhusu utaratibu wa manunuzi ya serikali kwamba umefanywa na jina la mtu binafsi na huo si utaratibu Mhe. Mwenyekiti.

Kwa kweli naomba sana katika hii Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuwa atutajie. Lakini kama serikali inahisi kamati ilidanganya au sisi tumetoa taarifa ambazo si sahihi basi tuunde Kamati Teule hapa kwa mujibu wa Kanuni za Baraza kwa ajili ya kwenda kuchunguza suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hili tunataka liwe funzo na hapa si hapala pale tu, lakini zipo taarifa hapa kwamba hata hili janareta la Baraza la Wawakilishi limechukuliwa na kuletwa tu hapa, wakati Baraza la Wawakilishi ni chombo ambacho Katiba inakilinda na wala halikushirikishwa kwa mujibu wa taratibu zake. *(Makofi)*
Sasa kumekuwa na utaratibu huu wa manunuzi ya ajabu na wala huko tusiende si wakati wake umeshapita, lakini sasa tunajadili hii mitambo ya *television*, tuambiwe Mhe. Mwenyekiti jina la afisa huyu tumjue hapa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ikiwa kama kuna makosa kwenye taarifa baina ya iliyotolewa na kamati au sisi Waheshimiwa Wajumbe ama Waheshimiwa Mawaziri, basi tuunde Kamati Teule kwa ajili ya kwenda kuchunguza ukweli wa suala hili, kwa hiyo naomba sana suala hili vyenginevyo bajeti hii sitoipitisha. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu anataka jina lililotumika liletwe mbele ya Baraza lako tukufu lililoagiza vifaa. Kwa hivyo, nataka nimhakikishie Mhe. Mjumbe aipe muda serikali kulifuatilia jambo hili tuweze kujua ni nani na baadaye jina hili liweze kuja katika Baraza lako tukufu.

Aidha kuhusu janareta kwa kuwa Baraza la Wawakilishi haina bajeti ya janareta hili. Kwa kweli tuliiomba serikali kutokana na hali halisi ya matatizo yaliyojitokeza ya humu ndani hasa ya uzimwaji wa umeme na tukakubaliana kwamba lipatikane janareta. Kwa hivyo, tuliiomba Wizara ya Fedha isaidie kutupatia najareta na ndio maana Wizara ya Fedha ilichukua dhima hiyo ya kulilipia janareta na kutupatia janareta hilo.

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Mjumbe atusubirie tupitishe bajeti yetu hii ya Wizara ya Habari na baadaye tutafuatilia jina hilo na tutalileta mbele ya Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu kabisa hoja ya Mhe. Mjumbe. Ukweli ni kwamba pale palikuwa na *officer* mmoja wa *External Finance* ndiye aliyekuwa akishughulika na mambo haya yote.

Kwa hivyo, mara nyingi na ninaamini nafikiri kwa sababu amesema kitu na Mhe. Waziri amekiwasilisha kwenye kamati basi labda huyo *officer* alitumia jina lake wakati mwengine kwa ajili ya kurahisisha yale mawasiliano. Lakini haina maana kwamba ile mali ni yake au yeye pengine fedha za serikali itatumika vibaya. Sasa hilo nikiri kama imefanyika hivyo ni kosa na hilo tutalifuatilia, kwa ajili ya kulirekebisha na lisitokee tena.

Mhe. Mwenyekiti, nakiri ni kweli alikuweko *officer* mmoja ambaye ndiye alikuwa full *responsible* anayekwenda mbio kwa kushughulika na haya na yeye ndio kama *linkmen* wa wizara zote kwa *purchasing* na wala sio huko. Kwa mfano, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha yenyewe, Wizara ya Ardhi. Kwa hivyo, kweli kiuratatibu si utaratibu mzuri na hili Mhe. Mwenyekiti tutalirekebisha lisiweze kutokezea tena. Ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sijui mawaziri au serikali kwa ujumla wake wana hofu gani kumtaja huyo mtu kwanza tutajiwe kwa jina. Pili hoja zilizotolewa Mhe. Mwenyekiti zinanisikitisha na ninasema watatufikisha pahala mawaziri tuseme maneno ambayo hatupendi kuwambia kabisa. Mhe. Mwenyekiti, sipendi watufikishe pahala tuseme kwamba serikali hii si makini, kwa sababu tumeshaisifu sana tokea tumeanza bajeti hii.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, anaponiambia kwamba tuwape muda walitafute jina na hoja hii niliitoa jana Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli nilimwambia Mhe. Waziri kwamba wakati ule ulituambia jina hulijui, lakini leo unao muda wa kutosha kwenda kulitafuta mpaka kesho, hivyo masaa 24 hayajatosheleza kwa serikali ambayo ni makini kutupa jina la *officer* wake ambaye anashughulikia masuala hayo.

Pili Mhe. Mwenyekiti, kuambiwa kwamba hizi kauli wananchi zinawachosha, kwa sababu hizi fedha ni za walipakodi, kwamba serikali inafuatilia, iachiwe, itashughulikia majibu haya yameshawachosha wananchi.

Kwa hivyo, nasema naweza kukubali kwa hoja moja tu, kwanza tutajiwe jina la huyu *Officer* wa *External Finance* hapa, yaani jina lake tunaomba. Pili serikali ituambie kama Mhe Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amekiri ni kukiuka kanuni kama amefanya hivyo.

Kwa kweli hizi kauli za kwamba anarahisisha utaratibu kwa kukiuka utaratibu sisi Baraza lako hatukubali hata siku moja, kwa sababu *otherwise* itakuwa Katiba, Sheria, Kanuni tunazozipitisha hapa hazina maana yoyote, kama mtu anaweza kutafuta njia yake ya urahisi na urahisi huo ni urahisi gani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, serikali ni taasisi sasa kama inaagiza kitu basi iagize kwenye taasisi yake inayohusika sio kwa jina la mtu binafsi, analipia wapi huyu kutoka kwenye mfumo wake bila ya shaka ni kutoka fedha za serikali katika kulipia, kwa nini isitajwe ile taasisi.

Kwa hivyo, ninasema hivi Mhe. Mwenyekiti, hakuna ugumu wowote wa kuagizia kitu kwa jina la taasisi, tena nafikiri itakuwa na *credibility* zaidi taasisi ya serikali inapoagiza kitu kwa jina la taasisi, yaani inatoa *credibility* zaidi kwa yule anayeuza kuliko mtu binafsi, kwa hivyo haiwezi kuwa inarahisisha Mhe. Mwenyekiti. Kwa kweli hapa lazima kuna harufu ya mchezo mchafu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba tutajiwe jina hilo na wala sio jina tu, halafu nikubali kuipitisha kwa kuambiwa tu, kwamba serikali kupitia Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakiri kuwa kufanya hivyo ni kukiuka kanuni, basi tuambiwe serikali itamchukulia hatua gani *officer* huyo.

Otherwise kama hatukubalini katika hilo, basi naomba Baraza lichukue *role* yake na iunde kamati, kwa ajili ya kwenda kutafuta kumefanyika nini na lipendekeze kwenye Baraza hili, nini hatua za kuchukuliwa kwa maafisa kama hawa wamekuwa hawazionei uchungu fedha za walipa kodi, *ICU* haitengenezwi na machupa ya gesi yanakaa chini na fedha zinachezewa kama hivi, hivyo hatuwezi kukubali hata siku moja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimhakikishie Mhe. Mjumbe kwamba huyu *officer* hakutenda kosa kwa utaratibu tuliokuwa nao au tunaokwenda nao yeye alikuwa ni kama *facilitator*, yaani ana-*act* kwa niaba ya Katibu Mkuu anaandika zile barua pamoja na *transaction* zao mabarua anakwenda *BoT* na Wizara ya Fedha, yaani ana-*act on behalf of government*.

Kwa hivyo, *officer* mwenyewe ni *External Finance* anaitwa ndugu Ramadhan bila ya kuficha yeye ni *officer* na wala hakukamata fedha *cheque* wala chochote, isipokuwa yeye anakwenda kwenye taratibu. Sasa kama ilikuwa kosa kutumia jina lake kwenye hizo taratibu basi hilo tunakubali tutalirekebisha, ili ilisitokezee tena.

Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Mjumbe, anahisi kidogo utaratibu ni kinyume basi hilo tubakubali na huo ndio ukweli wenyewe, yaani hivyo ndivyo mambo

yanavyokwenda. Kwa kweli si rahisi kwa sababu kule alikuwa anakwamba *BoT* na Wizara ya Fedha inabidi aende *physical*, yaani anaonana na maofisa wenzake pengine inatakiwa saini, kwa hiyo anatia pale kwa niaba ya Katibu Mkuu, kwa sababu yeye ni *Senior Officer* pale wa *External Finance*, lakini hakushika *cheque*, fedha mkononi wala chochote.

Sasa kama hilo ndilo kosa basi nakiri ni kweli hilo limefanyika na ninamuahidi Mhe. Mjumbe tutalirekebisha, lakini huo ndio uliokuwa utaratibu na umesaidia sana kufanikisha. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tutafikishana pahala mpaka tuseme tutumie kanuni tupige kura. Lakini ninachosema kwamba namheshimu sana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na mwenyewe amesema kabla kama ilitendeka hivyo ni kosa alisema yeye. Sasa majibu yake ya pili anasema kwamba haijakiuka utaratibu. Kwa hivyo, ni kosa su si kosa Mhe. Mwenyekiti.

Pili narejea tena kusema kuwa mimi siamini kwamba ukitumia lugha gani ya *facilitation* kwamba Kanuni zetu za Fedha za *Procurement* popote zinaruhusu zinaruhusu mtu kwa jina lake kununua mali kwa niaba ya serikali sikubali Mhe. Mwenyekiti, *unless* wanitajie wapi katika Sheria za *Procurement* pamoja na Kanuni za Fedha zinaruhusu kufanya kitu kama hicho. Kwa hivyo, sikubali Mhe. Mwenyekiti, hivyo nasema tuambiwe.

Kwa kweli katika maelezo yake ya mwanzo alipokuwa anatusaidia mwenyewe amesema kwamba kama imefanyika hivyo itakuwa ni kosa, nilisema hapa waziri alituthibitishia na kamati pia ilithibitisha kuwa ndivyo ilivyofanyika.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikiambiwa hapa kwamba Wajumbe wa Kamati walipoliuliza swali hili hata hiyo lugha iliyotumika na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji ndugu Hassan Mitawi alipobanwa alijibu akasema kwamba kuna *deal* nyengine huko sisi huwa hatushirikishwi, yaani alitumia neno *deal*. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba huu utaratibu wa tukikibali humu ndani Baraza kwamba mambo haya tuyaachie yaande hivi kwa maelezo ya jumla ya mawaziri tu, ndipo tunapolea utendaji mbovu katika serikali, kwa sababu kama hatuchukui hatua Mhe. Mwenyekiti wewe ni mwanasheria, yaani kama hakuna adhabu katika ukiukaji kwa sheria, basi sheria zitakuwa hazina mamana na wala hakuna mtu anatayekuwa na *incentive* ya kuzitekeleza.

Kwa kweli sheria zinakuwa na nguvu endapo mtu anapojua ikivunjwa kunakuwa na adhabu, sasa huyu mtu amekiuka. Kwa hivyo, lugha ya

kuambiwa kwamba hakukiukwa utaratibu isipokuwa ame-*facilitate*, una-*facilitate* kulikuwa na ubaya gani kusema mitambo hii hata kama imenunuliwa na Wizara ya Fedha na kama taratibu za serikali zinasema kwamba Wizara ya Fedha ndio mnunuzi, basi ilikuwa itajwe pale ni Wizara ya Fedha na serikali itafanya utaratibu wake.

Kwa hivyo, wakati wa kuzitoa Wizara ya Fedha itakuwakilisha *officer* wake akazitoe na huo ndio utaratibu. Sasa mimi sione *facilitation* gani iliyokuwa ikifanyika hapa, lazima kuna kitu hapa.

Kutokana na hali hiyo, ndio maana ninasema serikali ichague mawili ama tuunde kamati ikachunguze ukweli huu au hapa serikali yenyewe na mimi naipa *option* hii ambayo ninaipenda zaidi kwamba serikali itwambie humu ndani, yaani serikali iji-*commit* baada ya kututajia jina, basi huyu mtu atachukuliwa hatua kwa taratibu zao kwa yale mambo ambayo ameyakiuka Kanuni za Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kama sivyo nisiendelee kupoteza muda wa Baraza lako Kanuni yetu hapa inaruhusu kama fungu siridhiki nalo basi tupige kura kifungu cha 96 (6) (g) kinaruhusu hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tusiendelee kupoteza mdua hapa kama serikali hairidhiki na mapendekezo yetu, basi tupige kura na Wajumbe waamue kwamba tunaridhika kupitisha matumizi haya ambayo kila siku yanavuruga matumizi ya fedha za walipakodi, naomba sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, suala liliopo ni kwamba huyu *officer* wa Wizara ya Fedha ndugu Ramadhani, yeye alikuwa ni *facilitator* kama ilivyozungumzwa na katika shughuli zake hizo alikuwa ana-*shuttle* baina ya Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania.

Kwa hivyo, tujue kwamba katika Benki Kuu hawaruhusu kununua kitu chochote cha fedha zozote isipokuwa lazima kuwe na utaratibu wa *tender*. Hivyo, *tendering* zilikuwepo kwa watu watatu na akapatikana mmoja ambaye ndiye aliyeleta hivyo vifaa. Sasa kama kuna utaratibu ambao ulikiukwa, ambapo serikali tunahisi kuwa hakuna utaratibu uliokiukwa kwa sababu ya hiyo *tendering*.

Kwa maana hiyo, *Bank of Tanzania* wasingeliweza kukubali kununua hizo kwa fedha hizo za wafadhili mpaka ule utaratibu ukamilike. Sasa nafikiri kama kuna shaka hiyo, basi mimi ninasema tutachunguza na tayari tumeshamtaja kwamba ni ndugu Ramadhani, ikiwa kuna makosa yaliyotendeka au yaliyofanywa na

ndugu Ramadhani, basi hatua za kiserikali kwa mujibu wa utaratibu tutazichukua. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza niseme bado sikubaliani na maelezo ya serikali na sasa ili nisiendelee kupoteza muda wako wa Baraza hili Kanuni ya 49 (4) (j) katika hoja ambazo zinaweza kutolewa bila ya kutoa taarifa Mhe. Mwenyekiti, ni hoja ya Kuunda Kamati Teule na iko ukurasa wa 36.

Kwa hivyo, naomba nitoe hoja katika Baraza lako kwamba Waheshimiwa Wajumbe watukubalie tuunde na mimi kwa kifupi nasema hivi kwa sababu siamini nasema wazi Mhe. Mwenyekiti, kwamba serikali katika hili ina nia ya kulishughulikia suala hili, kwa sababu mengi yanakuja na tunapewa majibu kama haya. Kwa hivyo, nasema Mhe. Mwenyekiti, katika hili Baraza lina *role* yake kwa mujibu wa Katiba pamoja na Sheria za nchi linayo mamlaka yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja hiyo bila ya kutoa taarifa kwa kutumia Kanuni ya 49 (4) (j) kuomba kuamua tuamue kuhusu kuunda Kamati Teule ya Baraza kwa ajili ya kwenda kuchunguza kadhia nzima kama hizo taratibu zilifuatwa kama kulikuwa na *tendering*, ilikuwaje, ali-*facilitate* au alikuwa na chake, baada ya kuridhika, kama alivyowahi kusema Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kama hakuna mchezo mchafu kamati itabaini, baada ya kamati kubaini itakuja kuliridhisha Baraza kwamba hakuna mchezo mchafu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kila mtu atakuwa clean na wananchi wataondosha wasi wasi ambao wanao. Mhe. Mwenyekiti, naomba tutumie Kanuni hiyo ulihoji Baraza lako tukubaliane kuunda Kamati Teule, ili ikachunguze kadhia nzima ya Mitambo hii ya *Digital* ya TVZ. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuamua hoja kuna Waheshimiwa Mawaziri wawili wanataka kusaidia suala hili. Kwa hiyo, tuanze na Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum).

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba unisaidie kwa uwezo au uzoefu wako, hivi ombi likitolewa kwanza linajadiliwa kabla ya kuamuliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nilisema kabla ya kuamua hoja. Kwa hivyo, tuwasikiliwe Waheshimiwa Wajumbe wetu hawa na kimsingi hoja kama hiyo inabidi turudi katika Baraza. *(Makofi)*

Unless otherwise useme hutaki maelezo zaidi.

Mhe. Haji Faki Shaali (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, nadhani kabla ya kwenda mbele anavyozungumza Mhe. Mjumbe mwenzangu mimi ninamuomba atusaidie kitu kimoja angekuwa muwazi zaidi na yeye, yaani angekwenda katika utaratibu wa Kanuni zetu za Baraza na yeye pia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, angetuambia ni sheria ipi au kifungu gani kilichovunjwa katika huo utaratibu mzima uliofanyika, lakini hajatuambia ni sheria gani iliyovunjwa wala kifungu cha sheria ambacho kimevunja. Sasa huwezi kuunda Kamati Teule wakati yeye mwenyewe hajasema ni sheria ipi ya mwaka gani, tena kifungu gani kilichovunjwa. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, kwanza unapotaka kuzungumza hoja maelezo yako katika mjadala unaelezea kwamba mimi ninaazma ya kuwasilisha hoja.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo Mhe. Mjumbe hakuwaki kusema hayo na hoja hiyo imeibuka hapa na hata kama imeibuka hapa basi unatakiwa useme kwa mujibu wa Kanuni na utaratibu, kwamba natoa hoja hii na kwa sababu kuna sheria fulani kifungu namna kadha zimevunjwa hajatuambia Mhe. Mjumbe.

Suala jengine Mhe. Mjumbe tumemwambia serikali inasema kwamba huyo mtu ni Ramadhani na pili italifuatilia hilo na halafu itaripoti katika Baraza kama kuna sheria yoyote iliyovunjwa basi itaripoti katika Baraza. Sasa hapo itakaporipoti wao au kamati ama mjumbe yeyote anayo haki ya kujadili kusema kwamba hii hatuikubali au tunaikubali.

Vile vile na yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe alisema mwanzo kwamba atakuwa tayari ikiwa serikali itaji-*commit* kusema kwamba hatua zitachukuliwa. Kwa hivyo, sisi tunasema kuwa tutatizama ikiwa imekwenda kinyume na utaratibu, basi huyu mtu atachukuliwa hatua.

Sasa kamati hiyo Teuli ni ya nini Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu Kamati Teule hiyo kwa mujibu wa utaratibu itakuwa haina maana na bado haija-*qualify* kufanywa au kuundwa Kamati Teule. Hivyo, yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe ayaheshimu maneno yake aliyosema kwamba, serikali iji-*commit* iseme kuwa kama kuna tatizo basi huyu mtu atachukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, na sisi tumesema hapa kwamba upo utaratibu ambao umefuatwa, basi tutaituzama ikiwa umevunjwa serikali itamchukulia hatua *officer* huyu. Sasa *commitment* gani nyengine anayoitaka kama si hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba niseme nilipokuwa nachangia nilizungumza nadhani Mwenyekiti wewe mwenyewe ni makini usingeniruhusu kujibiwa hoja ambayo sikuichangia katika mjadala. Kwa kweli sidhani kwamba umefika hapa hukumbuki tulichokizunguma na bahati nzuri nilipokuwa nikichangia ulikuwepo. Mhe. Mwenyekiti, naamini uliniruhusu kwa sababu ulikuwa unajua kwamba nilihoja suala zima la ununuzi wa Mitambo ya *Digital*.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nimesoma hapa kwamba kuna hoja lazima uzitolee taarifa na turejee katika mjadala, lakini Kanuni ya 49 imesema kwamba kuna hoja ambazo unaweza kuziibua bila ya kuzitolea taarifa na zimeorodheshwa pale kifungu cha 49 (4) (a) mpaka (j). Sasa kifungu cha (j) kinaeleza kuhusu hoja ya kuunda Kamati Teule.

Hivyo, nimeibua vipi? Nimeibua kwa sababu maelezo niliyoomba kutoka serikalini hayaniridhishi, tena naamini nisijisemee peke yangu wanasemea na Waheshimiwa Wajumbe wengi wa Baraza lako hili tukufu, ambao haturidhiki na utaratibu kama huyu wa majibu ya jumla ya serikali katika vitu kama hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Katiba yetu serikali haiwezi kujisimamia wenyewe, Baraza hili lina mamlaka kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kuisimamia serikali. Sasa hapa tunachokifanya ni sehemu ya majukumu hayo tuliyopewa na Katiba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimeulizwa kwamba utaratibu gani uliokiukwa na wala siwezi kusema kifungu kimoja kimoja, kwa sababu maelezo yaliyoibuka katika mjadala huu yanaonesha mambo mengi sana. Kwa mfano, nilisema serikali itatuambia kwamba *tendering* ilifuatwa, kuna na fedha. Kwa hivyo, nasema mimi mwenyewe binafsi na ninaamini na wenzangu hatuamini maelezo ya serikali. *(Makofi)*

Sheria iliyokuwepo ya *The Public Procurement and Regulations* ndio inayoongoza na *specifical* kuna vifungu vya 20 na 21 vinaelezea vya sheria hii kuhusu taratibu za kufuatwa na wala haisemi mtu kwa jina lake binafsi au serikali ingeniambia kwamba sheria hii inaruhusu mtu kwa jina lake binafsi kuagizia mali kwa niaba ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana ninasema kwamba maelezo mengi yanatolewa, lakini hayajikiti katika nukta yenyewe. Sasa sheria kifungu gani kilikiukwa katika *Public Procurement* ama vipi haya yatafanya na hiyo kazi ya kamati ambayo ninayoiomba iundwe, itatuletea taarifa yake na halafu Baraza litaamua.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini serikali inagopa, yaani kwa nini serikali iwe kila wakati inaingilia kati kuzuia Baraza kufanya wajibu wake na kutekeleza kazi zake ambazo zimepewa na Katiba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna mgawanyo wa madaraka otherwise itakuwa hatuna maana. Kwa kweli serikali inayo majukumu yake na Baraza pia linayo majukumu yake. Sasa ikiwa kila wakati serikali tuiachie ikajisimamie wenyewe na ijichunguze wenyewe pamoja na kujihukumu wenyewe, basi Baraza hili Mhe. Mwenyekiti tuliondoshe. Kwa hivyo, mambo yanakuja hapa kwa sababu hiki ni chombo cha wananchi kinachopaswa kusimami haki zao. *(Makofi)*

Hivyo, Mhe. Mwenyekiti kifungu gani na utaratibu gani naomba nimsaidie Mhe. Mjumbe aliyeuliza swali hili nasema hayo tutakwenda kuyatizama na nimetaja vifungu vya 20 na 21, lakini pengine yataibuka mengi zaidi. Kwa maana hiyo, nasema kwa mujibu wa Kanuni ya 49 (4) (j) tuunde Kamati Teule yende ikachunguze kadhia nzima sasa, kwa sababu mwanzo tulitaka kujua jina, lakini haya maelezo yaliyoibuka hapa yananipa wasi wasi juu ya kadhia nzima ilivyoendeshwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Baraza lipewe nafasi yake, serikali iheshimu mamlaka yake na pia iheshimu mamlaka ya Baraza lako Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa hiyo sheria iliyovunjwa ni Sheria ya Manunuzi.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, naelewa nia nzuri ya Mhe. Mjumbe kwamba sio kumkomoa mtu yeyote lakini ni kulinda utaratibu wa kuendeshaji wa serikali ambao ni kazi yake, pia Baraza nalo lina taratibu zake.

Kwanza hoja aliyoizungumza kifungu cha 49 cha Kanuni za Baraza Mhe. Ismail Jussa Ladhu ni kifungu cha jumla cha kutoa hoja Baraza linapokuwa katika Baraza sidhani kama ni katika Kamati ya Matumizi. Lakini utaratibu wa Kamatii ya Matumizi Mhe. Mjumbe pia najua anaelewa kwamba utaratibu ulioelezwa Sehemu ya Tisa vile vifungu vilivyofuata *specifical* vinapaswa kufuatwa na Baraza linapokuwa katika Kamati ya Matumizi.

Kwa hivyo, kifungu cha 49 ambacho ni cha jumla hakiwezi kutumika katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuleta hoja. Kwa maana hiyo, hoja yake hiyo nadhani ameileta katika wakati ambao hauhusiki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba hoja yake ya msingi aliyoitaka tayari imeshajibika ni kuhusu *commitment* ya serikali imeshatolewa. Sasa hii ku-*shift*

goal, mimi nadhani ni sawa na kucheleweshe au kutumia haki ya Mjumbe kusema kwa ajili ya kucheleweshe shughuli za Baraza, kwa sababu yalishatolewa majibu aliyotaka sahihi. *(Makofi)*

Hivyo, kusema sikubaliani nayo. Mhe. Mwenyekiti, hilo liko wazi kwamba sasa hapo ni ku-*abuse* ile *right* ya kusema, yaani kuitumia vibaya ile haki jambo ambalo Kanuni pia haliruhusu.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kwamba hoja yake ya Kamati Teule inakiuka utaratibu wa Kanuni. Lakini pili hata hiyo hoja yake ya kutaka kusema kwamba iundwe haikuja kwa msingi ambao unakubalika kwa Kanuni hizi, kwa sababu alishajibiwa sahihi kile ambacho alitaka. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nakubali au niseme nakubali maneno ya Mwanasheria Mkuu aliposema kwamba nia yangu ni kuhakikisha kuwa fedha za walipakodi zinalindwa ipaswavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimetumia Kanuni hiyo ya 49, nadhani unaweza kutusaidia kama ni makosa kuibua katika utaratibu wa Kamati ya Matumizi, basi naomba utusaidie. Lakini nafikiri ninayo haki na nimeshasema Mhe. Mwenyekiti, katika muongozo wako uliotupa pale, kwamba tunaweza tukarejea katika Baraza.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti maelezo niliyoyaomba yalikuwa yanahusika na Kamati ya Matumzi, ambapo suala lenyewe nililolitolea hoja nimeliibua katika mjadala wa suala lile. Sasa nasema maneno yaliyotolewa hayakuniridhisha nadhani tunayo haki hiyo.

Sasa kama kifungu hiki ili kitumike ni kufanya Kamati ya Matumizi irudi kwenye Baraza, basi nadhani hatuwezi ku-*defeat purpose* ya msingi kwa kuhakikisha uwajibikaji kwa kutumia *procedure* kama Kamati ya Matumizi haiwezi, basi Mhe. Mwenyekiti uturuhusu kurejea katika Baraza kwa ajili ya kuamua.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, sikubaliani na maelezo ya Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba natumia haki yangu, ili kucheleweshe mjadala pasi na sababu, hilo Mhe. Mwenyekiti silikubali kabisa, kwa sababu tumeletwa hapa na wananchi, ili kuja kuwatetea na ni haki yetu kuwasimamia haki zao Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, naomba sana kama kifungu hiki hakiruhusu, basi Mhe. Mwenyekiti niliombe Baraza lako turudi katika Baraza kwa ajili ya kuliamua suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kuna masuala mawili hapa ambayo ningeomba niyaelezee kabla hatujafikia maamuzi tufanye nini kama kuunda Kamati Teule au vipi.

Kwanza nadhani tufikie pahala tuelewe je kuna matumizi mabaya ya fedha yaliyofanyika, kwa sababu inapotokea kuna matumizi mabaya ya fedha iliyotumika, basi ipo haki ya kupunguza fungu kwa utaratibu wa kutoa shilingi. Sasa ikiwa hakuna matumizi mabaya yaiyofanyika, lakini labda sera kwa ujumla utaratibu, yaani mpango ule haukufuatwa sasa ule ni utaratibu wa kutoa shilingi mia moja.

Hivyo, hayo ndio mambo yanayohusu hasa katika Kamati ya Matumizi ama hukubaliani na matumizi yalivyotendeka au hukubaliani na sera hiyo iliyopitisha jambo hilo. Kwa hivyo, hapa kitu kilichokuja ni tofauti kidogo na wala sijapata taarifa hadi sasa kama kuna matumizi mabaya yaliyofanyika nadhani haijatoka hiyo hapa.

Sasa suala lililokuja hapa ni kwamba utaratibu wa sheria ya Manunuzi ulionesha hapo haukufuatwa na haukufuatwa kwa sababu kuna mtu binafsi ambaye sijui kama aliingia kwenye *tender* au vipi sina hakika.

Lakini katika suala la mawasiliano kati ya chombo na chombo kwa kawaida wakati mwengine inawezekana ikaandikwa barua na taasisi fulani lakini ikaambiwa *attention* kwa mtu fulani, kwa sababu ya mtu yule ndio aliyekuwa anafanya mawasiliano ya mara kwa mara, sasa sina hakika kama ndugu Rama baadae amegeuka akawa vile vile yeye kaingia kwenye hiyo tenda sina hakika hiyo, kwamba kwa upande mmoja amefanya kazi kwa niaba ya Katibu Mkuu ambae ndio Waziri anachosema hapa lakini kwa upande mwengine akaingia kama mfanya biashara sasa hilo sina hakika na kama kungekuwa na hayo basi hata mimi ninayeendesha kikao hiki ningepatwa na mashaka kidogo kwamba umefanyika *doble standard* ya kazi moja ya ufanyaji biashara lakini chini ya Afisi ya Wizara yako. Hebu tupatieni malelezo ili tupate kifikia pahala tuweze kuamua hili jambo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. mwenyekiti naomba nielezee kwa ufupi tu ule utaratibu unaotumika, suala liliopo la msingi lililoulizwa ni ununuzi wa mtambo wa TV ilitangazwa kwenye magazeti kwamba kuna hicho kitu watu waka-*apply* wakaleta tenda zao hizo tenda zikapelekwa *BoT* wala sisi hatukuzigusa, *BoT* wana masharti yao wao ndio walioangalia zikapelekwa kule moja, mbili , tatu , nne kwa sifa tunazotaka huyu ndio anayefaa akabarikiwa yeye. SMZ wala hatukutia mkono wetu wakambarikia huyo wakamchukua zikafunguliwa BOT na *PBZ* ukanunuliwa huo mtambo.

Kwa hivyo hata hiyo pesa hapa haikuguswa nasisitiza tena, kama umekiukwa utaratibu wa sheria namba 5 haikukiukwa utaratibu wote umekwenda sahihi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Ismail Jussa mimi ni mmoja kati ya waumini wakubwa sana kuona kwamba taratibu za baraza zinafutwa kwa upande mmoja, sheria za nchi zinafuatwa ni muumini sana wa jambo hilo na ukija kwenye matumizi huko tena ndio usiniambie sipendi kabisa kuwepo matumizi mabaya ya aina yoyote. Najua wengine huingia pamoja na maadili ya kidini kwa sababu tunajua baadae yatatuathiri. Mhe. Ismail Jussa hebu tusaidie maana hili jambo linakuwa ni gumu kwa sababu moja tu, matumizi mabaya kimsingi hayakufanyika kwa sababu taratibu za tenda zimefuatwa taarifa tuliyoipata hapa, *unless use wise* tuambiwe kwamba hiyo tenda haikufikia utaratibu wake.

Ndugu Rama alikuwa anafanya kazi kwa niaba ya katibu Mkuu ndicho tulichoelezwa pale, sheria unazungumzia kwamba haikufuatwa sawasawa ya manunuzi, kwanza niombe radhi lile suala ambalo umelitaja kwamba Mwanasheria Mkuu kasema labda ulikuwa unachekelewesha kikao hiki, mimi nasema hapana ulikuwa unatafuta uwazi wa mambo na hiyo ni haki, kutafuta uwazi ili taratibu ziwe zimetimia katika shughuli zetu hizi.

Serikali kwa ujumla hapa inatoa ahadi mbele ya baraza hapa mbele ya kamati hii kuwa itamfuatilia na itafatilia na labda mimi niongeze kwamba hiyo taarifa itakayofuatiliwa na wala hakuna ubaya kumshirikisha Mhe. Ismail Jussa Ladhu iletwe Barazani hapa ili wajumbe wapewe hiyo taarifa kwamba suala la taratibu zile kama kuna makoseo ahadi imetolewa hapa kwamba hatua zitachukuliwa kwa huyo aliyefanya hayo makosa. Mhe. Ismail Jussa hebu tusaidie kama kuna *commitment* ya serikali.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naomba niruhusu kuzungumza maneno machache kabla sijasema, moja nadhani wewe na wajumbe wengine wote humu ndani ni mashahidi jinsi sisi wajumbe tunaoitwa *back bencher* jinsi tunavyotoa mashirikiano kwa serikali, ndio maana yamekuja mambo mengi hapa tumeyaibua lakini mwisho hatujakwamisha bajeti hata moja, kwa hivyo nataka hilo lieleweke kwanza kama ulivyosema nia yetu ni kuisaidia nchi sisi ndio walinzi wa haki za wananchi na pesa zao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka niseme katika watu ambao nawaheshimu sana na mimi sio peke yangu wote wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanakuheshimu sana Mhe. Mwenyekiti, lakini sikuridhika na majibu ya serikali lakini naheshimu uongozi wako Mhe. Mwenyekiti, kwa muongozo uliotoa kwamba umetoa pendekezo la kuniomba nikubali kwamba atuipe nafasi serikali ikalichunguze lakini halafu ripoti yake iilete katika baraza hili.

Nalikubali pendekezo hili lakini sikubaliani na ule ushauri wako kidogo kwamba na nadhani katika hilo utanikubalia, kwamba ni shirikishwe na mimi kwa sababu gani.

Kwa sababu ukinishirikisha mimi mmoja itakuwa hii kamati haiujulikani kama ya serikali au ya baraza, kwa hivyo kama serikali imechukua jukumu bado ikafanya wajibu wake kwamba ni sehemu ya kufanya kazi *executive* na kazi ya *registration* itakuja kufanyika hapo ripoti yao ikishakamilika na kuletwa katika baraza hili. Kwa hivyo sijui wanahitaji muda gani kama ndani ya kikao hiki hiki kwa sababu siku zinakwenda haraka hata ukisema kikao cha Oktoba kitakuja tu.

Nakubali tuendelee kwa hoja hiyo kwamba wakachunguzwe chini ya muongozo wako Mhe. Mwenyekiti utakuja kutwambia ni lini iletwe taarifa hiyo na naomba tukubaliane kabisa ripoti hiyo ikiletwa tuijadili wajumbe, halafu hapo hapo tutaona kwamba tutaridhika na maelezo hayo au tutahitaji kufanya uchunguzi zaidi kwa kutumia mamlaka tuliyopewa na kanuni na katiba kwenda kuchunguza.

Kwa hivyo kwa misingi hiyo na heshima yako nakubali tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe Mhe. Ismail Jussa Ladhu kanikumbusha jambo moja tena limetokea ndani ya baraza mimi wakati huo ni mjumbe tu wa kawaida, alikuwepo mjumbe mmoja wa jimbo la Magomeni sio Mheshimiwa Salmin alikuwa Mhe. Mussa Ussi Ameir kuhusu habari ya mchele huu wa Mbeya akashirikishwa kwenda kuchunguza kwa bahati mbaya hakuna majibu yaliyokuja. Sasa watu walikuwa wanatuelemea yeye kwamba jee na yeye alikuwa yumo. Sasa Mhe. Ismail Jussa Ladhu yeye hataki aje kuambiwa hivyo anataka kubaki kwa kuendelea kujadili masuala yakapata uwazi wa mambo, Mhe. Ismail Jussa wewe hutoshirikishwa na ripoti iletwe sasa sijui Mhe. Waziri unatuahidi muda gani hebu twambie.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, tunaahidi kwamba kikao cha Oktoba tutaleta ripoti yetu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi, nilipokuwa nachangia hotuba ya Mhe. Waziri hapa nilizungumzia suala la ukodishwaji ule wa kisiwa cha Changuu, sasa Mhe. Waziri ametoa maelezo hapa juu ya ukodishwaji ule lakini tulikuwa tunahoja zaidi kuacha dola efu nane ambazo zilikuwa zikipatikana wakati kisiwa kikiendeshwa na Shirika la Utalii na kukikodisha kwa dola 3,500 kwa muwekezaji. Sasa hapa utaona kuna tofauti kubwa ya pesa hapa, lakini maelezo yake Mhe. Waziri anasema kwa sababu huyu ambae amekodishwa analipa kodi

ya ardhi, ongezeko la thamani nafikiri kakusudia *VAT* analipa *ZSSF* yaani michango ya wafanyakazi, hivyo hawa Shirika la Utalii walikuwa hawalipi hivi kwanza nataka kujua hilo.

Lakini pesa walizokuwa wakikusanya ni dola zaidi ya elfu nane huyu anailipa serikali zaidi ya dola 3,500 mimi nilikuwa nataka ufafanuzi kuhusu hili Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Sina taarifa rasmi kama walikuwa wanalipa au walikuwa hawalipi, lakini kama tulivyoeleza kabla kwamba hivi sasa hatuna mamlaka na tumesema kwamba hata hivyo bado hatujaangalia mikataba yote kuitizama kama ina maslahi na tukiona haina maslahi basi nadhani wakati wowote tunaweza kukata tu. Kwa hivyo Mhe. Mjumbe namuomba kwamba atupe muda tufanye *revue* hiyo tukiona haina maslahi tunakata na kama ina maslahi tutatizama walikuwa wanalipa au hawalipi tutaangalia hilo suala, ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sijui kama nimemfahamu vizuri Mhe. Waziri maana yake nilikuwa simsikii vizuri kwamba wanaipitia tena ile mikataba, sina uhakika kasema nini kwa sababu sauti yake simsikii, sasa naomba yale maelezo ayatoe vizuri ili niweze kutengeneza hoja yangu vizuri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nimesema haya masuala kuna masuala mengine ambayo tunaingalia ile mikataba, tukiona ina maslahi na taifa basi tutaendelea nayo lakini tukiona haina maslahi tutaipitia upya na kuweza kuihaulisha tuna haki hiyo.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nimemsikia vizuri Mhe. Waziri kwamba wataiangalia tena upya, lakini mimi ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa hawa shirika la utalii wakikusanya pesa zaidi ya hizi ambazo zinatolewa hivi sasa na muwekezaji ndio hoja yangu, sasa kipi kilichopelekea tuwache pesa nyingi ambazo zinakusanywa na wazalendo wetu wenyewe aje muwekezaji atupe pesa kidogo zaidi. Hoja yangu ipo hapo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti serikali nia yake kubwa ni kuendeleza uwekezaji nchini na moja katika eneo la kisiwa kile cha Changuu hali ya majengo yenyewe ya pale ilikuwa haipo katika hali nzuri, jkwa hivyo uamuzi wa serikali uliamua kukaribisha wawekezaji ili pale mahala paimarishwe na pavutie kwa nia ya kuendeleza wawekezaji wa utalii, malipo haya yanayolipwa ni sehemu tu ya malipo ambayo serikali ilitegemea ingekusanya zaidi kwa njia mbali mbali za kodi, wakati huo huo ni

kuzikusanya dola eflu nane kwa mwezi na wakati mwengine zilikua hazifikii lakini bado sio kwamba kulikuwa na faida, ila kulikuwa na hasara za uendeshaji wa shughuli za kisiwa kile pale kwa wafanyakazi na mambo mengine.

Kwa hivyo sio dola efu nane safi sasa Shirika wanapata dola elfu tatu na mia tano safi na kodi nyengine ambazo zinatokana na uendeshaji ule, lakini hata hivyo mkataba wenyewe unatoa nafasi kwa kila baada ya kipindi kupitiwa na kuangaliwa, kama sasa unahitaji kufanyiwa hivyo basi serikali itafanya hivyo ili kuhakikisha kwamba taifa linapata haki zake na maslahi yake.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sikubaliani na mawazo ya Mhe. Waziri, kwa sababu ikiwa muwekezaji anatulipa dola 3,500 kwa sasa hivi anazosema yeye ni safi analipa kodi ya ardhi, ongezeko la thamani hili shirika la utalii tumuite muwekezaji wa ndani ambayo tunahimiza kila siku kuwa na wawekezaji wa ndani hili ni shirika la serikali likikusanya dola elfu nane, likiweza kufanya mahitajio yake. Ingawa Mhe. Waziri anasema kuna uendelezaji pale katika kisiwa kile kwa sababu hakuna hicho kitu wale makobe wetu wenyewe kawakuta pale pale, yale majumba kayakuta pale pale zaidi sifikirii kama anafagia anachofanya kwa sababu panakuwa panaanguka majani mengi na kupiga piga rangi labda lile jengo si kitu chengine cha ziada ambacho amekiongeza muwekezaji huyu pale.

Mimi nafikiria hakuna haja ya kuendelea na juwekezaji wa aina hii ni vyema serikali ikafuta mkataba huu ili kisiwa kile kikarejeshwa kwa Shirika la Utalii kikaweza kujiendeleza kwa maslahi na manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti uwekezaji pale umefanyika tena umefanyika vizuri na mimi nakubaliana na Mhe. Mwakilishi twende tukaone na picha za zamani zipo hali ilipokuwa kwa kisiwa kile cha Changuu na hali ilivyo sasa, isipokuwa nakubaliana nae kuwa kwa kuwa mkataba unaruhusu kupitiwa tuone kama muda wake umefikia tutizame kwa maslahi ya taifa letu, lakini uwekezaji Mheshimiwa upo tana mzuri na pahala pako wazi mtu yoyote aende ataona mabadiliko hayo. Tujue tu shirika la utalii hali yake ilivyo sasa hivi uwezo wake wa kuendeleza kwa sababu wanavyo vianzio vyengine lakini bado wanashindwa kutokana na mtaji.

Kwa hivyo haya mambo yanayofanywa na serikali imepima na uwezo halisi kwa shirika lenyewe hivi sasa bado tunafanya tathmini ya mashirika tuone kwamba bado shirika la utalii lina uwezo wa kuwa kama shirika au kuchukua hatua nyengine.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri maelezo aliyotoa Mhe. Waziri na maelezo aliyotoa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais yana maana na mimi sipendelei kutoa amri ya kusitisha mikataba hapa, kwa sababu mikataba ina dhima zake unaweza kukatisha mkataba lakini baadae ukaitia hasara serikali. Sasa kauli aliyoitoa Mhe. Waziri kwamba tufuatilie mikataba hiyo na kama itakuwa na maslahi iendelee na kama haitokuwa na maslahi tukatishe bila ya kuitia hasara serikali nafikiri ni jambo la maana, vyenginevyo kuna baadhi ya mikataba ukiukatisha basi unapaswa uulipe nadhani kwa wenzetu kuna mkataba mmoja huko mpaka leo unaleta tabu kubwa sana wa mambo ya nishati Mhe. Ismail Jussa Ladhu anajua serikali inadaiwa mabilioni mengi mno ambayo hadi sasa haijajulikana yafanyike lini sasa hiyo ndio dhima ya mikataba wakati mwengine.

Kwa hivyo sio vizuri kukatisha mkataba ndani ya chombo hiki halafu serikali ikaja ikawa ina deni kubwa la kulipa, nadhani tukubaliane kwamba Waziri afuatilie mikataba hiyo kama itakuwa na maslahi basi iendelee na kama haina ifutwe na ripoti hiyo tupewe katika baraza.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti mimi nakubaliana na rai ambayo umeitoa hapo lakini labda nitoe pendekezo kwamba ni vyema tukaunda kamati ya baraza katika kuchunguza mikataba hiyo, ekenda kuchunguza kwa sababu sio huo tu kuna mingi sasa ipitie ile mikataba halafu itoe mapendelezo yake kwamba huu unafaa na huu una maslahi kwa wananchi, huu haufai. Kwa sababu naona ukiiwachia Wizara au Waziri mhurika ndio akenda kufanya hilo na yeye ndie aliyefanye hilo sifikirii kama patatendwa haki.

Naomba Mhe. Mwenyekiti tukaunda kamati miongoni mwa wajumbe wako hapa kwa ajili ya kupitia mikataba mbali mbali ambayo inahusu mambo ya uwekezaji kama haya, ili tukaweza kujisafisha kwa sababu haya ni malalamiko ya wananchi wanapokuwa wanajua kitu kama hichi halafu serikali inakwenda inasema tumeshachunguza tunaona hakuna maslahi ya kumuondosha yule muwekezaji, lakini ukitizama kile kipato ambacho anatulipa na kipato ambacho kilikuwa kinapatikana ni kidogo itakuwa kama hatukuwatendea haki wananchi.

Nakuomba sana Mhe. Mwenyekiti tuunde kamati na hiyo kamati wawemo wajumbe wa baraza lako kwenda kuangalia hiyo mikataba, ombi langu lilikuwa ni hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. waziri tukubaliane katika utafiti huo nitakupatia baadhi ya wajumbe ushirikiane nao katika kuangalia mikataba.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa tunazo kamati zetu za kudumu za Baraza la Wawakilishi zinafanya kazi hizo, pale wanapoona wanahitaji kutaka jambo lolote kwa maslahi ya watu wetu serikali yetu ipo hapa kuwatumikia wananchi na kamati hizi zipo pale kutusaidia namna ya utendaji bora, sisi tunakubali kwamba kamati ni dira ya utekelezaji mzuri wa shughuli zetu za serikali. Kwa hivyo kamati zetu za kudumu zinazo haki za baraza kuulizia jambo kufuatilia pamoja na yote hayo na mikataba hiyo wataona watafahamishwa kuliko kila siku kuunda kamati, hizi kamati tutaunda ngapi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti mimi ningeliomba kwamba kwa mujibu wa taratibu na kanuni kuna kamati jamani zinazohusika, kwa nini katika vikao vyetu tukubali tuunde makamati sasa hivi hizi kamati zinazofuata taratibu maana yake nini Mhe. Mwenyekiti.

Naomba lolote linalohusu katika kamati husika lirejeshewe kwa sababu tunafanya kazi kwa mujibu wa taratibu na kanuni za baraza, naomba sana suala hili lirudi pamoja na Mhe. Ismail Jussa Ladhu lirudi kwenye kamati yangu, mimi bado mwenyekiti nipo *very strong* sitokubali kuyumbishwa kamati yangu wakati imefanya kazi zake, naomba sana tufuate taratibu na tuheshimu kamati ambazo umeziunda kwa mujibu wa taratibu *(Makofi)*

TAARIFA

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani twende kwa mujibu wa kanuni, kanuni yetu kuna kamati za baraza lakini kanuni inaruhusu kuundwa kamati teule, hili neno kuundwa kamati teule lina maana maalum kwa hivyo mimi nadhani kama ikiwa kamati teule haina umuhimu katika baraza hili basi kifungu hiki tuondoshe. Lakini kama ina umuhimu kwa maana ya masuala maalum naomba liwepo, hii maana yake nini katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha tano kimeweka mgawanyo wa madaraka.

Kwamba inapofika pahali serikali ikawa ina tatizo lazima baraza lichukue mamlaka yake ya kusimamia serikali, kwa msingi huo basi mimi nakubali kwamba masuala yanayohusu sekta yapelekwe kwenye sekta lakini kwa masuala mahsus yanayoletwa mbele ya Baraza lako basi tuitumilie tume teule, kwa msingi huo huo kama ikiwa ni suala la Mhe. Ismail Jussa Ladhu kamati inayohusiana na mambo ya uchunguzi wa hesabu na mali za Serikali ni kamati ya *PAC.*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe sasa nakushukuruni kwamba mnakusudia kufanya kazi kweli kweli maana kila kamati inasema mimi nitaifanya hiyo kazi, sasa ili kuondoa hayo hilo jambo Spika ateue wajumbe

washirikiane na Mhe. Waziri kuipitia hiyo mikataba, nitaranda mote humo ili nitizame huku nimchukue nani, hapa nimshukue yupi ili kwenda hapa kumsaidia Mhe. waziri tufikie hapala pazuri.

Nasema hivyo kwa sababu tatizo ni kwamba hali yetu ni ngumu kwa hivyo kuchukua kamati kubwa nayo wakati mwengine ni matumizi mengine ya fedha, kwa hivyo tuchukue wajumbe wachache ambao wanaelewa na naelewa nyote mnaelewa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mimi nadhani kinachozungumzwa Mhe. Mwenyekiti ni suala la mikataba ya serikali, nadhani kwenye hotuba ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria alieleza nia ya serikali kuunda kitengo maalum cha usimamizi wa mikataba chini ya ofisi ya Mwanasheria Mkuu, moja katika kazi yake ni kufanya mapitio na katika *stard* ndogo tuliyoifanya ya mikataba ya serikali wasi wasi wangu labda tuainishe kwamba ni mkataba huo wa Changuu na mkataba gani na gani.

Lakini tukisema mikataba ya serikali wasi wasi wangu ni kwamba hiyo kamati inaweza kuchukua miaka miwili kwa sababu ni mingi na mambo ambayo mengine yanahitaji utaalam mahususi wa sheria, kwa hivyo mimi nilitaka nitoe indhari hiyo tu kabla ya uamuzi wowote ambao utachukuliwa.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muda wetu unakaribia kumalizika kwa hiyo nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais atoe hoja ili tukamilishe shughuli hii.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa shughuli iliyo mbele yetu na kwa vile muda uliobaki hautoshi kumalizia shughuli iliyo mbele yetu naomba Baraza lako litengue kanuni kwa muda ili tuweze kumaliza shughuli iliyo mbele yetu. Naomba kutoa hoja Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe niwahoji basi wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri mkataba ambao utakuwa unafuatiliwa ni huu ambao una hoja hapa mbele ya Baraza, kwa hiyo mkataba huo ndio ufuatiliwe na kutolewa taarifa baadaye kama vile ambavyo tulikuwa tumefikia pahala kwamba ikionekana hauna faida basi unakwenda, baada ya kutizama masharti yote na dhima zote. Nitakalojitahidi kulifanya ni kwamba ndani ya mkataba huu juu ya wajumbe hao nitakaowapeleka kuwe na wajumbe wale ambao wana sheria ndani yake na watu wanaoelewa mambo ya mahesabu na wengineyo kama hayo. Waheshimiwa Wajumbe nitajitahidi kamati isiwe kubwa na nitaizingatia yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe mmeyasema.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa maelezo yako yamejitosheleza mimi nahisi tuendelee kamati itafanya kazi yake.

Kifungu 0201	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	76,000,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba	493,900,000
Kifungu 0401		

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla ya kutoa maelezo yangu juu ya fungu hili naomba kwa heshima kubwa serikali pengine wangejiandaa baadaye huko siku za mbele wakafundisha dhana nzima ya mgawanyo wa majukumu katika mihimili mitatu ya dola, nadhani wangetufundisha hilo huko mbele na wao wakajikumbusha kwamba nani mtendaji, nani mtoaji haki na nani msimamizi wa majukumu hayo.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nilihoji kwenye fungu hili kwamba mafanikio haya ya Baraza ambayo tunayapata ni msaada mkubwa wa waandishi wa habari na vyombo vya habari, na kwamba waandishi wahabari wanastahili kupewa posho la nguo, posho la kazi na posho ambalo walikopwa mwaka 2005 kwa safari ya Holland.

Mhe. Mwenyekiti, nilipoangalia mahesabu kasma 211,110 posho maalum kuna milioni 60, posho ya safari ya ndani ni milioni 30, posho za safari ya nje ni milioni 43 jumla ni shilingi milioni 138, mwaka jana ilikuwa ni milioni 138 mara hii ni milioni 133. Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kujua kwa nini wafanyakazi hawalipwi ambapo madeni yao yote haya si zaidi ya milioni 20 tangu 2005 hadi hii leo, Mhe. Waziri amejibu na ameonesha kwamba jukumu hili labda ni la Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi sikuridhika na majibu hayo naomba anisaidie na nikasema kabisa kwamba kwa sababu Idara ya Utumishi inaelekea haiwajali wafanyakazi wake, basi fedha hizi milioni 73 ambazo zinatengwa tuzipunguze kwanza

tulipie deni tangu miaka sita nyuma halafu zitakazobakia ndio watafanya safari za nje. Mhe. Spika, Mhe. Waziri alisema kwamba safari ni muhimu lakini kwa mimi nadhani safari sio muhimu kuliko haki ya mtu. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu yangu kuwa sio kwamba hatuwajali wafanyakazi, tunawajali sana na tunasema tunawalima na madeni yote ya nyuma tutawalipa. Mhe. Mwenyekiti, namuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba hilo suala usiwe na wasi wasi nalisimamia mimi mwenyewe kwamba madeni yote ambayo waliyokuwa wanahitaji walipwe basi watalipwa. Mhe. Mwakilishi naomba usiwe na wasi wasi niamini juu ya hilo naomba unipe muda, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini kwamba Mhe. Waziri anafanya jitihada kubwa kwa sababu nimefuatilia nimegundua kwamba yeye binafsi kama Abdilah Jihad Hassan huwasaidia shilingi 30,000 hapa ndani ya Baraza, lakini ni Mhe. Jihadi na Katibu Mkuu sio ofisi. Kwa hivyo, akiniambia nimuamini miaka sita ya nyuma ndio imani yangu inakuwa ndogo kwa hiyo nataka aniambie mwezi huu wa saba baada ya bajeti hii lini atawalipa pesa zao na mimi aniletee kopi kwamba wamelipwa vyenginevyo mheshimiwa sitomuamini kwa hili. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu miaka saba mingi kwa shilingi 5000 za mtu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba ikimaliza hii bajeti kwa sababu tumekubaliana kwamba kila baada ya wiki mbili iwe tunawalipa, na tutafanya hivyo, pia ikimaliza bajeti tunakusanya madeni yao yote tutawalipa. Kama walivyoeleza kwamba mwenyewe nilikuwa natoa pesa zangu mfukoni ili kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa bidii. Lakini baada ya kumaliza bajeti sisi tutawalipa kila kitu wala usiwe na wasi wasi kwa hilo naomba uniamini.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kumuamini Mhe. Waziri lakini wasi wasi wangu kwamba kwa sababu yeye ukimgusa mwandishi wa habari vile anavyompenda yuko tayari auze chake awalipe. Mimi nazungumza mpango wa utumishi anambie baada ya bajeti hii pengine kuanzia jioni au kesho anambia saa ngapi atawalipa na mimi aniletee *copy* nishuhudie kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, maneno ndio matusi nawaomba sana waandishi wa habari wanisamehe kwa hili.

Mhe. Mwenyekiti, ninazo taarifa kwamba nguo wenzetu ambazo wanavaa haya makoti ni nguo kutoka katika Ofisi yako ya Baraza la Wawakilishi

wanaazimwa, huu sio ustaarabu mzuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri anambie kesho saa ngapi atawalipa hawa watu kwani sisi ndio wasimamizi wa haki za watu, wao wameshindwa miaka sita nije niwaamini leo. Kwa hivyo, aniambie Mhe. Waziri kwamba lini hawa watu atawalipa vyenginevyo Mhe. Mwenyekiti, kanuni ya 96 ibara ya (6) (1) basi inaniruhusu mimi kupunguza shilingi hivyo nipunguze kwa sababu inawezekana hawataki kutumia maslahi ya watu. Kwa hivyo, aniambie lini atawalipa hao watu sio aniambie baada ya bajeti, aniambie tarehe ngapi nije nipate ushahidi kwamba amewalipa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumueleza Mhe. Mjumbe kwamba siwezi kumwambia lini hasa, lakini kwanza nipe hizi fedha utakaponimalizia basi hiyo siku nitakayowalipa mimi nitakwita na nitakushirikisha na wewe.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya wiki zijazo kuna mwezi mtukufu wa Ramadhani na baada ya Ramadhani kuna skukuu, wenzetu hao wamevumilia muda mrefu sana, namuomba Mhe. Waziri aniambie kabla ya sikukuu hizi pesa atawapa au vyenginevyo sitokubali, tuendelee.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, adhma yangu hasa ilikuwa ni kuwalipa kabla ya sikukuu na nitafanya hivyo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu adhma yake ndio nia na kila jambo linataka nia naamini Mhe. Waziri atafanya hivyo, asipofanya hivyo itakuwa ametudanganya naomba kabla ya sikukuu awalipe, naomba tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako linatufanya kila wakati tukumbuke mpaka mawaidha *ina mal aamal bin niyaat*. Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu kuna masuala mawili nataka kuyahusisha hapa niliyazungumza, hili moja kwa sababu ni dogo tu naomba niliunganishe hapa hapa. Mhe. Mwenyekiti, katika waliochangia kuhusu hili suala la posho za watendaji mmoja nilikuwa ni mimi, hili nataka maelezo madogo tu kwa sababu Mhe. Hija ameshaligusia nalo ni kwamba nilipoitazama bajeti hii Mhe. Mwenyekiti, kulikuwa na hili suala la kifungu hiki kinachohusu posho maalum tunaona kimenona sana katika idara nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, hili alizungumzia kwenye Idara ya Utumishi lakini alizungumzia kwa wizara nzima kwa sababu idara hii ndio inayosimamia kwa mujibu wa utaratibu wizara nzima, unalikuta katika kila idara iliyokuwepo fungu la posho maalum hasa katika Idara ya TVZ ukurasa wa 579 hicho kitabu kikubwa, kwenye Idara ya Habari Maelezo ukurasa wa 581 na kwenye Kamisheni ya Utamaduni na Michezo limenona sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi

nilikuwa nataka nithibitishiwe kwamba ukilinganisha ilivyokuwa mwaka jana na mwaka huu kwamba ndio linakusudiwa kulipa hayo malimbikizo. Lakini nasema hilo Mhe. Hija ameshaligusa labda anitosheleze kwa majibu ya ziada tu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hoja yangu ninayotaka kuzungumza katika mchango wangu nilizungumzia suala la kadhia ya mkataba wa ukodishwaji ukumbi wa *Komba Disco Take* na Mhe. Mtando alipouliza hapa Mhe. Mwenyekiti, ulisema tubane pale kwenye mshahara wa waziri kwa sababu tumetafuta fungu la Shirika la Utalii Hoteli ya Bwawani hatuyaoni humu katika vitabu. Kwa hivyo, ndio penye fungu la Mhe. Waziri naomba nipate maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba kuna kampuni zilitenda kwa zaidi na Mhe. Waziri katika maelezo yake nashukuru amelithibitisha hilo na amelitolea maelezo. Lakini kapewa kampuni hii ambayo ilikuwa ime-*tender* kwa milioni 15. Mhe. Mwenyekiti, maelezo yake Mhe. Waziri alisema kwamba hizi kampuni nyengine zilisajiliwa katika kipindi kifupi kabla ya kutangazwa hii *tender*, ni kama vile vimeundwa kwa ajili ya *tender* hizi. Mhe. Mwenyekiti, moja katika hoja zake alizozieleza kwa kuchaguliwa kampuni hii alisema kwamba ni kwa sababu ya uzoefu wa miaka 10. Lakini katika mawazo yale yale akatwambia kampuni hii alipotaja usajili wake hii ya *National Marketing* imesajiliwa mwaka 2006. Kwa hivyo, mwaka 2006 mpaka 2011 ni miaka 5 miaka 10 haijatimia.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana napata wasi wasi kwamba huu uzoefu wa miaka 10 kwa kampuni hii umetokea wapi katika maelezo yake Mhe. Waziri ya majumuisho amesema kwamba kampuni hii imeandikishwa mwaka 2006. Kwa hivyo, katika hili nimuombe Mhe. Waziri awe makini katika maelezo anayotayarishiwa na watendaji wake kwa sababu asipoyafuatilia ndio yanaibua hoja zaidi kama hizi.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba nilisema kwanza kwa maelezo hayo idadi *feat* za *hole argument* ya kwamba kampuni zile nyengine zilikataliwa kwa sababu ziliandikishwa katika kipindi kifupi. Kwa sababu hata hii inaonekana imeandikishwa kwa maelezo yake ni sahihi kwamba ina uzoefu wa miaka 10. Kwa hivyo, kampuni hizi hazikufanya kioja ambacho *National Marketing* haikukifanya, na kama nilivyosema shughuli yenyewe ni ya ubigaji disko. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba anipe maelezo na katika hili naheshimu maelezo yako uloyatoa kabla kuhusu mikataba na kutokatiza mikataba kati kati. Lakini uzuri wa mkataba huu ni kuwa bado mwaka mmoja kwa hivyo ndio nafasi ya ku-*rectify*, lakini kuna ku-rectify kwa maana ya kuangalia upya mikataba hii kwa mwakani, lakini pia kuna ku-*ractify* katika mapato.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu na mimi katika mchango wangu nilisema kwamba mkataba umesema kampuni imekodishwa kwa milioni 15 kwa mwezi, lakini nikasema wanacholipa ni milioni 10. Pia Mhe. Waziri katika maelezo yake amethibitisha hilo. Hoja yake alisema kwamba ulikuwa katika hali mbaya, lakini Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu na nilitumia ripoti ya kamati adhimu ya Mhe. Asha Bakar Makame mwenyewe alisema tumuachia sekta zake, naam tutamuachia lakini natumia hoja yake aliyoileta katika ripoti za kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba na naomba nisome ukurasa wa 79 wa ripoti hii. Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo kifungu cha 2 na kijifungu cha 1 cha mkataba huo umempa dhima mkodishwaji kuufanyia matengenezo ukumbi huo kwa kadiri inavyohitajika ili kuhakikisha mandhari ya ukumbi huo yanatunzwa. Ila kijifungu hicho hakijampa jukumu mkodishaji kubeba gharama za utengenezaji wa ukumbi huo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama palikubaliwa milioni 15 haiwezakani tena mkodishaji wa Hoteli ya Bwawani ikakatwa milioni 5 katika gharama zile ikaambiwa zinaenda kuhudumia matengenezo ya ukumbi kwa sababu mkataba ambao yuko huyo mkodishwaji alishaukubali na uliondoa dhima hiyo kwa mkodishaji. Kwa hivyo, nilikuwa nataka hapa la kuupitia mkataba nadhani baada ya maelezo haya atajipa dhima ya kuhakikisha anajiridhisha ukifika mwisho wa mwaka.

Lakini katika mwaka huu ambao mkataba huu umeshatiliwa hizi milioni 5 namuomba Mhe. Waziri anithibitishie hapa kwamba ili kutunza msingi wa mkataba huu wizara itazidai zote zirejeshwe katika mapato ya serikali. Hizi Mhe. Mwenyekiti, ni fedha za walipa kodi lakini hapo hapo nitashauri kwamba mimi nadhani kwa shughuli kama hii Hoteli ya Bwawani ina uwezo wa kupigisha disko hatuhitaji pahala hapa kwenye mapato makubwa kwenda kumpa mtu mwengine halafu tunai-*disturb* Bwawani mpaka inaendelea kuombewa ruzuku hapa.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba katika hili mambo mawili. Moja ni *commitment* ya Mhe. Waziri kwamba hizi milioni 5 zitarejeshwa kwa sababu mkataba ulivyosema kwamba anabeba mkodishwaji sio mkodishaji. Lakini pili atuhakikishie kwamba katika kuangalia mkataba huu kuwa Hoteli ya Bwawani wenyewe iangalie uwezekano wa kuendesha huduma hizi wenyewe ama pale yanapopatikana kwa wingi mapato yarudi katika Hoteli ya Bwawani, ili kufaidisha walipa kodi wa nchi hii waweze kupata huduma zaidi. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo juu ya masuala hayo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ameeleza mengi Mhe. Mjumbe na kama nilivyoeleza ndani ya majibu yangu na namuhakikishia kwamba mkodishwaji ameshalipa madeni yote ambayo yanahitajika ndio maana tukasema kuwa mwezi wa Ramadhani tutafanya matengenezo yote baada ya kumwambia kwamba yote yale mapya nimeshayalipa hivi sasa. Pia ni kwamba mkataba upo hapa na kampuni tayari tumeshapitisha *tender* tena ambayo itatengeneza mambo hayo, ninayo hapa. Kwa hivyo, namwambia Mhe. Jussa usiwe na wasi wasi kila kitu kiko sawa kabisa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ili niridhike unajua kama nilivyosema nia ni kulinda maslahi ya wananchi wetu, sikumfahamu vizuri nataka aniridhishe tu kwamba hizi milioni tano tano zilizokuwa hazilipwi kwa maelezo yake yeye sasa zimeshalipwa na hata zikilipwa Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwamba nimemfahamu kama amelipa ndio maana maelezo yake yamemchanganya kasema kama kalipa gharama hizi na sasa kuanzia mwezi wa Ramadhani kunafanyiwa matengenezo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba dhima ya mkodishwaji kwa mujibu wa maelezo haya ya kamati yako ni kwamba kwanza ailipe Bwawani milioni 15 halafu nje ya milioni 15 jukumu bado la matengenezo ya ukumbi ni lake kwa mujibu wa maelezo haya.

Kwa hivyo, kama fedha wenyewe ndio imechukuliwa katika hizi kwenda kutengeneza itakuwa ndio ile ile kwamba mkodishwaji anakata katika mapato ya Bwawani halafu unatengeneza ukumbi. Mhe. Mwenyekiti, niseme kama ukumbi huu umechafuka basi itakuwa ameuchafua yeye kwa sababu kama nilivyoambiwa hapa anao miaka kadhaa, haiwezekani Bwawani ikabebeshwa dhima ya matengenezo. Mhe. Waziri mimi nasema hebu niwekee wazi kwamba hizi fedha za matengenezo ni nje ya milioni 15 au ndio hizi milioni tano tano amezirejesha naomba uniwekee wazi Mhe. Waziri kwa ufasaha kabisa ili turidhike sisi na wananchi wetu tunaowawakilisha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba hizi ambazo amelipa hazimo kabisa, hizi ni kutoka kwake ni madeni yake yote hazitoki katika mfuko wa Bwawani. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba karatasi ninayo na mkataba ninao na kila kitu wewe usiwe na wasi wasi mimi nitalisimamia hili suala kidedea na unalielewa hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru mimi nilipokuwa nikichangia kuhusu wafanyakazi ambao bahati nzuri kama ambavyo wajibu wao ulivyo wizara huwapeleka katika Chuo cha Uandishi wa

Habari, lakini kwa bahati mbaya huwa hawalipii kikamilifu. Kwa hivyo, wafanyakazi hawa husitishwa kwenye masomo katika chuo kile ambacho wao ndio wamiliki na matokeo yake chuo kinamilikiwa na waandishi wa habari wa binafsi.

Kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri hakutueleza vizuri mambo haya, hebu naomba atupe ufafanuzi kidogo inakuwaje chuo ambacho wizara inakimiliki inapeleka wafanyakazi kufunzwa mafunzo ya uandishi wa habari, lakini hawawalipii kikamilifu na matokeo yake husitishwa na chuo ikawa sasa kinatawaliwa zaidi na wanafunzi kutoka sekta binafsi. Mhe. Waziri naomba utupe taarifa kuhusu hawa wanasitishwa masomo yao ambao ni wafanyakazi wako hutokezea vipi na bajeti unatwambia tukupitishie hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba chuo kinamilikiwa na Mamlaka ya Wizara kwa ufupi na kwa kweli sina taarifa hiyo kama kuna watu wamekatishwa masomo, mimi taarifa hiyo sina lakini nipe muda ntaichunguza ipo kweli au kama haipo. Lakini mpaka sasa hivi sina taarifa hiyo, lakini chuo bado kiko mikononi mwa wizara hii, hivyo nakuomba Mhe. Mjumbe nistahamilie ili nilitizame hili suala kama lipo au halipo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, haya mambo sio mapya kwa sababu mimi nilichangia tokea jana, kwa hiyo inaonesha kwamba kazi haikufanywa, ikiwa nimuachie Mhe. Waziri ni imani yangu tu lakini ilikuwa yeye madhali maneno niliyasema jana ilikuwa akayafanyie kazi ili aje na jibu kamili. Mhe. Mwenyekiti, sasa sijui nifanye nini, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 0401	Idara ya Utumishi na Uendeshaji	637,340,000
Kifungu 0402	Chuo cha Habari	290,000,000
Kifungu 0403		

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia uhai na uzima. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hoja pale alijibu hoja nzuri sana akasema kuwa hawa wafanyakazi wa gazeti hili ameshawalipa mafao yao. Lakini ukweli uliopo mpaka leo hii ni kwamba hawajapata posho lao namuomba Mhe. Waziri katika ulipaji wake alizipeleka wapi hata mpaka leo hii hawajapata hao wafanyakazi wanaendelea kudhalilika tu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, taarifa niliyonayo ni kwamba hawa watu wameshalipwa kila kitu, sasa kama kuna wengine ambao hawajalipwa taarifa hiyo sina lakini hata hivyo

namuomba Mhe. Mjumbe aniidhinishie hili baada ya bajeti hii niwamalizie kile kitu wala asiwe na wasi wasi. Lakini mpaka hapo nina imani kwamba nimeshawalipa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na Mhe. Waziri kwamba amedanganywa na kwa vile Mhe. Waziri ameniahidi kuwa kama wako waliokuwa hawajalipwa na yuko tayari kuwalipa basi hili mimi sina pingamizi nalo, lakini aelewe kuwa suala hili amedanganywa na kuna watu bado hawajalipwa mpaka leo na wanaendelea kudhalilishwa. Kwa hivyo, naomba mheshimiwa kwa jitihada zake ninavyomjua naomba tuendelee.

Kifungu 0403	Mchango wa Gazeti la Zanzibar Leo	815,000,000
Kifungu 0404	Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la Chuo cha Maendeleo ya Utalii na umuhimu wake na hali yake ilivyo hivi sasa. Nikaeleza kwamba katika bajeti iliyopita Mhe. Waziri alituomba tumuidhinishie shilingi milioni 500 kwa ajili ya maendeleo ya chuo na mwaka huu ametuomba shilingi milioni 400 kwa shughuli hizo hizo za mandeleo ya chuo. Lakini ukiangalia kwenye bajeti ya Mhe. Waziri hajatueleza moja kwa moja ni kiasi gani cha fedha alichopata katika zile milioni 500 na hayo maendeleo ambayo yamefanyika na kwa sababu tunaona hakuna mabadiliko yoyote hali bado inaendelea vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii bado anaendelea kutuomba milioni 400 tumuidhinishie. Kwa hivyo, tumekuwa na wasi wasi juu ya hizi fedha ambazo anaziomba kila mwaka pengine anaweza kuwa hazipati lakini hajatueleza kwenye bajeti yake, pengine anazipata lakini matumizi yake anaweza kuwa sio mazuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba atueleze katika fedha alizopewa mwaka jana milioni mia tano katika bajeti hii amepata kiasi gani kutoka Wizara ya Fedha na zimefanyiwa shughuli gani hasa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tulipata hizo milioni 500 na tulifanya mengi kwa kweli marekebisho ya chuo kama unavyokiona hivi sasa hali yake. Vile vile nilieleza kwamba kuna makusanyo ambayo tumeyapata ambayo tumeyaeleza katika hali ya takwimu lakini labda Mhe. Mjumbe hakuyaangalia vizuri yamo humu katika takwimu zetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe aangalie vizuri kiasi gani tumekusanya.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, bado sijamfahamu vizuri Mhe. Waziri labda arudie kidogo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Nimesema makusanyo yote tumeyaeleza kitakwimu hatukutaka kufanya kama vile alivyotaka kama alivyoeleza Mhe. Haji Faki Shaali jana, tumeeleza katika hali ya kitakwimu hatukufanya ile *break down*. Kwa sababu ya kufupisha ile ripoti nzima. Kwa hivyo nafikiri aangalie vizuri zaidi katika masuala ya takwimu.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nilichoona mimi katika maendeleo ya chuo ni maeneo mawili, ambapo eneo moja fedha zilizotumika ni shilingi 74,255,000/- na eneo jengine ambazo zimeshughulikia na masuala ya maendeleo ya utalii ni shilingi 79,180,096/-; ambazo total ni shilingi 153,435,096/-. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu atwambie maeneo mengine yepi licha ya hayo maeneo mawili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sisi tulijaribu kuyakusanya yote kwa ujumla, lakini kama anahisi Mjumbe hayapo basi labda kutakuwa kuna nini, lakini makusanyo tumepata na tumeyaidhinisha ndani ya takwimu vile vile. Kwa hivyo, labda Mhe. Mjumbe anipe muda niangalie zaidi ili tutizame kama yamo au hayamo, lakini nina hakika kama yamo makusanyo. Nipe muda Mhe. Mjumbe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, mimi sizungumzii mapato yanayotokana na kitu, nazungumzia fedha za maendeleo za shilingi 500 milioni ambazo Mhe. Waziri amekiri kwamba hizo fedha wamezipata zote na ukiangalia kiambatanisho Nam. 4 ya hotuba yake fedha zilizotumika katika masuala ya maendeleo ni jumla ya shilingi 153,435,096/-. Je, hizi fedha zilizosalia zimetumika kwa nini kati ya shilingi 500 milioni.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nasema kwa mujibu wa takwimu zilizowasilishwa na wizara kwenye viambatanisho mwishoni mwa hotuba hii ya bajeti kuna kiambatisho Nam. 1(a) ambacho chini ya Idara ya Mipango na Sera kuna *item* ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii, ambapo kiambatanisho Nam. 1(a) kinazungumzia fedha zilizoingizwa hadi Aprili 2011 kwa matumizi ya kawaida. Kwa Chuo cha Utalii ni shilingi 120 milioni ambazo ni sawa na asilimia 63 hiyo iko kwenye ukurasa wa 74.

Halafu ukurasa wa 75 ambacho ni kiambatanisho 1(b), fedha zilizoingizwa hadi mwezi April, 2011 kwa kazi za maendeleo, Chuo cha Maendeleo ya Utalii ni shilingi 250 milioni kati ya shilingi 500 milioni ambazo ziliombwa na ambazo ni asilimia 50. hiyo ilikuwa ni mwezi April hadi April 2011. Kwa hivo, zimeambatanishwa au zimeoneshwa kwa uwazi kabisa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, nadhani hamjanielewa, ninachosema kwamba akiangalia Mwanasheria kiambatanisho Nam. 4 hiki

kimetoa mchanganuo juu ya fedha zilizoingizwa kwa ajili ya kufanya ukarabati na vifaa vyengine vya kompyuta ambapo *total* ni shilingi 153 milioni. Sasa mimi sitaki mafungu ya jumla, nataka kilichosalia hapa katika pesa hizi ambazo zimetolewa, zimetumika kwa ajili ya nini na kwa sababu bado hali ya Chuo cha Maendeleo ya Utalii kinaonekana hakiridhishi. Bahati nzuri serikali imetoa fedha za kutosha kwa ajili hiyo. Sasa mimi nilikuwa nahitaji anipe matumizi ili niweze kumuidhinishia na hizi shilingi 400 milioni ambazo ameomba, vyenginevyo nitakuwa mgumu kuidhinisha fedha hizi, ambapo zile zilizotolewa mwaka jana hazieleweki matumizi yake.

Kwa hivyo, ili tumuidhinishie hizi nikubali kuzitumia hizi shilingi 400 milioni za mwaka huu tupate mahesabu ya matumizi ya mwaka uliopita wa shilingi 500 milioni ambazo Mhe. Waziri amekiri kwamba amezipokea, lakini ukiangalia mchanganuo katika kifungu cha 4 ni shilingi milioni 153 tu, ambazo zimetumika. Sasa zilizosalia zimetumika kwa ajili ya nini, hiyo ndio hoja yangu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, fedha zote zilizopatikana ni shilingi 250 milioni na zote tumezifanyia ukarabati wa majengo pamoja na ununuzi wa vifaa vyote.

Mhe. Mwenyekiti: Tatizo Mhe. Waziri na hoja ya Mhe. Mjumbe pale hebu jaribu kuangalia kiambatanisho Nam. 4 ukurasa wa 78. hapo kuna ukarabati wa Chuo cha Maendeleo ya Utalii, hapo palipoandikwa nambari 3, 2011 kwamba fedha iliyotumika ni shilingi 74,255,000/-, halafu upatikanaji wa vifaa vya Chuo cha Maendeleo ya Utalii hapa kuna shilingi 79,180,096 nafikiri ni sawa Mhe. Salmin. Jumla ya hii ndio anasema shilingi 153 milioni wakati zilizopatikana ni shilingi 250 milioni. Sasa hizi nyengine mwenyewe anauliza pale zimetumika wapi?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe nimletee hii kwa maandishi.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea lakini na ahadi hiyo ya kuleta mwa maandishi kwa kuwa ameitoa basi uletewe kwa maandishi.

Kifungu 0401	- Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	400,000,000/-
Kifungu 0501	- Sauti ya Tanzania Zanzibar	541,000,000/-
Kifungu 0601	- Idara ya Televisheni	

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipatia nafasi kidogo ya kuweza kutoa maoni yangu kidogo. Kwa sababu wakati jana

nachangia Mhe. Spika, nilizungumzia suala zima la jinsi ya Televisheni Zanzibar ilivyokuwa haisikiki kule Pemba. Nilieleza wazi kwamba wale Wazanzibari wanaoishi Pemba wanalipa kodi sawasawa na wenzao wanaishi hapa Unguja. Lakini huu ni karibu mwaka wa nne hawajaona Televisheni Zanzibar kule. Kwa mnasaba huo Mhe. Mwenyekiti, nikamueleza wazi waziri kuwa kufanya hivyo anakwenda kinyume na mambo matatu, kwanza anakwenda kinyume na Katiba zote mbili ikiwemo ya Jamhuri ya Muungano wa Zanzibar na pia anakwenda kinyume na dhamira halisi ya Mapinduzi ya mwaka 1964 halikadhalika ana-*violate* hii *spirit* ya *GNU* ya kuleta kuleta *unit* ndani ya Zanzibar. Kwa hivyo, mambo matatu haya wame-*violate.*

Mhe. Mwenyekiti, naomba unuruhusu niende kwenye ibara ya 12, kwa sababu jana nilinukuu Katiba ya Jamhuri ya Muungano leo naona ninukuu Katiba ya Zanzibar.

Ibara ya 12 kifungu cha I na 5 kinasema:

> "Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria".

Kifungu cha 5 maana ya neno kubagua. Maana ya neno kubagua Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, wakati tupo kwenye Kamati ya Matumizi Mjumbe anaruhusiwa kusimama kutaka ufafanuzi sio kuanza kuchangia tena. Tunaomba ulinde kikao hiki ili twende na utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Saleh Nassor Juma nenda kwenye hoja yako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Niko katika kuya-*elaborate* tu ili kuyaweka sawa katika hili. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili la kuwanyima haki Wazanzibari walioko Pemba kwa maana ya Wapemba ni tatizo kubwa. Kwa hivyo, namtaka Mhe. Waziri sasa hivi anieleze ni lini Wapemba wataisikia na kuiona televisheni.

Halikadhalika katika mchango wangu nilieleza vile vile kwamba watendaji wetu katika wizara hii hiyo *technical team* ya Mhe. Waziri wanaonekana sio *creative,* ningeomba radhi kwa sababu sioni neon jengine la karibu, lakini sio *creative* kwa sababu wakati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere anaacha

madaraka pale katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kulikuwa hakuna TV hata moja, hivi sasa kuna TV nyingi tu Tanzania Bara. Lakini wakati Marehemu Mzee Abeid Amani Karume anafariki hapa katuachia TV ikionekana kila pahala, leo hii haionekani Pemba Televisheni Zanzibar. Kwa hivyo, nataka Mhe. Waziri anieleze ni lini Wapemba wataweza kuona na kuisikia Televisheni Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri labda nilipokuwa natoa majumuisho alikuwa hayupo, lakini kwa faida yake tu nimueleze kwamba tunajua hilo na ni suala ambalo linaniuma. Ilikuwa tuweke mitambo zamani sana kule Pemba lakini kwa sababu hii mitambo ilikuwa ina *expire date* yake ambayo haiku mbali, tukaona hakuna faida ya kuweka mitambo ambayo keshokutwa ina *expire*, tukaona tusubiri ya *digital* kabisa tukiifunga tufunge ya moja kwa moja ndicho tulichokifanya tu sisi hicho. Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba asiwe na wasiwasi mwishoni mwa mwezi huu au mwanzo mwa Agosti mitambo yote itakuwa imeshafungwa na wananchi wa Pemba nao vile vile watafaidika na mitambo hiyo asiwe na wasiwasi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, nilichokihitaji kwa sababu hapa tayari tumeshapata maneno mengi, kesho itafungwa, mwenzi ujao itafungwa na neno tendo hukidhi haja maridhawa kuliko neno Mhe. Mwenyekiti, haja ikishughulikiwa kwa matendo hupatikana wepesi, lakini ikishughulikiwa kwa matendo huchelewa kama sadaka. “Kula uhondo kwataka matendo Mhe. Mwenyekiti, asiye matendo hula uvundo”. Kwa hivyo, anieleze kwa matendo lini watafunga mtambo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoweza kumueleza ni kwamba tumeshaahidi hapa na haya masuala yalikuwa yanaulizwa siku zote katika kipindi cha maswali na majibu, nilimwambia mwishoni mwa mwezi wa Julai au mwanzoni mwa Ogasti tunafunga mitambo hii kwa nini ana wasiwasi. Tutaifunga Mhe. Saleh Nassor usiwe na wasi wasi, hebu niamini.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, ni waangalizi wa matumizi ya walipa kodi wa nchi hii, sasa inakuwaje serikali kuwa *bias*, kwa maana ya kwamba Wapemba wanalipa kodi na kodi yao inatumika katika kuchangia hiyo Televisheni Zanzibar, wenzao wa Unguja wanaona wao hawaoni. Hii ni *biasness*, ndio nilikuwa nase,a tu kwamba aji-*commit* yeye mwenyewe waziri lini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Sale Nassor kwamba serikali hii sio *bias.*

Serikali hii inawajali wananchi wote wa Unguja na Pemba na ndio maana ikachukua hatua ya kuhakikisha kwamba kununua mitambo kwa upande wa TVZ Pemba iweze kufanya kazi. Sio hayo tu, kila jambo la maendeleo ambalo linafanywa Unguja na Pemba linafanywa.

Vile vile nataka nimhakikishie hivi karibuni tumezindua umeme kutoka Pangani kuja Pemba hivi sasa Pemba hakuna tatizo la umeme ukilinganisha na Unguja. Kwa hivyo, serikali hii ipo kwa ajili ya kutumikia wananchi.

Kuna neno moja Mhe. Saleh alisema kwamba, Wapemba hawaoni TV. Ningependa nimkosoe mimi ni Mpemba na ninaiona TVZ. Watu walioko Pemba ndio ambao kwa sasa hawapati kuona TVZ na jitihada zinachukuliwa ili TVZ ionekane.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tunapohoji kuhusu mapato na matumizi ya serikali tusionekane kwamba tunaahirisha shughuli za Baraza, isihesabiwe kama serikali inavyotuona kwamba, tunapohoji sisi hatudhoroteshi shughuli za Baraza, lakini tunahoji juu ya matumizi mazuri ya walipa kodi wa nchi hii ambao sisi ndio waliotuleta hapa. Basi baada ya maelezo hayo nadhani tuendelee.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia Idara hii nilisema kwamba kuna taarifa mbali ya wafanyakazi halali walioajiriwa Idara ya Televisheni, lakini serikali hupeleka wafanyakazi wengine kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kama vile Vikosi vya SMZ. Lakini wakifika pale tena huwa tabu kuondoka na huongeza mzigo kwa wafanyakazi wa televisheni. Nilipoangalia maposho hapa posho maalum nimeona kutoka shilingi laki sita mwaka jana mara hii ni shilingi 13,200,000/-. Ni dhahiri kwamba wale wafanyakazi ambao si waajiriwa wa pale watakuwa wengi zaidi kwa hivyo naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: samahani Mhe. Mwenyekiti, naomba anieleze tena kwa sababu sikumpata vizuri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilihoji kwamba idara hii mbali ya wafanyakazi wale halali wa televisheni, lakini serikali hupeleka wafanyakazi wengine kwa ajili ya mafunzo ya vitendo kama vile Vikosi vya SMZ. Lakini wakifika pale tena hawaondoki tena hubakia pale pale, husababisha mzigo sasa kwa wale wafanyakazi halali wa idara ile. Nilipoangalia maposho maalum hapa nimeona kutoka shilingi laki sita mwaka jana limeongezeka shilingi 13,200,000/-. Tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake wale wafanyakazi ambao si waajiriwa wa pale watakuwa wengi zaidi. Sasa naomba ufafanuzi lini

wataondoka pale ambao si waajiriwa wa pale ili kuwapa nafasi wenzetu wa televisheni kufanya kazi zao kwa utulivu na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Hija kwa wale wa vikosi waliokwenda kwa mafunzo na mafunzo inakuwa kipindi maalum, basi mimi hilo namhakikishia nitalifuatilia mwenyewe nione kwamba wameshahitimu wataondoka mara moja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hata ukiona suala nimelipata mimi ninaekaa Mwambe basi si jambo la kufuatilia ni jambo la kunambia tu lini wataondoka. Kwa sababu wanajua kama wapo, lakini kwa sababu wameniahidi naomba baadae akishawaondosha aniarifu nimewaondosha. Tuendelee mbele.

Kifungu 0601 - Idara ya Televisheni

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Wakati nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba siwalaumu mimi pengine mafunzo hawana wafanyakazi vya kutosha kuhusu namna ya kupangilia vipindi. Wengine wakasema hata taarifa za habari zenyewe zinakuwa finyu sana. Je, Mhe. Waziri atatueleza vipi alivyojipanga kufanya marekebisho haya na tuyaone kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, tumeliona hilo na namuahidi Mhe. Mjumbe. Tunasema kwanza ni matatizo ya vifaa wakati mwengine yanasababisha udhaifu huo, lakini kwa sababu tutafunga vifaa vipya basin a masuala mengine yatayofuatia vile vile tutayarekebisha kwa hali na mali ili tuhakikishe kwamba tunakwenda sambamba pamoja na upya wa vifaa. Kwa hivyo, namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba asiwe na wasiwas tume katika mikakati ya kuwapa taaluma watendaji wetu pamoja na kujipanga upya.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, kwa kutoa nafasi ya Mhe. Waziri tuendelee.

Kifungu 0601	- Idara ya Televisheni	648,400,000/-
Kifungu 0701	-	

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Wakati nachangia hoja hii niliuliza juu ya tatizo liliopo la wizara ama serikali kutokuwa na hatimiliki ya picha ya rais. Mhe. Mwenyekiti, picha ya rais ni muhimu sana, kwa sababu ukiachia mbali bendera kama utambulisho wa nchi kinachofuatia ni picha ya rais na ndio maana kila wizara ama idara ya serikali

hutakiwa iwepo picha ya rais. Hii ina maana mmbili kubwa, maana ya kwanza ni suala la usalama wa nchi lakini suala la pili ni suala la kiuchumi. Sasa Mhe. Waziri kakubali kwamba wizara haina hatimiliki ya picha ya rais na baya zaidi ni kwamba umiliki wa picha hii ina mtu wa kawaida tena raia wa kigeni.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hivi serikali haioni kwamba hili ni tatizo na hasa tukichukulia kwamba wizara tunavyofahamu kiko kitengo cha wapiga picha na kina wapiga picha ambao ni *qualified*. Sasa hivi kwa nini serikali haimiliki picha ya rais. Yule raia wa kigeni leo akienda akiifanya anavyotaka nchi yetu itakuwa katika hali gani, si itakuwa iko kwenye mnada. Naomba majibu ya serikali.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ninavyoelewa mimi ni kwamba picha za rais wenye mamlaka ni Idara ya Habari Maelezo na tumeshafanya hivyo hivi sasa tunaziuza na tunazisambaza maofisini, hakuna mtu mwengine zaidi. Sasa kama mtu atafanya hivyo basi itakuwa ni kinyume na utaratibu, lakini utaratibu ni kwamba Idara ya Habari Maelezo ndio wanaopiga picha hizo na wanauza kwa kuwauzia taasisi nyengine.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, si suala la kununua na kuuza picha, mimi ninachokiulizia ni yule mwenye hatimiliki ya ile picha yenyewe *original*, maana yake picha si kwamba rais kila pahala tu anapiga picha kunakuwa na picha moja tu ndio inayotumika na rasmi katika shughuli hizi za kiserikali. Sasa ninachoulizia mimi ile picha miliki *original* anayo nani? Kama ikiwa Wizara ya wanayo hatimiliki ya ile picha yenyewe sina tatizo, lakini ikiwa haina naomba jawabu katika hili.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, suala la hakimiliki ni suala la kisheria. Katika picha ya mtu hakuna mwenye hakimiliki, si mwenye picha siye aliyepiga picha. Aliyepiga picha ana haki inaitwa *right of fixation*, yaani ile haki ya kupiga ile picha yenyewe akaiweka katika *medium* aliyoiweka kama ni karatasi, ubao au bati. Sasa haki ile sheria ya hakimiliki inamtambua. Lakini kwenye hakimiliki msingi wake ni kwamba ni ile haki ya ubunifu. Sasa mimi sijabuni sura yangu, wala hakuna mtu aliyebuni sura yake.

Kwa hivyo, hana hakimiliki juu ya ile picha yake ana *right of privacy* kama mwenyewe hataki kupigwa ile picha na ana *moral right* ya kwamba ile picha isitumike vibaya vile vile sheria inatambua hilo. Lakini hakuna mwenye hakimiliki ni masuala ya kukubaliana baina ya aliyepiga picha *original* ambaye ana *right of fixation* na ambaye sheria inamlinda na ana haki ya kukataa mtu mwengine asiitumie.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu ni dogo sana wala sio kubwa, nataka kujua tu mwenye hii picha ya rais *original* yake hii picha ina nani? Taarifa tulizonazo ni kwamba ina raia wa kigeni, sasa tunachotaka kwamba serikali inayo umiliki wa picha ile au haina. Picha ya rais ni tofauti na picha yangu mimi au picha ya mtu mwengine, yule ni kiongozi wan chi lazima kuwe na utaratibu maalum wa picha ile sio mtu tu wa kawaida mitaani huko. Sasa tunachotaka kwa usalama wa taifa letu na rais wetu ili picha tuondokane na matumizi mabaya serikali ijibu kama wanayo hatimiliki ya picha ile au hawana. Hilo tu ndilo ninalolihitaji.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, picha anayosema Mjumbe picha hii nakumbuka kwamba aliyepewa *contract* ya kupiga kuna mpiga picha mmoja anaitwa Raj. Sasa picha hiyo alipiga na hiyo *original* anayosema ipo na iko Ikulu. Sasa kam aanataka kwenda kuiona Mhe. Mjumbe tutampeleka ili akaione.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hii hoja ni muhimu sana na kwa sababu kuna maneno na kama nilivyoeleza hivyo, na kwa sababu hili ni suala la kiuchumi la kibajeti, kwamba wao wanauza picha lakini baadae watwambie kwamba picha hizi wao wananunua kiasi gani, kama hivyo ndivyo nilivyoeleza mwanzo.

Sasa hoja yangu ni kwamba, ikiwa picha ipo na kwa sababu ni hoja imekuja mbele ya Baraza lako tunahitaji kama Baraza tuione picha hiyo, waje nayo katika Baraza lako.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Ikulu kuna *respect* yake, hiyo picha iko Ikulu, sasa kama haamini tutamchukua tukamuoneshe picha hii hapa. Lakini huwezi kutoa vitu vya Ikulu ukavileta hapa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nadhani tunakaribia kuafikiana na *concern* yangu nadhani imefahamika vizuri. Kama ikiwa haipo kwa sababu mimi sidai picha Mhe. Mwenyekiti, nadai ile original yake ambayo ndio unayoizalisha ndio hicho ninachokidai mimi, sidai picha ya Ikulu kwenda kutunguliwa nikaoneshwa aa. Kama ikiwa haipo tunaiomba serikali iandae utaratibu imiliki picha hii. Ahsane tuendelee.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, nafikiri watu watatu wameshamalizika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama mawaziri wako wengine wamechoka unaweza kuwaruhusu wakenda wakapumzika nje wakaja na vitu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, katika mchango wangu nilipokuwa nikizungumzia Sekta ya Habari kwa ujumla wake nilizungumzia suala zima la haja ya kuwawezesha wafanyakazi hasa kwa maana ya waandishi juu ya kuwapatia posho zao. Sasa hili naliomba kwa ujumla wake tu nipewe maelezo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alizungumza hapa kuhusu Idara ya Televisheni lakini Idara ya Habari Maelezo kuna suala hilo hilo kwamba bajeti ya posho maalum imevimba sana, tumetoka shilingi 852,00 mwaka jana mpaka imekuwa milioni 13 mwaka huu. Kwa takriban zaidi ya asilimia 1,000 ndani ya mwaka mmoja ndio ongezeko lake. Inafanana na ile ya *Television Zanzibar* aliyoisema Mhe. Hija ambayo ilitoka shilingi laki sita mpaka milioni 13.2.

Sasa mimi naomba kwa ujumla katika hii Idara ya Habari Maelezo tuambiwe hii posho maalum inakwenda kwa waandishi, inakwenda kwa wakubwa wa idara. Maana yake ndio lile tatizo nililosema kwamba mara nyingi mambo haya unashtukizia yanawafaidisha wakubwa wa idara hizi lakini waandishi kama tulivyoelezwa humu wanaendelea kuwekwa humu kutwa nzima wanawajibika lakini posho zao hazipatikani.

Sasa naomba kama ongezeko hili la zaidi ya asilimia 1,000 katika idara mbali mbali za Sekta ya Habari zinalenga kuwalipa malimbikizo ya maposho yao wafanyakazi hawa. Naomba maelezo kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi maalum kama tulivyoeleza kipo pale kama ni *contingency*. Iwapo itatokezea haja ya kuwalipa basi tutatoa mle mle hamna matatizo. Kwa hivyo, Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi zile taratibu za kuhaulisha zipo ikionekana haja basi tutazitoa na tutawalipa haki zao.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu haya mepesi mepesi tu ya Mhe. Waziri wasi wasi utaendelea kuwepo. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema *contingency* inatajwa hivyo hivyo katika bajeti kwamba ni *contingency*. Mhe. Mwenyekiti, nasaidiwa na wazoefu kwamba inakuwa ni asilimia 10. Lakini unapoona fungu la posho maalum, kama nilivyosema nimezuilia hapa lakini katika televisheni lipo hili, katika Idara ya Habari Maelezo lipo, ukija katika Kamisheni ya Utamaduni na Michezo pia lipo hivi hivi limevimba ghafla linaruka kwa asilimia 1,000.

Mhe. Mwenyekiti, haya si maelezo ya kutupa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaowawakilisha wananchi, tunaosimamia fedha za walipa kodi. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anambie fungu hili litakwenda kutiwa kama ikitokezea haja, haja ipo wana madeni tumesema hapa. Litakwenda kuwalipa badala ya kuwanufaisha asilimia kubwa, litakwenda kuwalipa wafanyakazi wa idara hizi ili waweze na wao kufanya kazi kwa motisha ambayo wanastahiki kuzipata. Mhe. Mwenyekiti, naomba majibu makini.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kifupi ni kwamba kifungu hichi maalum sisi tumo katika kutanua kasi na makusudio ni kuwalipa watu wote madeni yao si kwa sababu ya mtu maalum. Tumeweka kwa sababu iwapo inapotokezea haja kuna watu hawajalipwa basi tutatoa katika kifungu maalum kile ili kuwalipa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi niko *serious*.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naendelea kumwambia tena haya majibu anayapenda sana Mhe. Waziri si leo tu, usiwe na wasi wasi ukasema kwa majibu mepesi mepesi kama haya utaendelea kuwepo. Wasi wasi utaondoka Mhe. Mwenyekiti, ikiwa tutapata majibu makini na yanayotosheleza kiu zetu. Hili naomba nimwambie kwa jumla tu.

Lakini pili nasema najua hata nikifanya vipi kwa maelezo haya sipati majibu. Mhe. Mwenyekiti, naomba tuendelee lakini naomba mwakani mafungu haya ya posho maalum tutakuja kupewa matumizi tupate *breakdown* zilizopo hasa za fungu hili lote, mwakani katika bajeti hatuna haraka Mwenyezi Mungu akituweka hai na uzima. Kama nitakuwa nimeshatangulia mbele ya haki nitamuomba Mhe. Mansoor Yussuf Himid aje aninong'oneze pale kwenye kaburi langu.

Lakini naomba sana kwamba katika haya mafungu aje atuletee maelezo juu ya posho maalum zimetumikaje. Kwa sababu katika maelezo yake sasa hivi hayatoshelezi, lakini sitaki kuendelea kukwamisha naomba twende hivi hivi tutoe maelezo ya kina juu ya matumizi ya mafungu haya ambayo yamechupa kwa zaidi ya asilimia 1,000 katika makisio ya mwaka uliopita na mwaka huu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nataka niungane na Mhe. Waziri na kumhakikishia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba fungu hili wameliweka kwa kuzingatia hayo madeni ambayo wajumbe walikuwa wanatetea sana wafanyakazi hasa waandishi wa habari na wale ambao wanakwenda kufanya kazi katika mazingira magumu. Kwanza hilo nataka nikubaliane na nakubaliana na *concern* ya Mhe. Mjumbe.

Lakini wasi wasi wake kwamba pengine fungu hili limetunishwa kwa ajili ya kuwalipa wakubwa tu na kuwaacha wale wafanyakazi hasa wale wanaoingia katika *shift* kwenye taasisi zote za habari kama televisheni, redio na sehemu nyengine.

Lakini kama atakumbuka Mhe. Ismail Jussa Ladhu nilipokuwa nikiwasilisha hotuba yangu ya bajeti na nilipokuwa nikitoa majumuisho nilisema kwamba serikali kupitia wizara yangu tutapitia upya maposho yote ya wafanyakazi na watumishi wa serikali. Yale ambayo tunayahisi yana mapungufu yaani hayastahili kulipwa, basi serikali itayapitia upya na itayaondosha yale ambayo hayastahiki.

Kwa hiyo, hili wasi wasi wake Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba pengine maposho haya yatakuwa yanawalipa wakubwa mimi nadhani yeye kisharuhusu, lakini nataka nilihakikishie Baraza kwamba hivi sasa tuko katika zoezi la kupitia maposho yote ya watumishi wa umma na *breakdown* itawekwa na serikali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nilitilie mkazo ni kweli kwamba unaweza ukakuta katika taasisi kumewekwa maposho nyeti, lakini posho nyeti pengine liko kwa dereva wa mkurugenzi wa kawaida, lakini kwa muendesha *ambulance* hakuna posho nyeti. Sasa mimi nadhani hili kama nilivyosema kwenye bajeti yangu ni kwamba serikali kwa ujumla wake inayapitia maposho yote, yale ambayo yanaonekana hayastahili kulipwa basi serikali itayaondosha hata kama yamo ndani ya bajeti. Pesa hizo serikali itazielekeza kwenye matumizi mengineyo. Nilisema kwamba taarifa hiyo itawasilishwa hapa Baraza la Wawakilishi.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Ismail Jussa Ladhu pamoja na wajumbe wako wote wa Baraza hili tukufu waelewe kwamba zoezi hilo lipo na wala sikusema kwa utani. Ni mpango wa serikali kuyapitia maposho yote ili kuhakikisha kwamba yule anayestahiki kulipwa posho analipwa na yule ambaye hastahiki basi aondoshewe posho hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilishakubali kwamba tuendelee kutokana na haya maelezo. Lakini nataka kusema kitu kimoja tu kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ametoa ufafanuzi huu. Haya ndio majibu ambayo tungeyategemea kutoka kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo. Lakini kinachojitokeza hapa Mhe. Mwenyekiti, ndio ule wasi wasi kwamba tulitegemea nilishikilia fungu hili, ukisoma hichi kitabu tulipoanza hoja hii tumeambiwa fungu hili linatumiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na

Michezo. Anayemwakilisha huyu anayewajibika kwetu sisi ni Mhe. Waziri wa Habari.

Mhe. Spika, nilitegemea Mhe. Waziri anapokuja kuomba idhini ya mafungu hapa yeye mwenyewe kwanza ameyakamata, sasa leo tunachoambiwa ndio kama hicho kwamba maelezo ya Mhe. Waziri anayeshughulikia Utumishi wa Umma na Mhe. Waziri anayekuja kuyaombea mafungu haya tulitegemea atupe kuliko yale majibu ya jumla jumla. Kwa hivyo, nashukuru kwa maelezo yale na nasema kwamba hili liwe fundisho sio kwa waziri huyu tu lakini mawaziri wote wanaokuja kwamba mafungu yao wanapokuja kuyaombea hapa wawe wenyewe wameya-*master* wanayajua. Kwa sababu sisi tunayachukua maelezo ni sawa serikali inawajibika kwa pamoja tunakubali, lakini tunategemea umakini wa yule waziri katika wizara ile kwamba awe anayajua.

Mhe. Mwenyekiti, katika hilo niseme kwa jumla ndio hili tatizo kwamba majibu mengi yanayokuja mepesi mepesi katika wizara hii inaonekana kama vile Mhe. Waziri huwa hajitumi kwenda kufanya utafiti wa mambo kama haya, ndio maana mara nyengine anatwambia anataka kutuletea majibu kwa maandishi katika vifungu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, tunayakubali maelezo ya Mhe. Waziri anayehusika na Utumishi wa Umma na Utawala Bora lakini hebu mawaziri wanapokuja hapa wawe *serious* wao wenyewe wamejiandaa wanayajua mafungu wanayoyaombea tunapoomba maelezo watutosheleze. Ahsante sana.

Kifungu 0701	Idara ya Habari Maelezo	202,000,000
Kifungu 0702	Tume ya Habari na Utangazaji	160,000,000
Kifungu 1101	Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale	300,760,000
Kifungu 1201		

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nachangia kifungu hichi cha Kamisheni ya Utalii na Michezo nilizungumzia suala la viwanja. Mbali na majibu ambayo alinipatia Mhe. Waziri lakini bado sijaridhika.

Mhe. Mwenyekiti, mwezi wa Januari, 2012 vilabu vyetu vitakuwa vinashiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa ya Afrika pamoja na Kombe la Shirikisho.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa vilabu vimeshaanza kusema kwamba sisi hatushiriki mashindano hayo. Kwa mfano klabu bingwa ya Mafunzo wameshasema hawashiriki kwa sababu hatuna viwanja. Inabidi timu zile ziende Dar es Salaam ambapo zinaongeza gharama za matumizi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna timu moja ya Jamhuri ambayo inatoka Pemba na timu moja ambayo itatoka hapa Zanzibar bado haijajulikana kwa sababu kila mmoja anapewa nafasi anakataa kutokana na gharama.

Swali langu liko hapa Mhe. Mwenyekiti, ni lini Mhe. Waziri atatwambia kwamba viwanja hivi vitakuwa tayari kabla ya mwezi wa Januari ili vilabu vyetu hivi vipate kucheza mashindano haya katika nchi yao. Timu ya Jamhuri icheze Pemba katika Uwanja wa Gombani ambao uko katika Jimbo la Wawi na timu ambayo itakubali kushiriki mashindano hayo hapa Unguja itumie Uwanja wa Amaan.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali kwamba siwezi nikamwambia lini *exactly* vitakuwa tayari viwanja hivyo kwa sababu viko kwenye matengenezo. Lakini nina imani kwamba tutakapomaliza kuvitengeneza viwanja hivyo timu zetu zitavitumia kama kawaida.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atwambie ni mwezi gani viwanja vitakuwa tayari.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, sijui nimueleze vipi maana yake siwezi nikamwambia siku fulani kwa sababu haya ni mambo ya kiufundi na kitaalam. Kuna *factors* chungu nzima zinaweza zikatokezea hapo kati halafu nikakwambia siku fulani utakuja kunilaumu mbona ulinambia siku fulani na haikuwa. Kwa hivyo, mimi ninachoweza kukuhakikishieni kwamba baada ya miezi miwili basi haya masuala yote yatakuwa usiwe na wasi wasi Mhe. Mjumbe.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba baada ya miezi miwili mambo yatakuwa mazuri tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia kuhusu Chama cha Riadha. Nilitoa hoja zangu kusema kuwa bado tunakitupa na hususan hasa katika uchaguzi. Uchaguzi umefanyika tangu tarehe 29 Machi, 2003. Naomba Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wake Mhe. Waziri anambie uchaguzi mwengine utafanyika lini katika chama hichi ili kuweza kukiinua chama chetu cha riadha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba hichi chama kilikuwa bado hakina katiba. Kwa hivyo, watakapokuwa na katiba yao, maana ni jukumu la Baraza la Michezo kuangalia katiba za vyama vyao, hapo ndipo tutakapoanza kufanya mchakato

mzima lakini mpaka waunde katiba. Sasa tunasubiri waunde katiba yao ipitishwe tuhakikishe kwamba hapo tunamaliza kazi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Michezo limemudu kusimamia marekebisho ya katiba za vyama vifuatavyo ikiwemo na hiyo. Lakini hapa imenikanganya namuomba Mhe. Waziri anifafanulie. Unajua kila mtu na lugha yake, kama Mhe. Salmin Awadh Salmin anavyosema achowee labda na mimi ningesema achowee ili niweze kufahamu zaidi.

Kwa sababu huku upande mwengine ukurasa wa 68 kuna hiyo ndio riadha yenyewe anasema "*CECAFA* wametakiwa kukamilisha marekebisho ya katiba zao kabla ya kufanya uchaguzi." Lipi nilifuate kwa sababu huku tayari wameshasimamia marekebisho hayo lakini huku vimetakiwa vyama hivi vifanye marekebisho.

Lakini pamoja na hayo Mhe. Mwenyekiti, wakati tuliokuwanao sasa hivi hawa watu wa riadha ndio wanatuletea heshima Zanzibar na kwa kweli wapo katika hali ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kuchangia nilisema kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitoa pesa shilingi anazijua yeye Mhe. Waziri atanieleza. Fedha zile ziko wapi na mpaka leo wanariadha wale hawajapewa. Sasa yapo mambo mawili hapo katika kuchangia yangu naomba nipewe ufafanuzi.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, katika hiyo *paragraph* aliyosoma inasema kwamba itasimamia na halafu kuhakikisha kwamba ile katiba inakamilishwa. Kusimamia haina maana kwamba katiba imeshakamilishwa, kusimamia ni pamoja na *process* nzima ya kuendeleza kuwaharakisha kwamba jamani fanyeni haraka katiba imalizike.

Kwa hivyo, alivyosema Mhe. Waziri ni sawa sawa kwamba katika huo usimamizi wanasubiri katiba imalizike, baada ya kumalizika katiba ndio wao watashughulika. Kwa hivyo, yale aliyoyasema ni sawa sawa Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Spika: Wala haikuwa na haja ya kuchowea maana kuchowea ina watu wake maalum.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, sasa mapya haya kayaleta Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Narudia tena lugha yangu Baraza la Taifa la Michezo limemudu kusimamia marekebisho ya katiba ya vyama vifuatavyo na vyama vyengine vimeshafanya uchaguzi. Vimefanya vipi

uchaguzi. Sasa hapa mimi sijui nichowee vipi. Amejidhatiti kuwa amemudu kusimamia lakini huku amesema wameshakamilisha uchaguzi. Sasa hapa vipi, naona lugha inanipa utatanishi. Naomba Mhe. Abubakar Khamis Bakary anieleze pengine kisheria lita lina tafsiri ya Kiswahili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna mambo mawili tofauti. Kwanza ni suala la uchaguzi na pili kusimamia ile katiba . Unaweza ukafanya uchaguzi kwa utaratibu ambao ulikuwepo zamani, lakini kama mnataka kurekebisha wizara inaweza ikasema kwamba tengenezeni katiba ili mfanye *process* nyengine. Sasa uchaguzi unaweza ukaja kwa kutumia utaratibu mwengine uliokuwepo. Lakini ili kui-*perfect* zaidi lazima kuwe na katiba baadae ndio kuwe na uchaguzi au kuwe na utaratibu mwengine.

Kwa hivyo, bado nasema kwamba ilikuwa ni sawa sawa kusimamia urekebishaji huo na baadae kuhakikisha kwamba katiba inarekebishwa. Kwa hivyo, anachosema Mhe. Waziri ni sawa sawa ni kusema kwamba wanasubiri katiba sasa.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na katiba hapa ya Zanzibar, tulikuwa tunatekeleza kwa mujibu wa ile katiba ilivyokuwa, lakini baada ya marekebisho kutakuwa na utaratibu mwengine ndio zinavyokwenda *process* hizo. Kwa hivyo, bado nasema kwamba *statement* aliyosema Mhe. Waziri ni sawa sawa sasa tunasubiri huo utekelezaji au urekebishwaji wa katiba ili utaratibu mwengine uende kama ilivyopangwa.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria bado mimi sijamfahamu lakini nitamfahamu hivi. Kumbe waziri alikuwa na uwezo wa kuwaambia hichi chama cha riadha fanyeni kwanza uchaguzi halafu baadae mtarekebisha ile ndio lugha ninayoitaka mimi kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri. Unaweza ukafanya uchaguzi halafu baadae waziri akawaambia rekebisheni. Kwa sababu mwaka 2003 ndio ulifanyika uchaguzi kwa maana hiyo katiba ile inaweza ika-*play* pale kwa mujibu wa sheria yenu.

Lakini kwa ninavyojua mimi Mhe. Mwenyekiti, bado inaweza ile ikafanya kazi. Kwa hivyo, mimi namuomba Mhe. Waziri bado atamke lini utafanyika uchaguzi wa chama cha riadha kwa sababu kila leo wanakwenda kwenye kimataifa na uongozi ule uliokuwa zamani sio. Ndio maana nikasema kuwa walipewa pesa za zawadi na Mhe. Rais hazikuwafika walengwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, utafanywa uchaguzi baada ya kurekebisha katiba hamna matatizo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, *wallahi* waziri wangu nakupenda sana lakini kutokana na hichi chama ambacho kina umuhimu wake kwa hapa Zanzibar sasa hivi kila siku tunakusanya zile medali tena za dhahabu sio fedha haiwezekani kuwa na utawala ule wa nyuma kwa sababu umeshakuwa na kasoro. Wamepewa fedha milioni na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hilo hajalizungumza Mhe. Waziri hataki kunijibu. Aliyepewa ni kiongozi wa chama kile kazila fyuu. Ni nani huyo Mhe. Waziri na kwa nini zisifike, bado tunang'ang'ania uchaguzi utafanyika mpaka katika irekebishwe.

Mhe. Mwenyekiti, tuweke kanuni kando ya kusema kuwa uchaguzi ufanyike, sio kanuni kando ya Baraza samahani sikukusudia hilo, nimekusudia kanuni kando yeye katika sheria zake zile *by law* tunazompa aweke upande kwa kunusuru huo uongozi ambao sasa hivi umeshaonesha kuwa wana *element* ya rushwa. Kwa hivyo, aweke kanuni kando ili uchaguzi ufanyike haraka tupate chombo ambacho kinastahiki kinachokwenda na maadili.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, tutaweka kanuni kando na tutalitekeleza ombi lake Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimuamini huyu Mhe. Waziri wangu kabisa na ndio maana nikawa nasema kuwa Mhe. Rais Dk. Ali Mohammed Shein hakukosea. Kwa hivyo, naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia Mhe. Waziri nilimuuliza maswali mawili lakini kwa bahati mbaya naona hakunijibu sijui alisahau. Nilimuuliza kwa ajili ya kupata faida na kujua zaidi katika Baraza letu.

Nilimuuliza katika chama hichi cha michezo ya mpira *ZFA* na kule Bara kuna *TFF*. Je, kutokana na fedha zinazoingia kwa michezo ile inayoingia chama kile cha michezo cha Tanzania Bara *TFF* kutokana na misaada inayotoka *FIFA*, Zanzibar tunapata kiasi gani. Kwa hivyo, nilitaka atupe maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Mwakilishi alikuwa hayupo lakini nililijibu hilo swali katika maelezo yangu ya majumuisho. Nimesema kwamba tuna mahusiano na tunapata fedha na tunazitumia kwa mambo yetu. Vile vile tunakusanya katika masuala ya kurekodi mawimbi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri akitujibu ageuke huku kwa sababu sisi huku nyuma hatupati chochote, mimi sikumsikia chochote anachosema. Mhe. Mwenyekiti, naona Mhe. Waziri ameshataabanika na mimi sisikii basi namuachia tuendelee.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri hajachanganyikiwa bado tunaendelea na kazi vizuri. Hoja tatu kwenye fungu hili tumeshamaliza, sasa tunaweza tukamfuata kwa pembeni hivi ili akatusaidia maelezo kwa baadhi ya mambo ambayo hayajakamilika.

Kifungu 1201	Kamisheni ya Utamaduni na Michezo	564,600,000
Kifungu 1202	Baraza la Kiswahili	

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nitangaze maslahi yangu, mimi ni Mtumbatu kwa hivyo natetea Utumbatu wangu kwa kamusi ya Tumbatu. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri ametwambia kwamba tumpe milioni 90 kwa ajili ya mishahara ya milioni 15 sina wasi wasi nazo hizi nitampa, lakini milioni 75 kwa ajili ya uchapishaji wa makamusi ya Kitumbatu, Kipemba na Kimakunduchi. Sasa mimi ni Mtumbatu natetea maslahi yangu kwamba imekuwa ni kauli ya serikali miaka yote kwamba watazichapisha kamusi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nilipoangalia bajeti ya nyuma miaka mitatu kumbe hutuomba tuidhinishe pesa lakini hakuna fedha ya kuchapishia kamusi. Ni kusema kwamba huwa wanalidanganya Baraza kwamba watachapisha lakini fedha huwa haitengwi. Sasa mara hii Mhe. Waziri bahati nzuri ametuomba tumuidhinishie na fedha ametenga. Nimuombe anifahamishe ni nili hii kazi itaanza na labda amekusudia kuchapisha nakala ngapi kwa ajili ya Watumbatu, Wapemba na Wamakunduchi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, tumekusudia mara tu baada ya kuidhinishiwa fedha hizi basi tuanze kuchapisha nakala hizi. Kuhusu ni nakala ngapi, bado zijazijua ni nakala ngapi, itabidi niwaulize watendaji wangu ni nakala ngapi ambazo tutakusudia kuzifanya. Lakini tuna nia hiyo baada ya kwisha bajeti tusambaze nakala zote nchi nzima, ahsante.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu 1202	Baraza la Kiswahili	90,000,000
Kifungu 1203	Mchango wa *AECROTANAL*	20,000,000
Kifungu 1204		

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe Mwenyekiti, wakati nachangia kifungu hiki nilizungumza kwamba ruzuku ambayo inatoka katika kupewa Baraza la Michezo milioni 140, katika ruzuku hii kuna milioni 20 ambayo inakwenda katika mishahara inabaki milioni 120. Katika hizo milioni 120 milioni 20 inakuwa ya vilabu vile ambavyo vinawakilisha nchi, milioni 10 kila moja, zinabaki milioni 100 ambayo ndio inakwenda kwa vyama 30.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba vyama 30 kwa milioni 100 ni kidogo. Kwa mfano *ZFA* inapata ruzuku ya milioni 4 ambayo inaendesha mpira wa vyama vyote vya Zanzibar kwa milioni 4 na inaendesha timu ya taifa ya wakubwa na vijana.

Vile vile *ZFA* sio mwanachama wa *FIFA* haina mipango mingine ya kupata fedha, ndio nikasema hizi kidogo. Lakini Mhe. Waziri hakuweza kulizungumza suala hili. Pia vilabu hivyo ambavyo vinashiriki Mhe. Mwenyekiti, milioni 10, nikasema kwamba klabu inagharimika zaidi ya milioni 70 katika kushiriki mashindano hayo ya kimataifa ya klabu bingwa inapewa ruzuku ya milioni 10. kwa hivyo nikasema angalau kuwe na ongezeko la fungu kidogo. Nilimuomba Mhe. Waziri anipe maelezo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nakubali kwamba fungu halitoshi na hii ndio hali halisi na sio wizara yangu tu ni wizara nyingi tu, hakuna kinachotosha. Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Mjumbe na yeye ni shahidi kwamba yanapotokea masuala kama haya ya mashindano ya ligi, mara nyingi huwa tunatafuta wafadhili au wadhamini. Yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe ni shahidi na nimeshatafuta mdhamini na yeye mwenyewe alinishauri nifanye hivyo na kuna wengine nawatafuta na nimeshawapata *PSB* ambao watatudhamini katika masuala ya michezo.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba tushirikiane kwa hili kama alivyotushirikisha katika kumtafuta mdhamini wa *Grand Multer* . Kwa hivyo, na *PSB* na yeye ameshakubali, kwa hivyo, nahisi hakutokuwa na hali ya wasi wasi kuhusiana namashindano yetu au kushiriki katika ligi itakuwa ni kama kawaida, ahsante sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile waziri kakubali kwamba fungu ni kidogo, na yeye kasema kwamba atajitahidi kuwatafuta wadhamini kuweza kusaidia basi tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia katika hivi vyama vya michezo hasa katika chama cha riadha, nilisema kuwa kuna fedha za zawadi zilitoka. Lakini Mhe. Waziri hakunijibu kama yule

aliyechukua fedha zile kama kajulikana atachukuliwa hatua gani na lini atazileta.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kuona hiki chama chetu katika utaifa wake ukoje katika nchi za nje hiki chama cha riadha.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kuhusu nani aliyechukua fedha. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti mimi sina taarifa hiyo. Lakini nitalitafuta na nitamjibu.

Swali la pili kidogo sijalipata vizuri, unaweza kuuliza tena.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, hivi vyama vinakuwa vina utaifa katika nchi za nje za wenzetu huko. Sasa hiki chama cha riadha nacho ule usajili wake au utaifa wake ukoje katika Jumuiya za Kimataifa, tumejiunga sisi.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bado hatujajiunga, lakini tumo katika *process* za kufanya mchakato. Wacha wamalize katiba, tuangalie hatima mbele, tutafanya kila kitu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana naye lakini nimwambie suala moja tu, kuwa afuatilie huko kwa sababu kuna fedha ambazo ni dola 15,000 ambazo zinaletwa kwa ajili ya wanachama wa riadha kwa kimataifa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwa nia nzuri tu azifuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la mwisho namuomba tena Mhe. Waziri afanye uchaguzi haraka, fedha zinapotea ovyo.

Kifungu 1204	Baraza la Michezo la Taifa	140,000,000
Kifungu 1205	Baraza la Sanaa na Musiki	40,000,000
Kifungu 1206	Bodi ya Sensa na Sinema	37,000,000
	Jumla ya Fungu	

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa makusudi kwa sababu tunamaliza tunataka kupitisha fungu la jumla la wizara. Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki kuna vifungu viwili ameviombea Mhe. Waziri, lakini tumepekuwa sana kuanzia kwenye Kamisheni ya Utalii mpaka wizara nzima hii, mafungu hayo hatuyaoni. Kwa hivyo, nilikuwa naomba muongozo wako tu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 45 pale Shirika la Utalii ameliombea milioni 245,440,000. Halafu kuna Hoteli ya Bwawani kwenye ukurasa wa 48, ameliombea milioni 800,000,000, Lakini katika hivi vitabu hatukuona popote vifungu hivi. Nilikuwa naomba muongozo wako kwamba tukiidhinisha tumeidhinisha kwa sababu ya hotuba, au vifungu hivi vilivyokuwemo humu vitakuwa vinapata wapi mafungu yake.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi ni kwamba hili shirika hatujaliunga na Bwawani liko mbali mbali kwa kweli. Sasa sijui, au swali sijalifahamu labda au kuna marekebisho. Labda Waheshimiwa Wajumbe waangalie ile *additional*.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ilivyo ni kwamba Bwawani ni taasisi inayojitegemea na Shirika la Utalii ni taasisi inayojitegemea. Isipokuwa Bwawani inapata ruzuku kutoka serikalini kwa ajili ya kulipa mishahara ya watumishi wake. Pesa hizi mara nyingi zinakuwepo kwenye fungu la idara, utumishi na uendelezaji wa wizara. Kwa taasisi nyengine hutengewa fungu la moja kwa moja linaloonekana hapa kwenye buku hili kubwa la orodha ya vitabu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nadhani *format* aliyoitumia Mhe. Waziri kuieleza ni kama ile iliyotumika kwenye Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwamba Shirika la Bandari limeelezwa pale kuwa litakusanya kiasi fulani na linatarajiwa kutumia kiasi fulani, Lakini tulipokwenda kwenye kitabu kikubwa huwezi kukuta popote pale unapoweza kukuta kasma ya Shirika la Bandari ambayo sisi tunaiidhinisha. Nadhani format aliyoitumia inafanana na hiyo, kwa sababu shirika pesa zake wanazitegemea na kuziidhinisha na bodi kama hiyo bodi ipo na Bwawani nao ni kama taasisi inayojitegemea. Kwa hivyo, ruzuku yake sidhani kama ni ile ambayo anaweza akahakikisha mwenyewe, sidhani kama ni katika zile milioni 800,000,000 alizozieleza katika kitabu. Isipokuwa zile ni zile pesa ambazo wao wanazikusanya na kuweza kuzitumia.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, alivyoeleza Waziri, Mhe. Haji Omar ni sawa kwamba lile haliko pamoja na Shirika la Utalii linajitegemea na linapata ruzuku kutoka serikalini. Kwa hivyo, iko katika fungu moja kwa moja.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, hamna ruzuku ya Shirika la Utalii iliyooneshwa hapa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, Baraza hivi sasa kama kamati ndio inayopitisha vifungu vya matumizi. Ikiwa kuna matumizi yatakuwa nje ya

vifungu ambavyo tumeviidhinisha hapa, vitakuwa havijapata baraka ya chombo hiki, ndio nukta yangu, wala nisifahamike vyengine. Pengine hoja yake ni ndogo, niliwahi kukumbusha huko nyuma kuwa vifungu vya maendeleo ukaomba mwisho kwamba tuvijumuishe katika matumizi. Lakini hoja ya Mhe. Haji Omar Kheir Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haihusiki kwa sababu nikitizama fungu zima la Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni milioni 731,640,000, haijaingiza milioni 800,000,000. hizo milioni 800,000,000 ni za Bwawani peke yake zinaliwa zote, mbali ya Shirika la Utalii.

Kwa hivyo, nilikuwa nasema mimi nilikuwa natoa utaratibu, ndio maana nilitumia kifungu cha utaratibu kwamba nikuombe tu utakapokuwa unatuhoji na hizi basi kama zimesauliwa katika buku, utuhoji ili zipate idhini ya chombo hiki, basi hii ilikuwa ndio nukta yangu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, nakumbuka tuliwahi kupitisha, wizara nimeisahau, lakini ikawa haikutokeza kwenye buku hili la kasma, lakini imo katika botuba ile na idadi ya fedha ile ambayo imeombwa serikalini. Marekebisho tuliyofanya ya buku hili ni kwa kukubali zile pesa ambazo ziko kwenye kitabu kwamba nazo pia ni sehemu ya pesa ambazo zitatolewa na serikali na kwamba Baraza hili linaidhinisha hivyo. Sasa labda utuhakikishie jambo moja Mhe. Waziri je, fedha hii ya Shirika la Utalii, wao wana bodi yao ambayo inaidhinisha hayo au la, au kuna ruzuku ambayo inapitishwa na serikali moja kwa moja ili tuweze kuifanyia utafiti huo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, shirika halina bodi ya kuidhinisha hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: kwa hivyo, itabidi idhini itoke hapa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, ni kiasi gani? Mhe. Ismail Jussa hebu tusaidie ilikuwa ni kiasi gani hiyo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani ili ku-*simplify* kama sawa, uliombe Baraza lako tuidhinishe. Katika ukurasa wa 45 pale kwenye Shirika la Utalii pameombwa milioni 245,440,000 kwa kazi za kawaida na katika ukuraza wa 48 Baraza limeombwa milioni 800,000,000 kwa ajili ya Hoteli ya Bwawani. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tuzijumuishe halafu ndio tupitishe.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi mnavihitaji serikali ichangie, sio shirika lenyewe linatafuta. Haya. Kwa hivyo, tunakubaliana kwamba tukipitisha fungu marekebisho yake ni pamoja na kupitisha fedha hizi. Naona kama una wasi wasi mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mimi Mhe. Mwenyekiti, naomba niweke sawa maelezo ambayo mimi niliyasema. Bwawani inapata ruzuku kutoka serikalini, kinachotakiwa hapa kujulikana kwamba hizi milioni 800,000,000 ni katika ruzuku inayotoka serikalini au katika fedha zote ambazo zimekusanywa na hoteli ya Bwawani. Kama ni ruzuku ya Bwawani, basi nadhani tuliidhinishe, kama ni ruzuku na labda waziri mwenyewe anaweza akadhibitisha hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Hapa inaonekana ni matumizi kwa hoteli ya Bwawani.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nikubaliane na ile rai aliyoitowa Mhe. Ismail Jussa kwa sababu mbili. Kwa sababu kinachoonekana hapa, hii milioni 800,000,000 ni mapato ambayo yanakusanywa na Bwawani, lakini pia ndio matumizi, kwa sababu inakusanywa na Bwawani na sio shirika ni mapato halali ya serikali. Kwa hivyo, yanakuja serikalini, lakini Baraza hili lazima liidhinishe kuzirudisha tena Bwawani kwa ajili ya kutumiwa. Kwa hivyo, itumike kwa utaratibu huo, lakini hata Shirika la Utalii kwa kweli hizi pesa hazikupaswa kuwekwa hapa lakini kwa sababu hakuna bodi, nadhani hili Baraza ni haki yake kuidhinisha mpaka hapo itakapokuwa na bodi ndio itakuwa na mamlaka ya kuidhinisha. Kwa hivyo, nadhani yote mawili ni kufanya marekebisho tu yakaonekana na tukaidhinisha kama sehemu ya mapato au matumizi ya wizara hii ili waweze kutumia kwa uhalali.

Mhe. Mwenyekiti: Labda niulize swali moja, lakini jumla hii kuu iliyopo hapa haichanganyi fedha hizo. Itakuwa hazimo bila shaka. Sawa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani ili tusiendelee ku-*complicate* haya mambo. Kwanza nataka niweke sawa, kama nilivyosema vilivyoombewa hapa ni matumizi zote mbili ni matumizi. Kwa hivyo, mimi ufahamu wangu ulikuwa ni huo aliosema Mhe. Haji Omara kwamba ni wa ruzuku kutoka serikalini. Sasa inawezekana pia kuna mapato hatukutajiwa, lakini hilo sitaki kurudi tena huko.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema, mimi nadhani kama ulivyotuhoji siku ile ya Wizara ya Mawasiliano kwamba tupitishe fungu hili la jumla ambalo liko hapa katika kitabu na marekebisho yake. Sasa hapa tukitaka kufanya mahesabu tunaweza kuchelewa, kwa sababu kuna siku moja aliwahi kutujibu Mhe. Waziri wa Fedha kwamba hiki kitabu kitarekebishwa upya mwisho. Kwa hivyo,

tufanye na marekebisho yake kwa kufahamu kwamba inajumuisha na mafungu haya mawili, atakapokuja kufanya hicho kitabu kipya aje ajumuishe katika hicho kitabu ili matumizi yawe halali na baada kamati zako Mhe. Mwenyekiti, zitakapokuja kufuatilia matumizi zihakikishe kwamba na fedha hizi pia zimejumuishwa sio zile ambazo zitakuwa zimepitishwa nusu nusu. Naomba pendekezo hilo la jumla halafu tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri tukubaliane na hilo. Haya tuendelee.

	Jumla ya Fungu	**5,448,000,0000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0404	Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar	400,000,000
Kifungu 0501	Sauti ya Tanzania Zanzibar	2,440,000,000
Kifungu 1003	Baraza la Sanaa na Muziki	120,000,000
	Jumla ya Fungu	**2,960,000,000**

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza: Mhe. Mwenyekiti, naomba turudie kanuni ya ukurasa wa 48 ya 65 lakini sehemu ya 6 inahusiana na udhibiti wa amani, utulivu, heshima na uwajibikaji katika Baraza lako tukufu la Wawakilishi.
Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunamalizia lakini bado tuko katika sehemu hii ya matumizi, mmoja wa waheshimiwa wajumbe wako wa Baraza hili alitumia lugha ambayo hairuhusiki kutumika ndani ya Baraza hili kwa kumtaja mmoja wa mawaziri wetu kwamba amechanganyikiwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba mjumbe huyo aidha athibitishe kuchanganyikiwa kwa waziri wetu au aondoshe lugha yake na kumuomba radhi.

Mhe. Mwenyekiti: Hilo neno nililisikia, labda Mhe. Subeit sijui. Hilo neno nililisikia na nikakanusha kwamba waziri wetu hajachanganyikiwa. Sasa nadhani, Mhe. Subeit sijui ulitaka kusema nini.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kauli ya kusema kuwa kachanganyikiwa sijasema. Nimesema mimi sisikii akisema Mhe. Waziri, na madamu Mhe. Waziri keshataabanika basi tuendelee. Keshataabanika basi tuendelee. Kutaabanika ni kuchoka.

Waheshimiwa Wajumbe: Ahaaa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Sasa kama nimetumia kauli mbaya yakusema kutaabanika, lakini mimi ndio kauli niliyosema. Kauli niliyotamka mimi ni kuwa Mhe. Waziri kweshataabanika. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kumbe hatukusikia. Kimsingi ni kwamba amehisi amechoka, kutaabanika ni kuchoka.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza: Mhe. Mwenyekiti, nimeamini kwamba Baraza la Mapinduzi lina mawaziri waliotimamu na wenye nguvu za kutosha za kukabiliana na shughuli zao za kila siku. Kwa hivyo, hata hilo alilosema athibitishe kwamba waziri alichoka kwa sababu waziri alikuwa akijibu hoja zake, na ni yeye ambaye alikuwa ana tatizo la kusikia, labda tumshauri vile vile na yeye apime afya yake. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima yako kubwa, kwanza mimi siwezi kuomba radhi kwa kauli ninayoisema, kwa sababu sijasema kauli mbaya wala kauli chafu, kumwambia mwenzako umechoka sio kauli chafu. Mimi bado narudia kusema kwamba nilisema aah! Kwa sababu Mhe. Waziri keshataabanika, ni kumuonea huruma na kumuonea imani kwa maana tuendelee, sio kauli mbaya. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mimi nafikiri sote ni mashahidi kazi iliyofanyika hapa ni kubwa mno. Hatupaswi kusema kwamba tumechoka kwa sababu ni wajibu, lakini kimsingi kazi ni kubwa mno, nafikiri tukubaliane kwamba kazi ilikuwa ni kubwa, kama alivyoona Mhe Rashid pale. Mhe. Rashid Seif Suleiman kwamba yeye basi kwa imani na mimi nikasema tunakushukuru kwa imani yako Mhe. Waziri.

Nadhani tufikie pahala tumalize hili jambo, wala lisilete hoja iliyo kubwa kwa sababu kimsingi yaliyotokea hapa sote tumeona ni kazi kubwa mno, kiasi cha kuwa mtu afike pahala akapumzike. Nadhani Mhe. Waziri Fatma Ferej ili tukubaliane kwamba hali halisi ya mazingira yetu na shughuli hii ukubwa wake tumeiona, basi tufikie pahala tu kwamba hili liwe limekwisha.

he. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza: Mhe. Mwenyekiti, nimefahamu na nafikiri tuna matatizo ya viswahili vinavyopishana humu ndani, vile vile naamini kwamba halitotokea hilo ndani ya Baraza lako. Wasi wasi wangu tu ilikuwa kwamba isiwe wajumbe wamechupa mipaka, lakini nimefurahi kuthibitishiwa kwamba hakukuwa na hilo. Tuendelee.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri asikilize vikao vya Bunge la Uingereza, kwa sababu tumo ndani ya CPA sisi. Kwa hivyo, ajizoweshe kusikiliza Bunge la Uingereza ili na wao wajuwe kuwa

tunaweza tukawaambia baadhi ya maneno yaliyokuwa hayana kuvunjiana heshima, lakini yana mantiki ya kumuelekeza na kumuambia kwamba achangamke. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri masuala ya Bunge la Uingereza tuwaachie wenyewe. Sisi tuendelee na utaratibu wetu ambao una heshima kubwa na jana tu Mhe. Ismail Jussa Ladhu, alinileta salamu kwamba kuna watu wanaridhika sana kwa namna tunavyokwenda. Kwa hivyo, tena nipokee salamu hizo za pongezi ambazo zilipitia kwa Mhe. Jussa, kwamba kumbe wenzetu wanatuona huko nje tunakwenda vizuri mno. tujipongeze. *(Makofi).*

(Baraza lilirudia)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri kipindi kile alikuwa hakunywa maji bwana, sasa amepata pumzi amekunywa angalau na maji. Nakupongeza sana Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu pamoja na mabadiliko yake, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na makadirio hayo pamoja na mabadiliko yake wanyanyuwe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwe na kuafikiwa)

Mhe. Mshimba hebu kaa tuendelee, utaratibu upi tena, iliyobakia ni kuahirisha kikao, ndio utaratibu uliobaki. Waheshimiwa Wajumbe, nichukuwe nafasi hii kukushukuruni sana na tumekuwa makini sana katika kupitisha bajeti na hilo ni muhimu. Tunawathibitishia wananchi kwamba fedha za walipa kodi zitakuwa zinazingatiwa vizuri sana nah ii ni changamoto kwa Waheshimiwa Mawaziri wote tuwe makini sana katika kufuatilia hata mafungu haya ya matumizi.

Ni jambo muhimu sana tunapokuja kwenye kamati ya matumizi Mhe. Waziri awe na maelezo ya kutosha kuhusu matumizi ya mafungu mbali mbali, ili pale yanapohitajika kuulizwa na Waheshimiwa Wajumbe basi majibu muafaka yapatikane juu ya mafungu yale mbali mbali.

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa mashirikiano makubwa mnayonipa kuendesha kikao hiki. Sasa naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 9:00 jioni Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha – Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka 2011/2012

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na kabla ya kuwasilisha hotuba ya bajeti hii, naomba kueleza mambo mawili.

Kwanza kwa kujali muda wako baadhi ya aya nitazisoma kwa muhtasari, lakini urefu uliomo ndani ya kitabu ndio ufafanuzi wake. Pili kwa kuwapa Waheshimiwa Wajumbe uelewa zaidi wa hali ilivyo kwenye wizara hii, basi nimejaribu kutanguliza maelezo ya taaswira kabisa ya maelezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yangu.

UTANGULIZI

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tukiwa katika hali ya afya na kutujaalia amani na utulivu katika nchi yetu. Kwa niaba ya wafanyakazi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kwake kuiongoza Zanzibar akiwa Rais wa Awamu ya Saba chini ya Serikali yenye mfumo wa Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Pia napenda kuwapongeza Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwa hakika kikosi hichi cha viongozi hawa watatu wa juu wa nchi yetu kinaleta matumaini makubwa kwa wananchi wote na timu inayoheshimika sana hata nje ya nchi yetu.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa kuwa miongoni mwa Wenyeviti wawili wa Baraza hili tukufu ukiongozwa na Mhe.

Spika wa Baraza la Wawakilishi na Mhe. Naibu Spika, mkisaidiwa kwa pamoja na Katibu wa Baraza na maafisa wa Baraza wanaokusaidia katika kazi zako.

Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza pamoja na Wajumbe wote kwa michango yao na ushirikiano mzuri wanaotoa kwa Wizara yangu. Kamati hizi zimekuwa ni chachu muhimu sana katika kushajiisha wafanyakazi wa wizara yangu pamoja na wafugaji, wavuvi, wakulima wa mwani na wadau wengine wa sekta hizi katika kuendelea kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, niruhusu kutoa shukrani za pekee na kuipongeza Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, kwa ushauri na maelekezo yao ya msingi na busara zao katika kuielekeza wizara yangu. Uzoefu wa siku nyingi wa Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Asha Bakar Makame na umahiri wa wajumbe wa kamati hii unanisaidia sana mimi na watendaji wa wizara yangu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kukipongeza Chama changu cha Wananchi CUF kwa kunipa imani na kupendekeza jina langu katika nafasi ya kuwa msimamizi miongoni mwa wizara ndani ya Serikali hii yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa. *(Makofi)*

Aidha namshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kukubaliana na mapendekezo hayo. Kwa hakika mimi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando kupata fursa hii ya kuwatumikia Wazanzibari katika serikali yenye mfumo huu ni heshima kubwa na kwa Wazanzibari nina deni la utumishi kwao.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyojua, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imeanzisha Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi, kwa lengo la kuendeleza sekta za mifugo na uvuvi kwa ufanisi zaidi, ili ziweze kuchangia katika uhakika wa chakula kwa mazao ya mifugo na uvuvi, kuongeza kipato cha wananchi, kupunguza umasikini na hatimaye kuongeza pato la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Mapinduzi katika Sekta ya Uvuvi na Mifugo kama yalivyoelekezwa katika hotuba muhimu ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika uzinduzi wa Baraza la Wawakilishi hapo Novemba 2010, ambayo ilizingatia Dira, Ilani, Mikakati ya kupunguza Umasikini, Sera na ahadi mbali mbali ni nyenzo zitazotumika katika kufanikisha malengo yetu.

HALI YA SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI NCHINI

Sekta ya Mifugo:

Mafanikio katika Sekta ya Mifugo:

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo imeweza kupata mafanikio kadhaa kati yao ni kama yafuatayo: -

(a) Kupatikana kwa mtambo wa kuzalisha *"liquid nitrogen"*. Hii imesababisha kiwango cha upandishaji ng'ombe kwa sindano kuongezeka kutoka ng'ombe 500 hadi kufikia ng'ombe 1,275 kwa mwaka.

(b) Kuanzishwa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa maziwa ambavyo vinazalisha samli, siagi, mtindi na maziwa ya kunywa.

(c) Muamko wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa umeongezeka kwa wananchi wengi na kupelekea ongezeko la mahitaji ya mbuzi hao.

(d) Muamko wa wafugaji kuwapatia wanyama wao huduma bora za kinga na tiba umeongezeka. Hivyo kupunguza hasara na vifo vya mifugo kwa wafugaji.

(e) Kuongezeka kwa muamko wa wafugaji juu ya matunzo bora ya wanyama kwa kujali haki zao za kuwapatia mahitaji muhimu wanayostahili.

Hali ya Sekta ya Mifugo:

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo ina umuhimu mkubwa kiuchumi hapa Zanzibar. Mchango wa sekta hiyo katika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 4.5 hadi kufikia asilimia 4.7 sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Hii inatokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya mifugo kulikotokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la ndani.

Kwa hivi sasa jumla ya kaya 45,684 zinajishughulisha na ufugaji wa ng'ombe wakati kaya 78,428 zinajishughulisha na ufugaji wa kuku. Kutokana na kipaumbele iliyopewa wizara yangu, na kwa mikakati tuliyoiweka, nina matumaini makubwa kuwa wizara yangu itainua hali za maisha ya wananchi pamoja na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imeandaa mikakati maalum ya kuinua zaidi sekta hii hapa nchini, ikiwemo kuzidisha ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji, sambamba na huduma bora za utabibu wa mifugo zitakazopelekea kuongeza idadi ya mifugo na ubora wa mazao ya mifugo. Wizara yangu inafanya juhudi za makusudi katika kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa mazao ya mifugo ikiwemo kuku na maziwa.

Hivi sasa juhudi zinafanywa kushajiisha wawekezaji wa kati na wakubwa wa ndani na wa nje kuwekeza katika sekta ya mifugo na kuweka utaratibu wa ufugaji wa makubaliano *"contract farming"* kwa madhumuni ya kulinda soko la ndani na kuisaidia serikali katika kuwaendeleza wafugaji wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inatilia mkazo sana uanzishaji wa tafiti ndogo ndogo zinazowashirikisha wafugaji wenyewe, ili kupata mbinu bora za uzalishaji na mifugo bora yenye sifa za uzalishaji zaidi na kuhimili maradhi yaliopo nchini.

Changamoto katika Sekta ya Mifugo:

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Mifugo inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo uhaba wa nyenzo za kutolea elimu kwa wafugaji ikiwemo vyombo vya usafiri na uchache wa wataalamu ambao wengi wao wana elimu ndogo.

Aidha, taaluma ndogo kwa wafugaji, uwezo mdogo wa kununulia teknolojia na pembejeo kwa wafugaji na wasindikaji, maradhi ya mifugo, nasaba duni za mifugo yetu kiuzalishaji, uhaba wa malisho, wanajamii kukhalifu sheria za mifugo na utesaji wa wanyama ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta hii. Wizara yangu tayari imeandaa mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo.

Mtazamo wa Baadae katika Sekta ya Mifugo:

Mhe. Mwenyekiti, katika jitihada za kuimarisha Sekta ya Mifugo nchini, wizara yangu imejizatiti kuongeza ufanisi wa watendaji kwa kuwawekea mazingira mazuri ya kazi ikiwemo usafiri, vifaa vya kutendea kazi, kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi waliopo pamoja na kuwashajiisha vijana kuendelea na masomo yao katika fani za mifugo.

Aidha, wizara yangu inalenga kuboresha mfumo wa elimu ya ushauri kwa wafugaji ikiwemo kuendeleza skuli za wafugaji, kuwaunganisha wafugaji na taasisi za fedha, na kuanzisha vituo vya kujiendeleza kitaaluma kwa wafugaji hao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itaendelea kuhamasisha jamii juu ya utumiaji wa gesi inayotokana na samadi, ambao unachangia kwa kiasi kikubwa kuhifadhi mazingira kwa kupunguza matumizi makubwa ya kuni na mkaa katika visiwa vyetu. Hali hii itapunguza sana athari ya mabadiliko ya tabia nchi kunakotokana na ukataji mkubwa wa miti.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutilia mkazo masuala ya utafiti wizara yangu imejipanga kuanzisha programu maalumu ya kuimarisha miundombinu ya mifugo pamoja na kuhimiza tafiti mbali mbali za mifugo, kwa lengo la kubadilisha mfumo wa ufugaji uliopo hivi sasa, ili uwe wa kibiashara zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inakusudia kuimarisha mahusiano zaidi kati ya wizara, wafugaji wadogo wadogo na wa kati, wafanyabiashara wa mazao ya mifugo, wawekezaji wa ndani na nje, Jumuiya za kikanda na Kimataifa zinazohusiana na sekta ya mifugo, pamoja na wadau wengine kwa lengo la kuongeza uzalishaji na tija. Aidha, Wizara yangu itashirikiana na *ZAASO*, *ZALWEDA*, *WSPA* na Jumuiya nyengine za kitaifa na kimataifa zinazotetea haki na ustawi wa wanyama.

Sekta ya Uvuvi:

Mafanikio katika Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi imepata mafanikio makubwa katika kipindi hichi. Miongoni mwa mafanikio ya Sekta ya Uvuvi ni kama yafuatayo: -

(a) Kuongezeka kwa wavuvi na kiwango cha samaki wanaovuliwa;

(b) Kuongezeka ukulima wa mwani, ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini;

(c) Kuongezeka kwa mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la Taifa kutoka asilimia 5.2 mwaka 2009 hadi asilimia 6.1 mwaka 2010;

(d) Jumla ya wanajamii 200 kati ya hao, 127 wanawake na 73 wanaume wamepatiwa mafunzo mbali mbali yakiwemo ya ujasiriamali, uongozi, usimamizi na uendeshaji wa miradi. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wanajamii wote wa ukanda wa pwani hasa wanaotekeleza miradi yao;

(e) Kuongezeka kwa kiwango cha zana za kuvulia kwa wanajamii, ambapo jumla ya mashua 17 za uvuvi na nyavu za kuvulia 17 zilikabidhiwa kwa vikundi 22 kutoka vijiji 31 vya Unguja. Kwa upande wa Pemba jumla ya vikundi 21 vinavyojishughulisha na shughuli za uvuvi, upandaji miti na ufugaji nyuki vimepatiwa vifaa. Katika msaada huo jumla ya mashua 18 na mashine 18 zilitolewa;

Aidha, ujenzi wa masoko ya kuuzia samaki katika maeneo mbali mbali hapa nchini kama vile Nungwi, Matemwe na Pwani Mchangani kwa upande wa Unguja na Ole, Mvumoni, Wesha, na Kilindi kwa upande wa Pemba ulitekelezwa na ujenzi wa soko la Tumbe unaendelea;

(f) Mafanikio makubwa yamepatikana kwa kuwepo maeneo ya hifadhi yanayopelekea matumizi mazuri na endelevu ya rasilimali za baharini pamoja na upatikanaji wa mapato yanayotokana na rasilimali hizo ambapo jumla ya shilingi 167,396,150 zilipatikana;

(g) Kuongezeka kwa shughuli za ufugaji wa samaki, ambapo jumla ya vikundi 35 kwa Unguja na 40 kwa Pemba vya ufugaji wa samaki, kaa, chaza na lulu vimeanzishwa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imepata mshauri muelekezi kutoka *FAO* kutupatia ushauri juu ya namna bora ya ufugaji na ukulima wa mazao ya baharini na hivi sasa tunasubiri ripoti yake.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuliarifu Baraza lako Tukufu kuwa hivi sasa makampuni yote ya ununuzi wa mwani nchini yamekubali kuongeza bei ya mwani mwembamba kutoka shilingi 250 kwa kilo na kununua kwa shilingi 400 kwa kilo. Hivi sasa wakulima wa mwani nchini wameshaanza kufaidika na bei hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu mafanikio kadhaa yamepatikana kama yanavyojionyesha hapo chini:-

(a) Kupatikana kwa jengo la ofisi ya Mamlaka ambalo linategemewa kumalizika hivi karibuni.

(b) Kufanya doria za angani na majini kwa kushirikiana na KMKM, Polisi *Marine*, Jeshi la Majini na Anga. Hii

imesaidia kupunguza uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira na

(c) Kusimamia utoaji wa leseni kwa pamoja za uvuvi wa Bahari Kuu na kusimamia mgao wake.

Hali ya Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Mwenyekiti, Hali ya Sekta ya Uvuvi kwa sasa iko kama ifuatavyo: -

(a) Kiwango cha uvuvi wa samaki kimeongezeka kutoka tani 25,396 zenye thamani ya shilingi 47,714,069,596 mwaka 2009 hadi kufikia tani 25,693,080 zenye thamani ya shilingi 61,784,309,912 kwa mwaka 2010 zilizouzwa na wavuvi.

(b) Ukulima wa mwani umeongezeka kutoka tani 10,248 zenye thamani ya shilingi 1,665,542,469 katika mwaka 2009 hadi kufikia tani 12,500 zenye thamani ya shilingi 3,125,000,000 kwa mwaka 2010 zilizouzwa na wakulima wa mwani.

(c) Mchango wa sekta katika pato la taifa umeongezeka kutoka asilimia 5.2 kwa mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 6.1 kwa mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 0.9

Changamoto katika Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Mwenyekiti, Sekta ya Uvuvi inakabiliwa na changamoto mbali mbali zikiwemo: -

(a) Kuongezeka kwa wavuvi kutoka ndani na nje ya Zanzibar katika maeneo ya hifadhi, kuwepo kwa wavuvi wanaojihusisha na uvuvi haramu na kukithiri ukataji wa mikoko katika fukwe unaopelekea kupunguza mazalia ya samaki.

(b) Mabadiliko ya hali ya hewa (kuongezeka kwa joto baharini) kunakosababisha kupauka kwa matumbawe *"coral bleaching"* inayosababisha mtawanyiko wa samaki baharini.

(c) Kuwepo migogoro baina ya wavuvi, wawekezaji na wakulima wa mwani, kunaathiri sana shughuli za uvuvi.

(d) Uwezo mdogo wa jamii kuwekeza katika ufugaji wa mazao ya baharini, ukosefu wa utaalamu na uelewa katika fani ya ufugaji wa mazao ya baharini na uhaba wa wafanyakazi wataalamu wa fani ya mazao ya baharini.

(e) Kupungua kwa mapato ya Bahari Kuu kunakotokana na tishio la uharamia baharini.

(f) Kutokuwa na wavuvi wazawa wanaovua kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu.

(g) Kutokuwa na miundo mbinu ya uvuvi wa bahari kuu inayosababisha meli zinazopewa leseni za uvuvi wa bahari kuu kutolazimika kutia nanga kwenye gati zetu, jambo hili hukosesha nchi yetu mapato mengi.

Mtazamo wa Baadae katika Sekta ya Uvuvi:

Mhe. Mwenyekiti, mtazamo wa baadae katika sekta ya uvuvi ni kuendeleza uvuvi kwa kushajiisha uanzishaji wa kampuni za wazawa za uvuvi na ukulima wa mazao ya baharini kwa vikundi. Kutafuta njia na mbinu zitakazowezesha wavuvi wetu kuvua katika ukanda wa uchumi pamoja na kuhamasisha wawekezaji kutoka nje kwa ajili ya uvuvi wa viwanda. Aidha kufanya tafiti ili kutambua maeneo bora ya uvuvi *(potential fishing grounds).*

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inakusudia kuimarisha mahusiano zaidi kati ya wizara, wavuvi, wakulima wa mwani, wafanyabiashara wa mazao ya baharini, Taasisi ya Sayansi za Bahari, Jumuiya za kikanda na Kimataifa zinazohusiana na bahari, pamoja na wadau wengine ili kuongeza uzalishaji na tija.

Aidha, ufugaji wa samaki utaimarishwa badala ya kutegemea samaki wanaovuliwa moja kwa moja kutoka baharini. Miundombinu na taaluma ya ufugaji wa mazao mengine ya baharini itaimarishwa kwa lengo la kuongeza tija kwa wafugaji wa mazao hayo na kwa kuangalia ubora wa viwango vya mazao ya baharini yanayozalishwa.

TAARIFA YA MALENGO NA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2010/2011 NA MALENGO YA MWAKA 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia mabadiliko ya muundo wa Wizara, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeundwa na Idara sita ambazo ni hivi zifuatazo:-

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti,
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
- Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo,
- Idara ya Uzalishaji Mifugo,
- Idara ya Maendeleo ya Uvuvi,
- Idara ya Mazao ya Baharini na Ofisi Kuu ya Wizara Pemba.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Majukumu ya Idara:
Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina wajibu wa kuratibu, kubuni na kuandaa mipango ya maendeleo ya sekta ya mifugo na uvuvi, kusimamia, kutayarisha na kufanya mapitio ya Sera, Mikakati, Programu na Miradi ya Maendeleo kwa sekta hizi na kuratibu kazi za utafiti. Vile vile idara hii ni kiungo baina ya taasisi za ndani, za kikanda na za kimataifa.

Malengo ya Mwaka 2010/2011:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara ya Sera na Mipango, chini ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira kwa Sekta ya Mifugo na Uvuvi ilikuwa na malengo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha taratibu za uwasilishaji sera na sheria mbali mbali za Wizara na kusimamia utekelezaji wake.

(b) Kuratibu mashirikiano na taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa na utayarishaji wa miradi.

(c) Kufanya mapitio ya mpango mkakati wa sekta ya mifugo na uvuvi *(Strategic Plan).*

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 idara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Sera mpya ya mifugo imeshatayarishwa na kuwasilishwa katika ngazi za juu za uongozi wa wizara.

(b) Idara imeandaa mapendekezo ya miradi ya miundo mbinu ya uvuvi na mifugo, uchambuzi yakinifu wa ufugaji wa samaki, viwanda vya ukaushaji wa dagaa pamoja na

programu ya kuwaendeleza wavuvi Zanzibar na kuziwasilisha serikalini na kwa washirika wa maendeleo.

(c) Rasimu ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi imeshatayarishwa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

(d) Idara imefanya mapitio ya Sekta *(sector review)* ya Mifugo na Uvuvi.

(e) Uchambuzi yakinifu wa ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini *(feasibility study on marine aquaculture)* umeshafanywa kwa kushirikiana na Idara ya Mazao ya Baharini pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO).*

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012 idara inalenga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kukamilisha taratibu za uwasilishaji wa Sera ya Mifugo na kuzipitia sheria ndogo ndogo za mifugo na uvuvi pamoja na kusimamia utekelezaji wake.

(b) Kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, kutayarisha Mpango Mkuu wa Kuendeleza Uvuvi *(Fisheries Master Plan).*

(c) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu na mapato yatokanayo na sekta za mifugo na uvuvi.

(d) Kuanzisha Kitengo cha Habari, pamoja na kutoa nakala 1,000 za "Jarida la Mvuvi na Mfugaji" na kulisambaza kwa wadau.

(e) Kuratibu mashirikiano na taasisi mbali mbali za Kitaifa na Kimataifa.

(f) Kubuni na kutayarisha miradi mbali mbali ya maendeleo.

(g) Kuratibu kazi za utafiti za Sekta ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 idara itatekeleza mradi mmoja wa Kuimarisha Miundo Mbinu ya Mifugo, ambao utaendeshwa kwa fedha za Serikali (Kiambatisho na. 1)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 327,462,819/= kwa kazi za kawaida na shilingi 243,000,000/= kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kazi za kawaida shilingi 106,009,000/= ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI:

Majukumu ya Idara:

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ndio kiungo kikuu cha wizara hasa katika kusimamia na kuratibu taasisi za wizara, kusimamia uendeshaji wa kazi za kila siku za wizara ikiwa ni pamoja na uwekaji wa kumbukumbu za wafanyakazi wa wizara, utunzaji wa mali za serikali, kuhakikisha haki na wajibu wa wafanyakazi pamoja na kufanya jitihada za kuwaendeleza kitaaluma wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Idara inasimamia uajiri na maslahi ya wafanyakazi.
Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kwa hivi sasa ina jumla ya wafanyakazi 731, kati ya hao, wenye elimu ya kiwango cha shahada ya kwanza kwenda juu ni 38 tu (Kiambatisho na. 6). Hii inaonesha dhahiri idadi ndogo ya wataalamu tuliyonayo ikilinganishwa na wingi wa wafugaji, wavuvi na wakulima wa mwani wenye matarajio makubwa ya kupata huduma kutoka kwetu. Wizara kwa sasa inajipanga kuwaendeleza wafanyakazi kielimu pamoja na kuajiri wataalamu zaidi.

Malengo ya Mwaka 2010/2011:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambayo ilikuwa ni sehemu ya Idara ya Sera na Mipango ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira ilikuwa na lengo la kuendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji ya taasisi zilizo chini ya Wizara.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Jumla ya wafanyakazi 42 wanaendelea na masomo katika vyuo vya nje na ndani. Kati ya hao 11 ni wa kiwango cha cheti, nane stashahada, 21 shahada ya kwanza na wawili ni shahada ya pili. Miongoni mwao 15 ni wanawake na 27 ni wanaume (Kiambatisho na. 7).

(b) Kusimamia ukarabati wa jengo la wizara liliopo Maruhubi iliyokuwa Idara ya Maendeleo ya Mifugo. Hivi sasa wizara imehamia katika ofisi zake hizo kwa muda.

(c) Jumla ya wafanyakazi 95 wa wizara walijitokeza kwa hiari kupima afya zao, pamoja na kupatiwa ushauri nasaha.

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012 idara inalenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wafanyakazi wa wizara.

(b) Kuwaendeleza wafanyakazi kielimu katika maeneo yao ya kazi na kutafuta fursa za masomo kwa wafanyakazi hao kutoka taasisi mbali mbali zinazotoa fursa za masomo ndani na nje ya nchi.

(c) Kuendelea kusimamia haki na maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha wafanyakazi hao wanatekeleza wajibu wao kwa kufuata Sheria za Utumishi Serikalini.

(d) Kutunza mali za serikali zinazomilikiwa na wizara.

(e) Kufuatilia upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo yote ya serikali yanayomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

(f) Idara itashirikiana na taasisi nyengine katika kuendelea kuwashajiisha wadau wake kubadili tabia, ili wajikinge na maambukizo ya maradhi ya UKIMWI, madawa ya kulevya na kutowanyanyapaa wale waliopata maambukizo. Hii itasaidia kukuza sekta ya uvuvi na ufugaji.

(g) Kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi, ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi zaidi kwa wananchi ikiwemo kuwapatia vitendea kazi.

(h) Ujenzi wa josho la kwanza katika Wilaya ya Mkoani kisiwani Pemba katika Shehia ya Mjimbini.

(i) Kuendelea na utaratibu wa kuzifanyia ukarabati nyumba za wizara zilizoko Mkoroshoni kisiwani Pemba na Mkwajuni kisiwani Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 306,740,870/= kutoka serikalini, ili kutekeleza kazi zake za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 85,151,000/= zimetengwa kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA UZALISHAJI MIFUGO:

Majukumu ya Idara:

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uzalishaji Mifugo ina jukumu la kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu za maendeleo ya mifugo. Aidha, idara hii hutoa taaluma ya ufugaji bora kwa lengo la kuongeza uzalishaji na ubora wa mifugo na mazao yake, ili kuleta tija kwa wafugaji na wananchi kwa ujumla. Pia idara ina jukumu la kuimarisha uzalishaji wa mifugo ya asili kwa kubadilisha vinasaba (*cross breeding*).

Malengo ya Mwaka 2010/2011:
Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 idara ililenga kutekeleza yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma ya ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji ili kuongeza uzalishaji.

(b) Kushajiisha wananchi kutumia samadi inayotokana na mifugo kwa kuzalisha nishati mbadala kwa matumizi mbali mbali.

(c) Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kupandisha ng'ombe kwa sindano kwa matumizi ya mbegu bora za ng'ombe na mbuzi wa maziwa. *(Makofi)*

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011:

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa malengo haya hatua mbali mbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na yafuatayo:-

(a) Katika kuhakikisha wafugaji wanapatiwa huduma bora za ushauri jumla ya wafugaji 14,288 Unguja na Pemba wametembelewa na kupatiwa ushauri wa kitaalamu. Makundi yaliyopatiwa ushauri ni pamoja na wafugaji wa kuku, wazalishaji wa vifaranga, wafugaji wa ng'ombe wa maziwa, wafugaji wa mbuzi na jumuiya mbali mbali zinazojishughulisha na ufugaji. Aidha, wananchi wanaotarajia kuwekeza katika ufugaji wa ng'ombe, mbuzi na kuku walitembelewa na kupatiwa ushauri wa awali.

(b) Kwa kushirikiana na programu ya *ASSP/ASDP-L*, idara iliendelea kutoa taaluma kupitia mashamba darasa 172 Unguja na Pemba. Aidha, kwa kushirikiana na programu inayoratibiwa na (*ILO/JP5/CoopAfrica*), Idara imetoa mafunzo kwa ushirika wa ufugaji ng'ombe wa maziwa "JUWAPO" uliopo Fuoni, "Ungalipo" uliopo Chaani na ushirika wa kuku "Kupata Si Nguvu" uliopo Birikau-Pemba, pamoja na baadhi ya wafugaji wengine katika maeneo ya karibu.

(c) Idara ya Uzalishaji wa Mifugo, kwa kushirikiana na jumuiya ya kiraia ya kizalendo "*ZALWEDA*" na Jumuiya ya kiraia ya kigeni "*DANTAN*" kwa pamoja ziliendesha ushajiishaji wa matumizi ya nishati mbadala inayotokana na samadi ya mifugo kwa matumizi ya nyumbani.

Zoezi hili limeanza kisiwani Pemba ambapo semina iliyojumuisha wafugaji 50 waliotegemewa kuwa wadau wa mpango huu iliendeshwa. Kwa upande wa Pemba mtambo mmoja (1) umekwishafungwa katika eneo la Shumba Viamboni na miwili (2) imefungwa Unguja katika eneo la Machui.

(d) Jumla ya ng'ombe 1,274 walipandishwa kwa sindano. Kuimarika kwa huduma hii inatokana na kufungwa kwa mtambo wa kuzalishia "*liquid nitrogen*" katika kituo cha Maruhubi.

(e) Utaratibu wa ununuzi wa madume ya ng'ombe bora wa maziwa wawili wa aina ya *(Jersey)* na ukarabati wa sehemu ya maabara ya kituo cha kuzalisha mbegu bora umekamilika.

Malengo ya Mwaka 2011/2012:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, idara itatekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kushajiisha vijana kujiajiri katika kazi za ufugaji wa kibiashara.

(b) Kuendelea kuimarisha kituo cha upandishaji ng'ombe kwa sindano Maruhubi kwa kukarabati jengo la ofisi na kulizungushia uzio eneo hilo la kituo, na kutayarisha ardhi kwa kupanda majani kwa ajili ya malisho ya ng'ombe wa mbegu.

(c) Kuendeleza kazi za upandishaji ng'ombe kwa sindano ambapo ng'ombe 6,000 wanatarajiwa kupandishwa.

(d) Kufundisha taaluma ya upandishaji wa mbuzi kwa sindano, kwa wapandishaji *(CAHW's)* Unguja na Pemba na kuendeleza utafiti wa mbuzi bora. Katika hili la utafiti, naomba kutoa taarifa kwamba mwekezaji Sheikh Ali Yousouf amekubaliana na Idara ya Uzalishaji Mifugo, kufanya utafiti wa pamoja juu ya kabila ya mbuzi bora kutoka Cyprus ambao wanauwezo wa kuzaa ndama watatu kwa mpigo na kutoa maziwa lita 6 hadi 8 kwa siku. *(Makofi)*

(e) Kuimarisha ufugaji wa kuku wa kienyeji wanaofugwa na wananchi wengi walio masikini kwa kuwahamasisha juu ya utumiaji wa majogoo bora, ili kuongeza uzalishaji wa mayai na ukuaji wa kuku wanaozaliwa pamoja na kushajiisha matumizi ya chanjo ya mahepe.

(f) Kuanzisha kampeni ya unywaji wa maziwa na ulaji wa mayai katika jamii yetu. *(Makofi)*

(g) Kuanzisha utafiti shirikishi wa kuku katika kupata kuku wanaokua haraka, wanaotaga zaidi na wanaostahamili maradhi.

(h) Kuimarisha mfumo wa elimu kwa wafugaji kwa kutumia mashamba darasa, redio na televisheni, vijarida na vipeperushi, pamoja na kuongeza idadi na uwezo wa kitaaluma kwa wataalamu wa fani hiyo. Jumla ya wafugaji 15,000 watapatiwa elimu kupitia njia hizo.

(i) Kushajiisha ufugaji wa kuku wa kisasa kwa mashirikiano baina ya wawekezaji wa ndani na wafugaji wenyewe, ili kuongeza uzalishaji wa ndani wa mayai na nyama. Naomba nitoe habari njema kwamba Kampuni ya Sheikh Ali Youssuf na wizara yangu zimo katika hatua ya kutayarisha Hati ya Makubaliano ya uanzishaji uekezaji mkubwa wa ufugaji wa kuku wa mayai hapa Zanzibar.

Ni imani yangu kwa Sheikh Ali Youssuf tunavyomfahamu hasa sisi Wajumbe wa Baraza lako tukufu, uekezaji wake utaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya mifugo hapa Zanzibar. *(Makofi)*

(j) Kwa kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika pamoja na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto, Idara itashajiisha uundaji wa jumuia za ufugaji na kuzipatia mafunzo ya fani ya mifugo na uendeshaji.

(k) Kuzidisha mwamko wa usindikaji na matumizi ya mazao ya mifugo (nyama, maziwa, mtindi, jibini, siagi na samli) pamoja na kushajiisha wafugaji kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kisasa vya kusindika mazao ya mifugo sambamba na kutoa mafunzo ya usindikaji na masoko.

(l) Kuendeleza ushajiishaji wa matumizi ya gesi itokanayo na samadi na kufunga mitambo mitano (5) mipya kwa wafugaji wataojitokeza.

(m) Kukiimarisha Kituo cha Mbegu za Majani Kizimbani, kuendelea na mazungumzo na waekezaji kwa kuyaendeleza mashamba ya Kipange, Kitumba, Hanyegwa Mchana Chamanangwe, Magome na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 idara itatekeleza na kusimamia Mradi wa Kupandisha Ng'ombe kwa Sindano (Kiambatisho 2).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, idara hii ilikuwa sehemu ya Idara ya Maendeleo ya Mifugo ambayo ilipangiwa kupata shilingi 848,636,000/=. Kati ya hizo matumizi mengineyo yalipangiwa jumla ya shilingi 145,000,000/= kutoka serikalini. Hadi kufikia April 2011, shilingi 84,414,850/= zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 58.2 (Kiambatisho na. 11).

Kwa upande wa miradi ya maendeleo idara ilipangiwa jumla ya shilingi 147,000,000/= kutekeleza mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano. Hadi kufikia mwezi wa Aprili mradi ulipatiwa shilingi 135,500,384/= ambazo ni sawa na asilimia 92.2 (Kiambatisho na. 9).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, Idara hii ilikuwa sehemu ya Idara ya Maendeleo ya Mifugo ambayo ilipangiwa kupata shilingi 848,636,000. Kati ya hizo matumizi mengineyo yalipangiwa jumla ya shilingi 145,000,000 kutoka Serikalini. Hadi kufikia April 2011, shilingi 84,414,850 zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 58.2. Kwa upande wa miradi ya maendeleo Idara ilipangiwa jumla ya shilingi 147,000,000 kutekeleza mradi wa kupandisha ng'ombe kwa sindano. Hadi kufikia mwezi wa Aprili Mradi ulipatiwa shilingi 135,500,384 ambazo ni sawa na asilimia 92.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza malengo ya 2011/2012 Idara ya Uzalishaji Mifugo kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 226,248,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 141,500,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kazi za kawaida shilingi 89,448,000 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA HUDUMA ZA UTABIBU WA MIFUGO

Majukumu ya Idara

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Huduma za Utabibu wa Mifugo ina jukumu la kuhakikisha mifugo yote inayofugwa nchini inastawi na inakingwa na maradhi mbalimbali ya mifugo. Aidha, kuhakikisha mifugo yetu haienezi maradhi kwa binadamu kwa kufanya ukaguzi wa wanyama na bidhaa zao. Vilevile, Idara hii ina jukumu la kuondosha ukatili dhidi ya wanyama, kusimamia utoaji wa tiba na kinga kwa maradhi mbalimbali ya mifugo pamoja na kuzuia magonjwa yasiyo na mipaka *"Transbaundary Animal Diseases"* kuingia katika nchi yetu, kufanya uchunguzi wa mwenendo wa maradhi ya kuambukiza na yenye

kuathiri mifugo yetu, kubuni mbinu za kukabiliana na maradhi hayo na kufanya utafiti wa maradhi ya mifugo.

Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara hii ilikuwa ni sehemu ya Idara ya Maendeleo ya Mifugo ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na iliwekewa malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kutoa huduma za kinga, tiba, na ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji.

(b) Kuendelea kuimarisha karantini na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuikinga mifugo na binadamu dhidi ya maradhi yanayoweza kuletwa na mifugo au bidhaa zake kutoka nje ya nchi.

(c) Kuimarisha maabara za uchunguzi wa maradhi kwa kuzipatia zana na nyenzo za kufanyia uchunguzi wa maradhi hayo.

(d) Kuimarisha majengo yalioko katika chinjio kuu la Kisakasaka pamoja na uwekaji wa umeme katika kituo hicho na uwekaji wa uzio katika eneo la karantini.

(e) Kuanzisha eneo la karantini ya wanyama huko Pemba.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Idara ilitekeleza yafuatayo:-

(a) Kwa kushirikiana na Programu za *ASSP*/*ASDP*-L, Idara inaendelea na zoezi la kuchanja kuku wa kienyeji dhidi ya ugonjwa wa mahepe ambapo jumla ya kuku 223,573 wamepatiwa chanjo hiyo.

(b) Jumla ya wanyama 213,047 walikaguliwa na kuruhusiwa kuingia nchini. Kati ya hao, ng'ombe ni 6,586, mbuzi 648, kondoo 11, kuku (*vifaranga*) 205,791 na wanyama wengine 11. Aidha, bidhaa za mifugo zilizoingizwa nchini ni pamoja na mayai 138,229, nyama ya kuku kilo 6,565,

nyama ya ng'ombe kilo 8,225, nyama ya mbuzi kilo 14,065 na nyama ya kondoo kilo 13,765.

(c) Matengenezo ya maabara ndogo ya mifugo iliopo Chake chake Pemba na matengenezo ya sehemu ya maabara ya Maruhubi yamekamilika.

(d) Jumla ya eka kumi za eneo la karantini Kisakasaka zimefanyiwa usafi na kuzungushiwa miti hai. Sambamba na hayo matengenezo ya chinjio la Kisakasaka yameanza.

(e) Eneo la kuanzisha karantini ya wanyama Pemba limeshapatikana huko Nziwengi, ambapo kwa sasa Wizara ipo katika hatua za kulipima na kupata hatimiliki ya eneo hilo kabla ya kuanza ujenzi wa miundo mbinu. Aidha Wizara imeunda kamati ya pamoja baina ya maofisa wa Wizara, Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, pamoja na wafanyabiashara wa mifugo wa Mkoa wa Kaskazini Unguja ili kufanya utafiti ili kuangalia uwezekano wa kuanzisha kituo cha Karantini ya wanyama katika Mkoa Kaskazini Unguja.

(f) Kitengo maalum cha kuzuia ukatili dhidi ya wanyama chenye jukumu la kutoa elimu, ushauri na maelekezo juu ya matunzo mazuri ya wanyama kimeanzishwa. Jumla ya washiriki 50 kutoka vyombo vya ulinzi na usalama na Halmashauri za Wilaya walipata mafunzo juu ya haki za wanyama, uzuiaji wa mateso kwa wanyama na kinga dhidi ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa. Aidha, washiriki 120 wakiwemo watoa huduma za msingi za mifugo (*Community Animal Health Workers)*, walipewa mafunzo juu ya sheria za rasilimali ya mifugo, haki za wanyama na uzuiaji wa kichaa cha mbwa. Vilevile mikutano mengine kumi na moja ya kuwaelimisha wananchi kuhusu kichaa cha mbwa ilifanyika na kuhusisha washiriki 296 Unguja na Pemba.

(g) Jumla ya washiriki 2,500 kutoka Unguja na Pemba wamehudhuria mafunzo juu ya tahadhari ya kujilinda na maradhi mbali mbali ya kuambukiza. Aidha, wataalamu wanne wa Idara wamehudhuria mafunzo mbali mbali ya kuimarisha taaluma zao, ikiwa ni pamoja na namna ya

kubaini vimelea vya mafua makali ya ndege katika maabara.

(h) Kliniki za mifugo za wilaya zilizopo Kengeja, Konde, Maruhubi na Mangapwani na Micheweni ziko katika hatua ya mwisho ya matengenezo.

Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012 Idara inalenga kutekeleza yafuatayo: -

(a) Kuendelea kutoa huduma za tiba, kinga na uchunguzi wa maradhi ya mifugo kwa nia ya kuboresha afya za mifugo yetu nchini.

(b) Kuendelea kuimarisha karantini na ukaguzi wa mifugo na mazao yake kwa lengo la kuikinga mifugo na binadamu dhidi ya maradhi yanayoweza kuletwa na mifugo au bidhaa zake kutoka nchi za nje.

(c) Kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, kuziendeleza maabara za uchunguzi wa maradhi kwa kuzipatia zana na nyenzo nyengine za kufanyia uchunguzi wa maradhi.

(d) Kufanya ukarabati wa kliniki ya mifugo ya Dunga na ujenzi wa kliniki ya mifugo Unguja - Ukuu.

(e) Ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya kliniki 5 za mifugo zilizofanyiwa ukarabati.

(f) Kuendelea na uimarishaji wa mazingira ya kituo cha karantini Kisakasaka.

(g) Jumla ya dozi milioni moja za chanjo ya mahepe zitanunuliwa na kuchanjwa kuku wa kienyeji Unguja na Pemba.

(h) Kuendelea na utaratibu wa kupata hatimiliki ya eneo la Karantini Nziwengi Pemba pamoja na vituo vyengine vya mifugo, pia kuendelea kukamilisha hatua za uanzishaji wa eneo la Karantini huko Mkoa wa Kaskazini Unguja.

(i) Kutoa taaluma kwa wafugaji juu ya kuwakinga wanyama wao na maradhi ya kuambukiza kupitia vyombo vya habari, vijarida, vipeperushi pamoja na semina.

(j) Kuendelea kutoa taaluma kwa jamii juu ya kuepukana na tabia ya ukatili wa wanyama, na kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali kama *ZALWEDA* na *ZAASO* ya mama Anna iliyopo Kiyanga ya kupiga vita ukatili wa Wanyama.

(k) Kutayarisha mpango wa tahadhari ya mapema juu ya magonjwa ya miripuko katika sekta ya mifugo kwa kushirikiana na *"FAO"* kupitia programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara itasimamia utekelezaji wa miradi miwili ambayo ni:-

(a) Mradi wa Kudhibiti Kichaa cha Mbwa unaotekelezwa na SMZ ikishirikiana na *"World Society for Protection of Animals" (WSPA)* kwa Unguja na *"World Health Organization" (WHO)* kwa Pemba (Kiambatisho 3).

(b) Mradi wa Kudhibiti Mafua Makali ya Ndege na Nguruwe unaoendeshwa kwa ushirikiano wa SMZ na Shirika la Umoja wa Mataifa la *"UNICEF"* na *"European Union"* (Kiambatisho 4).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mapato yatokanayo na huduma ya utabibu wa mifugo yalikadiriwa kuwa shilingi 48,000,000 kwa Unguja. Hadi kufikia mwezi wa Machi jumla ya shilingi 27,628,560 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 57.6 ya lengo (Kiambatisho na 8). Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mapato yanayotokana na huduma za Utabibu wa mifugo kwa Unguja yanakadiriwa kuwa ni Shilingi 48,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Idara hii ilikuwa sehemu ya Idara ya Maendeleo ya Mifugo kama ilivyoelezwa kwenye Idara ya Uzalishaji Mifugo. Katika kasma ya maendeleo, Mradi wa Kudhibiti Mafua ya Ndege uliombewa shilingi 67,000,000. Mpaka kufikia mwezi wa Aprili 2011, mradi umetiliwa shilingi 53,854,949 sawa na asilimia 80.4. Mradi wa Kichaa cha Mbwa uliombewa shilingi 65,000,000 na mpaka kufikia mwezi wa Aprili 2011 umetiliwa shilingi 27,644,667 sawa na asilimia 42.5 (Kiambatisho na. 9).

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza malengo ya mwaka 2011/2012 Idara ya Utabibu wa Mifugo kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 283,619,416 kwa kazi za kawaida na shilingi 150,000,000 zimeombewa kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kazi za kawaida shilingi 60,431,000 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI

Majukumu ya Idara

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kuwahudumia wavuvi pamoja na wadau mbalimbali wanaojishughulisha na uvuvi kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi. Aidha, Idara ina jukumu la kuhakikisha kuwa rasilimali za baharini zinalindwa kwa kuzingatia matumizi bora na endelevu sambamba na jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za uvuvi kwa lengo la kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali za bahari.

Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 malengo ya Idara ya Uvuvi yalikuwa kama yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake.

(b) Kuendelea kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii ya ukanda wa pwani.

(c) Kuwashajiisha wavuvi vijana kuacha kuvua katika maeneo ya hifadhi na badala yake kwenda kuvua katika kina kirefu.

(d) Kudhibiti matumizi ya nyavu zenye macho madogo katika maeneo ya hifadhi na kupiga marufuku matumizi ya nyavu za *"monofilament"*.

(e) Kuendeleza kazi za doria katika maeneo ya hifadhi kwa kushirikiana na jamii.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza malengo ya 2010/2011 Idara ilifanya yafuatayo:-

(a) Kuendelea kushirikisha jamii katika uhifadhi wa maeneo ya hifadhi ya rasilimali za baharini kwa kuimarisha kamati za wavuvi pamoja na kamati za doria vijijini. Jumla ya kamati 61 kwa Unguja na 28 za Pemba zimeshiriki kikamilifu katika doria za kukabiliana na uvuvi haramu na shughuli za kitalii. Jumla ya vyombo viwili na vifaa vyake vya uvuvi haramu (nyavu sita, mashine moja na bunduki nne) vilikamatwa na hatua za kisheria zimechukuliwa.

(b) Doria 48 maalum za kudhibiti uvuvi haramu katika maeneo ya hifadhi za kisiwa cha Mnemba na Ghuba ya Chwaka "*MIMCA*", Ghuba ya Menai "*MBCA*" na Mkondo wa Pemba "*PECCA*" zimefanyika kwa kushirikiana na wanajamii, askari Polisi pamoja na KMKM. Katika doria hizo jumla ya vipande 11 vya nyavu za macho madogo na bunduki nne pamoja na vyombo vitatu vilikamatwa na mashauri yao kufikishwa katika vyombo vya sheria.

(c) Jumla ya doria 270 za kawaida zenye lengo la kudhibiti na kukagua leseni pamoja na harakati za kitalii zinazoendelea katika maeneo ya hifadhi ya kisiwa cha Mnemba, ghuba ya Menai na mkondo wa Pemba zilifanyika

(d) Idara iliandaa mafunzo kuhusiana na mpango wa usimamizi wa athari za kimazingira kwa jamii *(Community Mitigation Action Plans)* katika Shehia 10 zilizopo katika eneo la hifadhi ya kisiwa cha Mnemba na ghuba ya Chwaka na kila shehia iliwakilishwa na wanavijiji 10.

(e) Mafunzo kuhusiana na umuhimu wa kuwahifadhi na kuwalinda wanyama walio hatarini kutoweka wakiwemo pomboo, nyangumi na kasa yalitolewa. Mafunzo hayo yalitolewa kwa wamiliki wa mahoteli, wapelekaji watalii katika maeneo ya hifadhi pamoja na wavuvi waliokuwepo katika maeneo ya hifadhi za kisiwa cha Mnemba na Ghuba ya Menai. Jumla ya washiriki 220 walihudhuria mafunzo hayo.

(f) Jumla ya mikutano 48 imefanyika kwa shehia zote za *"MBCA"*, *"MIMCA"* na *"PECCA"* kwa lengo la kuwahamasisha wanajamii juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani na athari ya matumizi ya nyavu katika maeneo ya uhifadhi.

(g) Sheria mpya ya Uvuvi No. 7 ya mwaka 2010 imeshapitishwa na kutiwa saini na Mhe. Rais Mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa Awamu ya Sita mnamo tarehe 26 Julai 2010.

(h) Ujenzi wa ofisi mpya za Idara ya Uvuvi Unguja na Pemba unaendelea na ujenzi wa majengo matatu ya maeneo ya hifadhi ya kisiwa cha Mnemba na Ghuba ya Chwaka, Ghuba ya Menai na Mkondo wa Pemba umekamilika na yameshahamiwa.

(i) Kazi ya kuanzisha wigo wa maeneo mapya ya hifadhi ya visiwa vya Changuu na Bawe "*CHABAMCA*", Tumbatu "*TUMCA*" na Kojani "*KOMCA*" pamoja na kuyatangaza kisheria imeanza.

Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 malengo ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ni kama yafuatayo:-

(a) Kufanya ukaguzi wa maeneo ya uvuvi kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwa kushirikiana na kamati za wavuvi za jamii.

(b) Kuendesha mafunzo kwa wanajamii juu ya umuhimu wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya bahari na rasilimali zake. Jumla ya vijiji 60 na wavuvi 1,200 watafaidika na mafunzo haya.

(c) Kuendesha mafunzo kwa wanajamii juu ya uelewa na kuwashirikisha katika uhifadhi wa wanyama wa baharini waliohatarini kutoweka kama pomboo, nyangumi na kasa.

(d) Kuainisha maeneo madogo maalum yenye umuhimu kwa uhifadhi wa rasilimali za bahari katika ngazi ya jamii.

(e) Kuendesha mafunzo kwa wadau mbali mbali wa utalii kwa lengo la kuhifadhi rasilimali za bahari na mazingira yake.

(f) Kununua vifaa kwa ajili ya ofisi hizo zilizokamilika za "*MENAI*", "*MIMCA*", na "*PECCA*", na pia kukamilisha ujenzi wa ofisi za Idara Unguja na Pemba pamoja na kununua vifaa vya ofisi hizo.

(g) Kusimamia ujenzi wa soko la Kisasa Tumbe.

(h) Kuanzisha mafunzo kwa wavuvi wazalendo kuvua kwenye maji ya kina kirefu, na kutafuta boti za kisasa kwa ajili ya mafunzo hayo. Mhe. Mwenyekiti, katika kufanikisha mafunzo haya ambayo ni muhimu katika kuanzisha "*fleet*" ya wavuvi wazalendo, wizara yangu inafanya mazungumzo na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuona namna ya kuanzisha mtaala wa uvuvi wa Bahari Kuu katika vyuo vyetu vya amali vilvyopo Mkokotoni na Vitongoji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara itasimamia na kutekeleza mradi mmoja wa Usimamizi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani *"MACEMP"* (Kiambatisho na. 5).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 mapato ya leseni za vyombo na za wavuvi yalikadiriwa kuwa shilingi 20,000,000 kwa Unguja. Hadi kufikia mwezi wa Machi jumla ya shilingi 8,780,100 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 43.90 ya lengo. Kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 mapato yanayotokana na leseni za uvuvi kwa Unguja yanakadiriwa kuwa ni shilingi 20,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 jumla ya shilingi 669,344,000 ziliombwa kutekeleza kazi za kawaida na za maendeleo. Kati ya hizo shilingi 401,678,000 zilikuwa kwa kazi za miradi ya maendeleo na hadi kufikia mwezi wa Aprili shilingi 115,000,000 zimepatikana ambazo ni sawa na asilimia 28.6 (Kiambatisho na. 9). Kwa kutekeleza kazi za kawaida jumla ya shilingi 267,666,000 ziliombwa ambapo shilingi 51,678,000 kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2011 shilingi 11,000,000 zimepatikana kwa matumizi mengineyo ambazo ni sawa na asilimia 21.3 (Kiambatisho na. 11).

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 201,185,375 kwa kazi za kawaida na shilingi 216,000,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kazi za kawaida shilingi 60,338,000 ni kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MAZAO YA BAHARINI

Majukumu ya Idara

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mazao ya Baharini ina majukumu ya kuwahudumia wafugaji wa mazao ya baharini, wakulima wa mwani pamoja na wadau wengine wanaojishughulisha na mazao ya baharini kwa ajili ya kuinua hali zao kiuchumi. Aidha, Idara ina jukumu la kukuza, kuendeleza, kudhibiti na kufuatilia shughuli zote za ufugaji na ukulima wa mazao ya baharini kwa madhumuni ya kuwa na ufugaji bora pamoja na kuimarisha ubora na thamani ya mazao ya baharini.

Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 Idara ilikuwa na malengo yafuatayo:-

(a) Kuendelea kuishirikisha jamii katika uhifadhi wa rasilimali za baharini na mazingira yake.

(b) Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira ya baharini kwa jamii ya ukanda wa pwani kwenye maeneo ya ufugaji viumbe vya baharini na ukulima wa mwani.

(c) Kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya mazao ya baharini.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2010/2011 Idara ilitekeleza mambo yafuatayo:-

(a) Kutoa elimu ya mazingira kwa wanajamii wa shehia zote za mwambao wa bahari kwa Unguja na Pemba kwa kutumia njia mbali mbali zikiwemo mikutano na semina. Jumla ya mikutano na semina 25 zilizowashirikisha wanajamii 4,000 zilifanyika.

(b) Juhudi za kuwahamasisha wavuvi kujihusisha na ufugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini zimeendelea kuchukuliwa kwa kushajiisha uanzishwaji wa mabwawa ya ufugaji wa samaki katika maeneo ya Chukwani, Bumbwini Makoba, Fukuchani na Mangapwani kwa Unguja na Kiwani, Chambani, Makombeni na Mtangani kwa Pemba.

Katika juhudi hizo jumla ya mabwawa manane yametayarishwa na kuanzishwa.

(c) Kazi ya kutoa taaluma ya ufugaji wa mazao ya baharini kama vile ufugaji wa chaza, samaki, kaa pamoja na ukulima na uanikaji wa mwani zinaendelea kutolewa. Kwa hivi sasa kuna jumla ya vikundi 75 vyenye wanachama 1,500 wanaojihusisha na ufugaji wa mazao ya baharini kama vile samaki, chaza, kaa na kasa.

(d) Kuhamasisha wakulima wa mwani kujiunga na jumuiya zao za uzalishaji. Idara kwa kushirikiana na wakulima wa mwani imeanza utaratibu wa kuanzisha jumuiya ya wakulima wa mwani Zanzibar *(Zanzibar Seaweeds Farmers Association)* itakayowawakilisha wakulima wa mwani katika jumuiya ya wafanya biashara na wenye viwanda na Kilimo Zanzibar *(Zanzibar Chamber of Commerce, Industry and Agriculture)*.

Malengo ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara ya Mazao ya Baharini imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

(a) Kuhamasisha matumizi ya mwani ikiwemo kutengeneza sabuni na usarifu mwengine kwenye matumizi ya vyakula mbali mbali.

(b) Kutoa elimu kwa wakulima juu ya ukulima bora wa mwani utakaopelekea kuzalisha mwani bora na wa kiwango cha juu, na pia kutoa taaluma juu ya ujuzi wa ufugaji wa mazao ya baharini. Naomba kutoa habari njema kwamba katika kutekeleza azma hii, kundi la mwanzo la vijana 30 litaondoka wakati wowote kwenda Jamhuri ya Watu wa China kwenda kuchukua ujuzi wa ufugaji wa mazao ya baharini. Vijana hawa 30 wametoka kwenye majimbo ya waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili, mara kundi hili litaporudi, makundi mengine yataandaliwa na kupewa mafunzo ndani na nje ya nchi kwa lengo la kutoa taaluma hii muhimu kwa wananchi wetu.

(c) Kuhamasisha wakulima wa mazao ya baharini kuunda vikundi vya ushirika vya kuweka na kukopa ili kuwa na

mitaji ambayo itawawezesha kuanzisha vyanzo vya ziada vya kujiongezea kipato na kuwainua kiuchumi.

(d) Kuhamasisha wanajamii kujihusisha na ufugaji wa samaki, chaza, uzalishaji wa lulu na kaa, pamoja na kuimarisha usarifu na uuzaji wa mazao hayo katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

(e) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Sayansi ya Baharini ya Chuo Kikuu cha Dar-es- Salaam kuendeleza utafiti wa mwani mnene ambao unastahamili hali ya hewa na wenye tija zaidi, pia kufanya utafiti wa mazao ya kamba na majongoo bahari.

Mhe. Mwenyekiti, mapato yatokanayo na ushuru wa usafirishaji wa mazao ya baharini nje ya Zanzibar yalikadiriwa kuwa shilingi 40,000,000 kwa Unguja. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011 jumla ya shilingi 32,635,000 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 81.6 ya lengo (Kiambatisho na. 8). Kwa mwaka wa fedha 2011/2012 mapato yanayotokana na mazao ya baharini kwa Unguja yanakadiriwa kuwa Shilingi 40,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 Idara ya Mazao ya Baharini ilikuwa haijaundwa, hivyo haikuwa na bajeti rasmi. Katika kutekeleza malengo ya mwaka wa fedha wa 2011/2012 Idara hii kwa Unguja inaombewa jumla ya shilingi 120,667,732 kutekeleza kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 46,122,000 ni kwa matumizi mengineyo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara kwa upande wa Pemba kwa kushirikiana na Idara mbali mbali zilizomo katika Wizara hii. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, kazi zilizotekelezwa na Ofisi Kuu Pemba ni miongoni mwa kazi zilizokwisha elezwa chini ya Idara zote ziliomo katika Wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011 Ofisi Kuu Pemba ililenga kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 15,000,000/- kutokana na utoaji leseni za uvuvi, mazao ya baharini na ada ya huduma za utibabu. Hadi kufikia mwezi wa Machi ilikusanya jumla ya shilingi 6,623,000/- sawa na asilimia 44 ya lengo. Kati ya fedha zilizokusanywa, Idara ya Uvuvi ilikusanya shilingi 1,905,700, Idara ya Mazao ya Baharini ilikusanya shilingi 1,689,000 na Idara ya huduma za Utabibu ilikusanya shilingi 3,028,300. Kwa mwaka wa fedha

2011/2012 Ofisi Kuu Pemba inakadiria kukusanya jumla ya mapato ya Shilingi 12,000,000. Mapato haya yatatokana na huduma za utibabu wa mifugo (7,000,000), leseni za uvuvi (3,000,000) na mazao ya baharini (2,000,000).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutekeleza malengo yaliolezwa katika Idara mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi Kuu Pemba imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 623,075,788 kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 352,501,000 ni kwa matumizi mengineyo, ambapo Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekadiriwa kutumia shilingi 37,044,000, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imekadiriwa kutumia shilingi 68,656,000, Idara ya Mazao ya Baharini imekadiriwa kutumia shilingi 79,135,000, Idara ya Maendeleo ya Uvuvi imekadiriwa kutumia 82,374,000, Idara ya Uzalishaji wa Mifugo imekadiriwa kutumia shilingi 33,871,000 na Idara ya Utabibu wa Mifugo imekadiriwa kutumia shilingi 51,421,000. Mchanganuo wa makisio kwa Idara zote za Wizara ya Mifugo na Uvuvi ziliopo Pemba unaonekana katika kiambatisho na. 12.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2010/2011

Ukusanyaji wa Mapato 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 1,048,474,000. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2011 Wizara ilikusanya mapato ya shilingi 333,168,796.30, ambayo ni sawa na asilimia 32 ya lengo lililowekwa (Kiambatisho na. 8). Mapato kidogo yaliyokusanywa yamesababishwa zaidi na kushuka kwa mapato ya leseni za uvuvi wa bahari kuu. Hali hii inatokana na kuwepo kwa maharamia wa baharini katika pembe ya Afrika Mashariki.

Matumizi ya Fedha 2010/2011

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2010/2011 sekta za mifugo na uvuvi zilikuwa ni sehemu ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira. Sekta hizo ziliidhinishiwa jumla ya shilingi 1,796,980,000 ambapo shilingi 1,116,302,000 zilikuwa kwa kazi za kawaida na shilingi 680,678,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kawaida shilingi 196,678,000 zilitengwa kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi wa Aprili, fedha zilizopatikana ni shilingi 95,414,850 kwa matumizi mengineyo ambayo ni sawa na asilimia 48.5. Aidha, jumla ya shilingi 332,000,000 zilitolewa kwa matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 48.8 (Kiambatisho 9, 10 & 11).

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA 2011/2012

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya shilingi 1,020,000,000 kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali vya mapato (Kiambatisho 8). Sambamba na makusanyo hayo, Wizara yangu inatarajia kutumia jumla ya shilingi 11,628,445,000. Kati ya hizo shilingi 8,788,945,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo kwa kutekeleza miradi miwili ya maendeleo (Mradi wa Kichaa cha Mbwa na Mradi wa MACEMP) na shilingi 2,839,500,000 ni kutoka SMZ. Katika fedha za SMZ, jumla ya shilingi 2,089,000,000 zimetengwa kwa kazi za kawaida na Shilingi 750,500,000 kwa kazi za maendeleo. Kati ya fedha za kazi za kawaida jumla ya shilingi 1,289,000,000 ni kwa mishahara na shilingi 800,000,000 ni za matumizi mengineyo, (Kiambatanisho 9 hadi 12).

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzishukuru taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Marekani, Jamhuri ya Watu wa China, Jamhuri ya Watu wa Korea, Serikali ya India, Serikali ya Israel, Serikali ya Japan, Serikali ya Misri, Serikali ya Uholanzi, Serikali ya Uingereza na Ufalme wa Oman kwa kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi. Aidha, napenda kuyashukuru mashirika ya maendeleo yakiwemo "GEF", "KOICA", "SADC", "UNICEF", "WHO", "WSPA", “USAFRICOM”, Benki ya Dunia, Jumuiya ya Maendeleo ya Afrika "AU", Shirika la Chakula Duniani "FAO", Shirika la Maendeleo la Japan "JICA", Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo "IFAD", Shirikisho la Nchi za Mashariki ya Afrika "EAC", na Umoja wa nchi za Ulaya "EU" Vile vile napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru Wizara za SMZ, taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali kama Taasisi ya Sayansi ya Baharini, ” *Indian Ocean* Marine Affairs Society” na “Zanzibar Society for Protection of Animal” ambazo zinasaidia kuleta maendeleo katika sekta za Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati na kuwapongeza Katibu Mkuu Dk. Kassim Gharib Juma, Naibu Katibu Mkuu Dk. Omar Ali Amir, Afisa Mdhamini Pemba, Nd. Mayasa Ali Hamadi, Wakurugenzi, wataalamu na wafanyakazi wote wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi walioko Unguja na Pemba kwa utendaji wao mzuri unaoongeza ufanisi katika Wizara na kukubali kwao kufanyakazi katika mazingira magumu. Vile vile napenda kuwapongeza, wafugaji, wavuvi, wakulima na wafanyabiashara wa mwani, na wadau wengine wa sekta ya mifugo na uvuvi kwa jitihada na mashirikiano yao wanayotoa katika kuendeleza sekta hizi pamoja na

changamoto zinazowakabili. Napenda kuwahakikishia kwamba mchango wao tunauthamini sana na tutaendelea kuyafanyia kazi mapungufu yanayojitokeza kulingana na vipaumbele na nyenzo zilizopo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mkosefu wa shukurani iwapo sitawashukuru Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Madiwani, Masheha, Kamati za Maendeleo za Shehia, Kamati za Wavuvi, Vikosi vya SMZ na vyombo vya habari kwa mashirikiano yao mazuri waliyoyatoa kusaidia utekelezaji wa kazi zetu. Vile vile tunawashukuru wananchi wote kwa kuitikia wito wa kutumia mazao ya mifugo na uvuvi katika milo yao na tunawashajiisha wale bidhaa za ndani ili kuimarisha afya zao na kuwainua wazalishaji wetu kimapato. Hivyo basi, kwa niaba ya Wizara yangu napenda kuchukua fursa hii adhimu kuwaomba wananchi kuongeza juhudi katika uzalishaji na matumizi ya bidhaa hizo ili kuchangia katika suala zima la kufikia uhakika wa chakula hapa nchini kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nawaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako tukufu waipokee na kuijadili na kuikubali bajeti ya Wizara yangu na watupe maoni, ushauri na mapendekezo katika kuendeleza sekta ya mifugo na uvuvi kwa manufaa ya wafugaji, wavuvi na wananchi na Taifa hili kwa ujumla. Aidha, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 11,628,445,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kati ya fedha hizo shilingi 2,089,000,000 ni kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi 9,539,445,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kazi za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi ni Wizara yao Wajumbe waheshimiwa wa baraza hili tukufu, wavuvi wetu wachuuzi, wakaanga samaki, wakaushaji dagaa, wanywaji wa supu zote za pweza na zile nyengine, wafanyabiashara na wakulima wa mwani, wafugaji wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa, wachungao ng'ombe na mbuzi, wauzaji wa mayai, wakamuaji wa maziwa, wanywao maziwa na wanyonyao maziwa. Mhe. Mwenyekiti, watakuwa wanatusikiliza kwa makini na Wajumbe wa Baraza lako tukufu katika mjadala wa bajeti hii wanatusubiri tuwatengenezee mambo yao. Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa na unyenyekevu wa hali ya juu naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Asaa Othman Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari): Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani zote tunazitoa kwa Mola muweza ambaye kwa rehema zake ametuweka hai na uzima hadi siku ya leo. Nimesimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari juu ya mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa pongezi zetu za dhati kwa Mhe. Said Ali Mbarouk, Waziri wa Mifugo na Uvuvi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, pamoja na watendaji wengine wote wa wizara hii kwa kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kushirikiana bega kwa bega na kamati kila wanapohitajika kufanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila ikiwa sitatoa shukurani za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kwa kutenga muda wao na kutekeleza majukumu ya kamati yetu, kila wanapohitajika kufanya hivyo, bila ya kujali wingi wa majukumu ya kifamilia na kitaifa waliyonayo. Naomba niwatambulishe Wajumbe wa Baraza lako tukufu wana kamati hao kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Asha Bakari Makame	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mohammed Said Mohamed	-	M/ Mwenyekiti
3.	Mhe. Asaa Othman Hamad	-	Mjumbe
4.	Mhe. Salim Abdalla Hamad	-	Mjumbe
5.	Mhe. Abdi Mosi Kombo	-	Mjumbe
6.	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Mjumbe
7.	Mhe. Kazija Khamis Kona	-	Mjumbe
8.	Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu
9.	Ndg. Haji Khatib Haji	-	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza sana wizara kwa kufanikiwa kuibua miradi mbali mbali ya maendeleo ya kilimo na mifugo, kama Mradi wa Kusimamia Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani wenye jumla ya shilingi 8,892,445,000/= unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Programu ya Kuendeleza Miundombinu ya Ufugaji iliyotengewa shilingi 243,000,000/= inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar yenyewe. Mradi wa Kupandisha Ngo'ombe

kwa Sindano uliotengewa shilingi 141,500,000/= ambao pia unafadhiliwa na SMZ yenyewe. Utekelezaji bora wa miradi hii utaiwezesha wizara hii kupiga hatua kimaendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu inatoa pongezi za dhati kwa wizara kwa kuifanyia matengenezo maabara ndogo ya mifugo iliyopo Chake Chake Pemba, na sehemu ya maabara ya Maruhubi. Hatua hii ni muhimu kwani uchunguzi wa mifugo utatuwezesha kuyajua haraka maradhi yanayoikabili na kuipatia tiba inayofaa.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefurahishwa na wizara hii kwa kufanya mapitio ya sekta za mifugo na uvuvi pamoja na kutayarisha rasimu ya mpango mkakati wa sekta hizo ambayo tayari imewasilishwa Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Hii ni hatua muhimu katika kuleta mageuzi ya mifugo na uvuvi ili kuingia katika shughuli zinazotegemewa kibiashara. Aidha, mapendekezo ya miradi ya kuimarisha miundombinu ya mifugo na uvuvi yamewasilishwa Serikalini kwa washirika mbali mbali wa maendeleo na kilichobakia ni kumalizika kwa matayarisho kwa ajili ya kuanza kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tunatoa pongezi za dhati kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kusindika maziwa na kuzalisha siagi na mtindi. Hatua hii ni muhimu kwani itawawezesha wafugaji kuongeza thamani kwenye maziwa mara baada ya kuyasarifu na hatimaye kupata faida kubwa.

Halikadhalika, mchango wa sekta hii ya mifugo umekuwa na kufikia asilimia 4.7 ya pato la taifa kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Pamoja na ongezeko hilo, kamati yetu inaishauri wizara kuendelea kubuni mikakati madhubuti ya kukuza uzalishaji kupitia sekta hii ili iweze kuchangia zaidi katika jitihada za nchi yetu kujikwamua kiuchumi.

Aidha, kupitia programu mbali mbali za uhamasishaji wa jamii zinazofanywa na wizara, wafugaji wengi wamepata muamko wa namna bora ya kufuga pamoja na kutambua umuhimu wa kinga na tiba kwa wanyama wao.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na kupatiwa taaluma wavuvi pamoja na kuimarishwa kwa miundombinu ya uvuvi hatua kwa hatua, kamati yetu inatembea kifua mbele kwa mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, sekta ya uvuvi ilichangia kwa asilimia 6.1 kwenye pato la taifa. Kiwango hiki kinatarajiwa kuongezeka katika mwaka wa fedha 2011/2012 kwa kuendelezwa juhudi za Serikali na wananchi wake, kwani wahenga walisema “penye nia ipo njia”.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yetu imeipitisha bajeti ya wizara hii ingawa haikuridhika na mgao mdogo wa fedha walizopatiwa, jambo ambalo limepelekea baadhi ya kasma za wizara hii kuwa na fedha zisizowiyana kabisa na matumizi yaliyoelezwa. Hivyo, ni kusema kwamba, kwa kiasi kikubwa bajeti ya wizara hii haitoiwezesha wizara kufanya shughuli zake ipasavyo. Kwa mfano, kasma 211110 (posho maalumu) ambayo imetengewa shilingi 50,000/=, kasma 220302 (safari za nje) ambayo ina jumla ya shilingi 3,500,000/=. Halikadhalika, kasma nyengine nyingi zilizomo kwenye vifungu vya wizara hii ziko katika hali hiyo hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imefurahishwa sana na mafanikio makubwa waliyoyapata wafugaji wa mbuzi wa maziwa, ambao walianza mradi huo kwa kukopeshwa mbuzi mmoja kwa kila mfugaji kupitia mpango wa kopa mbuzi lipa mbuzi wa *HPI* na *PADEP*. Mradi huu umeleta mafanikio makubwa kwa wafugaji kwani wameweza kujikimu kwa matumizi yao na familia zao kutokana na faida kubwa wanayoipata kwa mauzo ya maziwa na nbuzi wenyewe. Tunaiomba wizara kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wafugaji hao zikiwemo mahitaji ya beberu kwa ajili ya mbegu, upungufu wa maji, uhaba wa madaktari wa mifugo na ukosefu wa njia bora za kuhifadhi maziwa kwa vile umeme upo mbali kidogo na maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaitaka Wizara ya Mifugo na Uvuvi hususan kwa upande wa Afisi ya Pemba kuwa na ubunifu wa miradi mbali mbali itakayoingiza mapato kwa maslahi ya wizara na taifa kwa ujumla, badala ya kutegemea ada ya mazao ya baharini na utibabu wa vinyama pekee ambao kwa mwaka huu wa fedha inatarajiwa kukusanya shilingi 5,000,000/= tu. Kiwango hiki ni kidogo mno hasa tukizingatia mahitaji makubwa ya wizara hii changa ambayo inahitaji kujiimarisha kwa kuanzia na majengo, rasilimali watu na vyombo vya usafiri.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya uvuvi ni moja kati ya sekta muhimu sana katika kuikwamua nchi yetu kiuchumi kutokana na kuwemo kwa rasilimali muhimu katika sekta hiyo hususan mazao ya baharini (samaki nk.). Kamati ilipata nafasi ya kuonana na viongozi na watendaji wa Idara ya Uvuvi, wavuvi pamoja na watendaji wa hifadhi za mazingira ya bahari. Kamati pia ilitembelea ofisi mpya ya Mradi wa Hifadhi ya Kisiwa cha Mnemba na Ghuba ya Chwaka (*MIMCA-Mnemba Island Marine Consevation Area*) iliyoko Uroa.

Aidha, uvuvi husaidia sana katika kuimarika kwa Sekta ya Utalii. Hivyo ni vyema Serikali ikatilia mkazo zaidi katika uhifadhi wa bahari hususan suala la kufanya doria. Aidha, ufanyaji wa doria katika fukwe utasaidia kuzuia uvamizi wa bahari yetu unaofanywa na meli za nje kuja kuvua kinyume na

sheria. Kwa mnasaba huu kamati inaiomba Serikali kuingiza fedha za kutosha katika fungu la mafuta kwa ajili ya doria ya baharini.

Kamati imebaini kuwa idadi ya wavuvi sasa imeongezeka kwa kiasi kikubwa na ambao uwezo wao ni wa kuvua uvuvi wa ndani tu na eneo wanalovua kwa sasa limekuwa dogo. Hivyo, kuna haja kubwa kwa Serikali kuona umuhimu wa kuanzisha chuo maalum cha uvuvi hapa Zanzíbar ili vijana wawe na taaluma ya kutosha kwa uvuvi wa kisasa nao ni wa bahari kuu, ambao utahitaji elimu ya kuendesha meli za uvuvi, matumizi ya mbinu na vifaa vya kisasa vya uvuvi

Pamoja na kuwepo haja ya kuanzisha Chuo cha Uvuvi, kuna haja pia ya kuwawezesha wavuvi waliopo kwa Serikali kuwapatia nyenzo zikiwemo mashine za *horse power* 40 ili angalau waweze kwenda mbali zaidi ya wanapofika sasa kwa ajili ya shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilielezwa kuwa aina ya ukulima wa mwani kwa kutumia vijiti huharibu mazingira kwani huharibu mazalia ya samaki, hupunguza kina cha bahari kwa kusababisha kufanyika kwa mafungu (mkusanyiko wa mchanga). Hivyo, kutokana na hali hiyo na tukizingatia kuwa tija ya mwani imeongezeka kiasi ni vizuri kwa Serikali kuaandaa mazingira bora zaidi yatakayowasukuma wananchi kuimarika kiuchumi bila ya kuleta athari za aina yeyote kama vile ufugaji wa samaki na chaza.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara kushirikiana bega kwa bega na taasisi nyengine za ulinzi na usalama wa taifa, ili kulitafutia ufumbuzi tatizo la kuwepo kwa maharamia wa baharini katika pembe ya Afrika Mashariki. Kwa kweli, maharamia hawa wanatupunguzia mapato nchini mwetu kutokana na kupunguza idadi ya wavuvi kwa hofu ya maharamia hao. Kwa mwaka uliopita wa fedha, wizara ilikusanya asilimia 32 tu ya kiwango kilichootarajiwa. Hivyo, kipaumbele maalumu cha kulinda eneo letu la bahari kinahitajika ili kuwapa fursa na uhuru zaidi wananchi kujitafutia riziki zao.

Mhe. Mwenyekiti, uhifadhi wa viumbe wa baharini ni suala muhimu linalotiliwa mkazo na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Kwa mantiki hiyo basi wizara imetoa mafunzo kuhusiana na umuhimu wa kuwahifadhi na kuwalinda viumbe bahari walio hatarini kutoweka kama pomboo, nyangumi na kasa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 1,020,000,000/=. Aidha, naliomba Baraza hili tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi 11,628,445,000/= kwa wizara hii, kati ya fedha hizo shilingi 2,089,000,000/= ni

mchango wa Serikali na shilingi 9,539,445,000/= ni mchango kutoka kwa wahisani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya kamati yangu na wananchi wa Jimbo langu dume la Wete naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwa sababu jimbo langu lina wavuvi na wafugaji naomba uniruhusu kusema machache juu ya sekta hizi.

Mhe. Mwenyekiti, sekta ya mifugo ina mchango mkubwa kwa kuinua pato la mtu mmoja mmoja na la kitaifa. Hivyo, kutokana na mwamko wa wananchi kwa sekta ya mifugo sasa hivi wananchi wanajitahidi kufuga ng'ombe wa maziwa, mbuzi wa maziwa, kuku wa mayai na kuku wa nyama. Mazao haya yana faida ndani ya kiwiliwili cha binadamu yanaongeza lishe, yanaongeza kipato, lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna faida kubwa ya mbolea ya wanyama kwa mazao yetu ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali tunayokwenda nayo sasa athari kubwa ya mazingira kutokana na utumiaji wa mkaa na ukataji wa miti matumizi ya gesi kwa matumizi ya nyumbani ni jambo la kutiliwa mkazo. Sambamba na hilo sekta hii imekabiliwa na changamoto nyingi, kwanza ni maslahi madogo ya wafanyakazi. Kwa hivyo, naiomba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein, Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Seif Ali Iddi mafya haya matatu yameleta matumaini kwa wa Zanzibari. Mhe. Mwenyekiti, hatuna budi kuwaunga mkono kwa jitihada zao zote wanazozifanya ili tuweze kukwamuka katika dimbwi kubwa la umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo pia lipo la taaluma ndogo kwa wafugaji juu ya uhaba wa elimu kwa wafanyakazi kama hotuba ya Mhe. Waziri ilivyoeleza, lakini pia kukosekana kwa vitendea kazi vyenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuipongeza kwa dhati kabisa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa muono wake juu ya sekta hii ya kuongeza masurufu kutoka mwaka jana ilitenga shilingi 53.8 milioni kwa magonjwa hatari kama yale mafua ya ndege na yale ya nguruwe. Mhe. Mwenyekiti, mwaka huu 2011/2012 serikali kwa kuchukua tahadhari kubwa imetenga shilingi 55 milioni, hatuna budi tuipongeze serikali kwa jitihada hiyo ili iweze kuwapa msisimko wafugaji wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mafua ya ndege na nguruwe wataalamu wanaita ni ***traspondaries animal diseases*** ni magonjwa ambayo hayana mipaka. Mhe. Mwenyekiti, tishio hili liliingia nchini Tanzania Mkoa wa Mbeya nguruwe

wengi walikufa kwa idadi kubwa sana, Mwenyezi Mungu alitunusuru visiwa vyetu havikuvamiwa na inshaallah havitovamiwa, lakini kinga ni bora kuliko tiba.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye bahari kuna mazao mengi samaki wamo, kuna mwani, sasa hivi wafugaji wetu wa samaki lakini pia kuna ufugaji wa chaza, halikadhalika kuna uzalishaji wa chumvi. Mhe. Mwenyekiti, tutakapoongeza jitihada ya watu wetu kwenye mazao haya na sisi tutaweza kusafirisha na kuongeza pato la nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi naiomba sana serikali kama vile tunavyolitizama zao la karafuu, basi zao la chumvi nalo wananchi wetu wanalisha kwa idadi kubwa. Kuna wakulima wa zao hili ndani ya majumba yao hawapungui packet 200, lakini soko sasa ndio tatizo. Naiomba sana serikali kupitia wizara hii ya Mhe. Said Ali Mbarouk iweze kufanya jitihada yakutafua soko ili wazalishaji wa zao hili waweze kuuza na kujipatia maslahi yanayostahiki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka ni kwamba imeajiri wananchi wengi, kwa sababu ya ongezeko la watu hasa vijijini. Lakini kadri wanavyoongeza na kujiajiri kwenye sekta hii bado tija wanayoipata ni ndogo kwani uvuvi wanaouvua ni ule ule aliokuwa akivua babu yangu wanakwenda zao pale mwaniona ni kwamba mvuvi yuko kwenye chombo wewe uko kwenye chombo bado unamuona yule pale. Mhe. Mwenyekiti, uvuvi tunaouzungumza leo ni ule uvuvi wa bahari kuu utakaomuwezesha kipato kikubwa mwananchi wa nchi hii. Lakini sio yeye tu kipato kikubwa pia kwa taifa hili kwa mnasaba huu umuhimu wa viwanda vidogo vidogo sasa hivi unahitajika. Mhe. Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo vitafaidika kwa wavuvi lakini pia vitakuza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni changamoto ambalo sasa hivi tumekabiliwa na wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, ushauri nini kifanyike ili tuweze kupata mafanikio zaidi ya sekta ya uvuvi tukaweza kuingia uhusiano huu tulioano kwa sababu nchini Cuba pale Havana wana maabara nzuri inayotegemewa duniani, si kubwa ya eneo lakini ina ufanisi mkubwa wa shughuli za mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa machache hayo, kwa sababu ni mjumbe wa kamati hii nilisema niweze kuchangia kiasi cha wafugaji wangu na wavuvi wa jimbo langu na kumshauri Mhe. Waziri wangu na niseme tu, naomba sasa kutamka rasmi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nawashukuru kwa kunisikiliza ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Asaa Othman. Waheshimiwa Wajumbe naomba tutambue kuwepo kwa wageni wetu walioko Gallery ambao ni

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa *Indian Marine Affairs Association*. Mr. Hamad. Vile vile tunae Mkurugenzi wa Taasisi ya Bahari ya Chuo Kikuu, Margareth Kiyawaliyanga. Karibuni sana. Halafu tunao viongozi wa Jumuiya ya *Zanzibar Animal Effect Society*, Bi Anna Vandable na Bi Helen Pics kutoka Uingereza. Karibuni sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa kuwa leo mchangiaji wa kwanza katika Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na kutupa pumzi kuweza kurudi tena baada ya kupitisha Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na sasa kuweza kuwa na nguvu ya kuweza kuchangia wizara hii ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha nyuma nilipokuwa nikichangia wakati wa bajeti ya serikali kuu nilijaribu kutoa ushauri, hebu tuangalie miradi iliyokuwa muhimu hasa inayokwenda zaidi kwa wananchi na kuweza kutoa kipaumbele ili kuweza kufanikisha lile lengo la kuondoa umasikini. Nilieleza sana suala hili Mhe. Mwenyekiti, lakini inavyoonesha bado Serikali Kuu na ndio maana ikawa watu wa *back bencher* wakali sana, hawakuwa na maana kuwa wawe wakali sana kutokana na kuwashutumu mawaziri wetu, lakini wamekuwa wakali kutokana na kufanikisha lengo liwe. Kwa sababu leo hivi vitabu haviishii hapa tu, vinaishia majumbani mwetu, tunakwenda kuonesha watoto wetu na watoto wetu wanawaonesha na watu wengine. Kwa kweli nimekuwa mnyonge sana leo katika kuchangia leo Mhe. Mwenyekiti, kutokana na ufingu wa bajeti ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kuu ina miradi saba, lakini vile vile katika miradi hii saba kwa kweli ningeomba mimi wakachukua miradi maalum kama nilivyoeleza, nikitoa mfano ni kama kilimo, afya na hii uvuvi. Mimi nasema kuwa tungeanzia hapa, ile *start* yetu ya mwanzo kabisa katika kuonesha jinsi gani ya kuweza kutaka kuondoa umasikini basi tungeanzia katika wizara hizo tatu. Lakini leo hata mwenyewe Mhe. Waziri ushahidi tosha kitabu chake chepesi kabisa, hakikuwa na makorokoro mengi hana kitu ati.

Sasa kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hili suala linasikitisha sana. Huwa tunasema tunataka kuuondoa umasikini, tuna sekta mbali mbali ambazo zinaondoka na umasikini, humu wametuonesha Mheshimiwa wangu.

Lakini vile vile nisisahau kumsifu Mhe. Waziri kwa sababu mwanzo nilianza na huzuni tu, asione kuwa ninamuacha kwa nini simsifu na katibu wake pamoja na mkurugenzi wake. Kwa sababu kutokana na unyonge wa kumuonea huruma kwanza hivi fedha huzipati ile asilimia yenyewe inayotakiwa ni maandishi tu yanayokuwemo humu basi. Lakini pili nimeingia unyonge kuona hata hilo

fungu lenyewe ni dogo na ndio maana nikasau kwanza kukusifu lakini ni wajibu wangu lazima nikusifu. Mhe. Waziri umefanya kazi nzuri kipindi kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yako ina mfumo mzuri sana, ina wataalamu wazuri tu, katibu wako ni mmoja wa mtaalamu mzuri sana wa mifugo asili na jadi sidhani kama utafeli hapa hata kidogo, nina uhakika wa asilimia mia moja katika mambo ya mifugo atakuinua tu Mhe. Waziri kutokana na fani yake. Kwa sababu si rahisi mtu mwenye taaluma yake akataka kuizembea, hapana ataifanisha kutokana na vile alivyoipata taaluma ile na yeye atataka kuiendeleza.

Nikija kwenye Mkurugenzi wa Uvuvi ndio mama yangu mzazi, na yeye halikadhalika, amesomea vizuri taaluma hiyo waheshimiwa, leo ukimwambia hebu nipe hesabu samaki wangapi wa Kiwengwa basi hapa hapa atakupa hesabu hata hafikiri, hataki kioo wala nini anakwamba tu Kiwengwa kuna samaki mia moja kutokana na ule utaalamu wake wa kazi yake. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini shughuli hiyo itaendeshwa vizuri sana kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niingie sasa katika kule kuchangia yenyewe na ndio maana nikasema leo ninachangia kwa upole kutokana na hali halisi ambayo Mhe. Waziri amebinywa sana. Tukiangalia ukurasa wa 4 Sekta ya Mifugo. Kusema kweli kule Pangeni mimi nina eneo moja kubwa sana, mara nyingi sana nilikuwa nikisema kuwa katika hii miradi tunayotoa ya *MACEMP* hii au *TASAF* kwa kuwasaidia wananchi wetu hususan kwenye mifugo, tujaribu sana kuwatafutia mifugo iliyokuwa hai, iliyokuwa *quality.*

Mhe. Mwenyekiti, nikwambie katika Jimbo la Kitope lilipata pesa nyingi sana katika masuala ya mifugo ya ununuzi wa ng'ombe, lakini ukipiga hesabu ni watu wachache tu waliobakia na ng'ombe. Kwa sababu ng'ombe wenyewe wote walioletwa ni hafifu wala sio wa kabila na wabovu. Sasa hili nalo Mhe. Waziri ningeomba mara nyengine ikitokea mifugo kama hii basi lile shamba lako Pangeni lingetumika tena ungekuwa na mbegu bora kabisa. Kwa sababu sasa hivi wataalamu wanapandishia mbegu nzuri tu, basi lile tungekuwa na mfano mkubwa wa uzalishaji Mheshimiwa tulitumie lile bonde tumeliweka tu kule, tungeanza na ufugaji wa mbuzi kama hivi sasa na ndio maana nikasikitika Mhe. Waziri hana pesa, kwa sababu angekuwa na pesa basi pesa zote angepata za kihalali angepeleka kule usingekwenda kutafuta Bara tena hata siku moja, lakini pesa leo tumefeli ukweli tuukubali na huyo katibu atakwambia ukweli tumefeli.

Katika ufugaji wa mbuzi tumefeli, ufugaji wa ng'ombe tumefeli, imekuja migombe mibovu halafu isitoshe wanafanya mchezo. Unakwenda kule Bara

unafikiria utapewa ng'ombe bora hata siku moja usitegemee kama utapata vitu hivyo, hupati bwana. Sasa mimi naomba Mhe. Waziri tuwe waangalifu sana, tunatumia vizuri pesa za wawekezaji hili mimi nakubaliana nalo. Pesa katika wizara yako Mhe. Waziri niseme labda asilimia mia moja pesa mmezitumia vizuri sana za wafadhili wetu, lakini tulichofeli katika mazingira ya *qualities* ya wale wanyama wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mbuzi kidogo sasa tulionao wa maziwa, lakini hao waliobahatika kupata mbuzi ni mbuzi kweli ukiwaona, sehemu za Muungoni sjui lakini ni sehemu za Kusini huko na wanatoa lita mbili mpaka tatu, wanashusha vile viwera maneno ya wenyewe na utahisi hasa kama huyu ni mbuzi mwenye sifa ya kutoa maziwa. Mhe. Mwenyekiti, wamebakia kidogo sana mbuzi hawa.

Nikija katika ufugani wa kuku halikadhalika, hivi sasa kuna haya mambo ya kuchanganya kuku wanaotumia sindano na hawa wa Kiswahili na unapata mbegu nzuri sana. Lakini ni sehemu ndogo sana ambayo inashajihisha wananchi ili kuweza kukuza suala hili, inakuwa ni ndogo na kutokana na hili narudia tena *capital* yao ni ndogo.

Mhe. Mwenyekiti kama tungekuwa tunajaribu kufanya suala kama hili kwa kupata fedha, kwa sababu utakuta wataalamu tunao, lakini huna nyezo mtaalamu huyo anataka apate i pesa iko wapi, wanataka vyombo vya kwenda kutolea taaluma viko wapi, hivi kweli tutaondoa umasikini jamani, serikali inafanya mzaha tu. Wallahi Mheshimiwa lakni basi Wizara ya Fedha bado iko mbele huko tutapambana nayo. Kwa sababu hiki kitu kinasikitisha kusema kweli, hatuko *serious* kwa sababu kuna mambo mengine tuwe *serious.* Leo mtu akija pale akisema mara hii kwenye bajeti yenu au miaka iliyopita mmetumia bajeti vizuri kwa misingi gani, wizara gani ambayo iliusukuma vizuri na ikaonekana hakuna. Sasa hili ndilo tatizo lenyewe. Mimi nafikiria Mhe. Waziri wa Fedha leo yupo na mimi ni shemegi yangu namuomba kabisa kwa makusudi ajitahidi sana wizara hii asiiminye katika kuwapa watu, wape asilimia zao zile zile mia kwa mia ili waweze kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekitini, niende kwenye uvuvi. Kwanza nimshukutu Mkurugenzi amejitahidi sana katika sekta hii. Mkurugenzi ni mwili wake tu ule mwembamba kawaida, lakini ni mfanyakazi ya kusahihisha wananchi kuondoa umasikini kupitia uvuvi, sote mashahidi. Mhe. Mwenyekiti, alifika pahali akaunda kamati na hizi Mhe. Waziri zitakusaidia sana tena uzisaidie Mhe. Waziri kamati hizi. Uzipe iya kuzisaidia kwa kifungu cha fedha ili wazidi kuwa na moyo wa kuweza kulinda.

Mhe. Mwenyekiti, kamati hizi zimetusaidia sana kuna kamati ndogo mpaka kamati kuu, wenyewe walijiwekea kwa mfumo wao. Kama ingekuwa hakuna kamati basi uvuvi haramu ungeendelea mpaka leo hii na samaki usingekuwanao, lakini wale walikuwa walinzi wazuri tu, wanapanda na mambo. Sasa hatari yake utakuta wanapata mashine ya boti moja hii inasikitisha kweli. Anapambana na majangiri huko mbele baharini kiboti chenyewe kimoja watu wanaoingia ni wachache. Hebu tujaribu kubadilisha mazingira hapa kwa hao watu wetu, tuwatafutie boti ambayo inaweza kubabe kamati nzima ili wakapambane na maharamia wenye kuvua uvuvi haramu.

Mhe. Mwenyekiti, uvuvi haramu sasa hivi unazidi kukua na mimi shahidi niliwahi kukwambia Mhe. Waziri kuanzia kule Kiwengwa tunaanza na sehemu ya Kairo mpaka Kumbaurembo wavuvi haramu wamejaa tele Mheshimiwa, wanatuathiri kule. Juzi kulitokea fujo kwa nini wenyewe wanakijiji wamesema kuwa sasa hatutaki uvuvi haramu waliohamia wamekuwa wakali, wamekuwa wababe, unakwenda kupigana katika nchi ya watu wewe unakwenda kufanya uharamia halafu unajifanya wewe mbabe hee. Mhe. Mwenyekiti, mimi hapo nilishangaa sana, hivi wewe nchi ya watu unakwenda kufanya uharibifu halafu unajifanya kuwa *staring* kutaka kupigana pale. Kwa kweli hiki kitendo si kizuri sana, sheria bado haijafanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulirekebisha sheria yake hapa wala sisemi kama ina mapungufu ni sheria nzuri, lakini usimamizi wake haujawa tayari kabisa hebu tusimamie na tuoneshe watu wanaofanya kitu hicho tunatangaza kwenye redio tumeshawafunga na tumewanyang'anya nyavu zao na mikuku yao. Lakini Mhe. Waziri tuko kimya kabisa. Sasa kwa kweli tunaujengea uvuvi haramu kwa nguvu, tujipange sana tu kwa sababu ukanda ule unaharibikiwa vibaya sana, wananchi wa Kiwengwa wameshachoka kwa kuvamiwa na kuchukuliwa samaki wao kinyume na utaratibu wa sheria. Sisi hatumkatazi mtu kuvua bwana, hata kidogo ni ruhusa kabisa bahari yote lakini nenda kwa utaratibu wa kisheria, kavue uvuvi unaotakiwa kwa mujibu wa sheria. Lakini wewe leo unakuja na zana ambazo serikali inalani kabisa zana zile leo unakwenda kumruhusu mtu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kabisa hii sheria ianze kazi mara moja na baada ya bajeti hii nakuomba Mhe. Waziri ufanye ziara sehemu ya Kiwengwa Kairo pamoja na Kumbaurembo wewe na maafisa wako ili kwenda kukemea hili suala mara moja liondoke.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba wizara hii ina ufinyu wa bajeti yake, kwa sababu utakuta wizara hii imetumia fedha nyingi sana katika kuwasaidia wananchi wenye vikundi kwa kuwapa boti, lakini boti zile ni ndogo Mheshimiwa, haziendi katika bahari zilizokubalika kwenye samaki zinaishia

katika bahari ndogo kutokana na zile boti zenyewe ni ndogo. Sasa hivi tujipange, ni bora katika shehia tutoe boti kubwa lakini inaweza kufika katika bahari kubwa na ikavua samaki wa uhakika kuliko kutoa utitiri mwingi wa boti hizi ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, huo ni ushauri wangu tungefanya hivyo. Kwa sababu ingekuw atumeamka mapema tungekuwa na njia hiyo basi mimi naamini sasa hivi Zanzibar tungekuwa tunazalisha sana samaki. Lakini tulijaribu na tukaona labda hii itakuwa ni suluhisho zuri kuchukua viboti vidogo vidogo hatimaye vinapanda juu pale kwa sababu upepo ukija vinawekwa juu. Lakini ukiwa na boti nzuri ya aluminium ina zana zote za kisasa sidhani kama watalala usingizi wananchi wetu. Mheshimiwa tuzitafute boti hizo na mimi nakuamini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna huu uvuvi mwengine wa juu na suala hili Mhe. Waziri nilikwambia, lakini nakushukuru sana Mhe. Waziri na wewe uliona hiki kitu kitakuwa na maslahi kwa wananchi na kitakuwa ni mkombozi wa kuondoa umasikini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tunageuka katika systiem za uvuvi wa kijuu wa kufuga. Wenzetu Bara kila elo nikiangalia katika televisheni na magazeti wanaondokana na umasikini kwa mabwawa ya kufuga samaki. Siku moja nilikwenda Hong Kong nilikuta sehemu moja jina lake limenitoka kwa kuwa ni jina la Kichina lile, lakini nilikuta wanafuga ngisi, ni mradi wa mtu tu, ngisi tele unafikiri atakuwa masikini yule, hata siku moja, *simple* kabisa. Mwenyewe kalitengeneza vizuri bwawa lile tayari sehemu moja ameweka wale wadogo wadogo na sehemu nyengine tayari wale wa kuvuliwa ana *stage* kama tatu hivi. Sasa na sisi Mhe. Waziri wakati huu tubadilike, viboti vidogo vile vinapigwa mawimbi Mhe. Mwenyekiti, siku nyengine kuna upepo mkali hawendi kwa dhoruba. Utasikia leo chombo gani kimezama, kimepasuka sijui na wizara yako Mhe. Waziri watu kama wale kuna msaada wa kuwasaidia wanaopata dhoruba kama ile utakuja kunieleza.

Utakuta kuna nyavu nyengine zimekatika hawazipati Mhe. Mwenyekiti, sasa hatumjengei mazingira yule kwa sababu tunataka kumuondolea umasikini tunakwenda kumzamisha katika ule umasikini wenyewe, lakini akiwa na uvuvi wa juu na wakati taaluma tayari ipo basi anaweza akakaa akavuna vizuri samaki wake juu bila ya kupata mtatizo na umasikini tutakuwa na uhakika wa kuuondoa umasikini. Lakini kama hatuna kitu hicho tutakuja kusumbuka Mhe. Waziri, tena tutasumbuka sana tu. Ndio maana nikasema kuwa kuna mambo ambayo tunayafanya kwa makusudi.

Juzi hapa tumeambiwa zimetengwa shilingi 600 milioni kwa kuokoa maji yapatikane haraka sana. Kwa nini na hizi tusitafute fedha tukamtengea Mhe.

Waziri tukasema na sasa tunaamua tuondoe umasikini kwa kupitia uvuvi. Shilingi milioni mia tisa tunasema hizi tunazipeleka huko mara moja, tunaweza sio kama hatuwezi, lakini basi tu, sijui kwa sababu gani serikali inakuwa haitilii maanani kitu kama hicho. Lakini mimi sidhani kabisa labda kuna kitu kinanisumbua sana kwenye kichwa changu, kwa sababu hii ni sekta ambayo ina-*deal* na wananchi, wanapata shida kule chini Mheshimiwa, wanafika pahala wanasema kuwa vipi serikali yetu jamani inatusahau. Mhe. Mwenyekiti, hili suala mimi naomba tuliangalie.

Lakini pia kuna jambo moja, hivi karibuni nasikia huko wenzetu walipitisha sheria ya uvuvi wa Bahari Kuu. Mimi nikauliza sheria hii kweli wenzetu kule Bara wamepitisha hata na sisi tusiletewe huku, ukiangalia ni kweli itakuwa imepitishwa kwa sababu tayari ofisi imeshajengwa kule, lakini haifanyi kazi kwa sababu sheria bado haijakuwa kamili. Wameshachaguliwa Wakurugenzi, watendaji, sasa tuone basi madhali haijapita kwenye jengo hili hiyo si sheria tunakubaliana hivyo, tuko kwenye Muungano hivo na sisi tumo katika sehemu ya Muungano. Lakini sheria inapopitishwa sisi hatushirikishwi tunasikia tu sheria ya Bahari Kuu ishapitishwa na kila kitu, leo ukitaka kuvua sehemu ya Bahari Kuu unaambiwa upite huko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tuiangalie hii sheria, kwa kweli sheria hii haikututendea haki Wazanzibari tuseme ukweli ulivyo. Mfano Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna kesi ya samaki kule, kesi ile Mhe. Mwenyekiti, nani aliyepata samaki Zanzibar, wenzetu wamegawana samaki huko sisi hata mmoja hakuletwa wa dawa huku, tunakwenda wapi Mheshimiwa? Mimi namuomba Mhe. Waziri aiangalie hii sheria ikoje halafu aje anambie sheria ni halali au si halali. Kwa sababu naona kama imepitishwa kinyemela tu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hili naomba utusaidie katika kuja kunijibu na unijibu vizuri sana hii sheria ikoje katika kufanya kazi kwake. Wazanzibari tunanufaika nini na kama hatunufaiki na kitu chochote basi sheria hii hatuitaki.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kama nilivyokwambia kuwa mimi bado nimo katika masikitiko makubwa sana ya wizara hii kwa sababu imejipanga vizuri katika njia ya kuondoa umasikini lakini bado Serikali Kuu haijakuw atayari kutaka kuisaidia wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, namalizia kusema kwamba fedha hizi ambazo wamepewa wizara hii kama ingekuwa ni suala la kuonesha *pilot* jinsi gani ya fedha kama kuonesha kuwa kidogo basi mimi ningewaambia wizara hii fedha ziletwe Jimbo la Kitope uone kama hazikumezwa vuup, kutokana na udogo wake na jimbo lenyewe lina watu elfu kumi na pesa hizo uziweke pale Jimbo la Kitope basi hazisaidii Mheshimiwa zitamezwa na wewe utaulizwa ndio umetuletea nini.

Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makuu kabisa Mhe. WAziri wa Fedha ajitahidi sana kuisaidia wizara hii na kuipatia fedha. Kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru sana Mhe. Waziri na katibu wake na Mkurugenzi wa Uvuvi pamoja na wakurugenzi wengine wajitahidi sana kwa njia zao. Kwa sababu hivi sasa namshukuru Mhe. Waziri ananipelekea kijana anakwenda kusomea uvuvi wa juu, sio mimi hata na wenzangu wengine katika majimbo wamepata raha hiyo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hilo nililisahau lakini nimshukuru sna Mhe. Waziri na hilo alifanye na wengine azidi kuwapeleka kila anapoona kuna wafugaji wa chaza, ngisi, majongoo na kadhalika apeleke taaluma ili tuweze kuondoa umasikini kwa haraka sana. Na kwa hilo Mheshimiwa yuko tayari na ninaamini hili anaweza kulifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na wewe kwa kunipa muda na kunistahamilia na mimi naunga mkono kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Kitope, ahsante sana.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii usiku wa leo kuchangia machache kuhusu wizara hii mpya ya Mifugo na Uvuvi. Kwanza napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba nzuri iliyochukua muda wa saa kamili. Kwa hivyo anastahiki pongezi kwa kuweza kusoma haraka haraka hotuba yake na kutubakishia muda wa kuweza kuijadili.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, lazima tujue umuhimu wa mambo mawili ambayo amekabidhiwa, pamoja na kwamba ni sehemu muhimu ya kupata mapato wananchi katika mambo ya ufugaji na mambo ya uvuvi, lakini ni sehemu muhimu sana ya lishe ya wananchi wetu. Kwa kweli sehemu hizi mbili kama zitakuwa hazikuangaliwa vizuri ndio tunaangukia ule ugonjwa wa Koshakoo na Mtapiamlo na mengine ambayo yana ukosefu katika kiwiliwili chetu. Sasa kwa hivyo, wizara hii kwanza itizamwe kwa njia hiyo, lakini na wao wenyewe kazi zao wazifanye kwa njia ya kusaidia mambo hayo mawili.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi kilichopita nilitoa mfano siku moja baada ya kukaa na mtu mmoja katika mazungumzo yetu kilipita kipakacha kina dagaa na kwa lugha za huko wanaita towea. Yeye anatembeza dagaa kuwauzia wananchi sasa yule niliyekaa naye akaniuliza unaweza kukisia dagaa lile anaweza akawauzia wananchi wangapi? Pengine halizidi kilo kumi dagaa lile, lakini nyumba 30 au 40 zinauziwa dagaa lile. Sasa angalia ni kiasi gani kila nyumba inavyokula dagaa kilo kumi. Kwa hivyo, mtu mmoja katika nyumba ile anakula kitoweo au samaki au dagaa yule kiwango gani? Kwa hivyo, katika *conclusion* yangu siku ile nikasema basi ilivyokuwa tunakula wali kwa dagaa au kitoweo na sisi tumezungukwa na bahari, basi tufike wakati tule samaki kwa wali na wafikishaji wa eneo hilo ni wizara hii. Kwa sababu samaki wamo na wananchi

wetu wanataka kufuga kwa upande mmoja wa nchi kavu lakini namna gani ya kuendelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Mwakilishi aliyetangulia kwamba kwanza kwenye kamati kawashukuru kwa ripoti yao na aliyetangulia kusema kwamba bajeti ya wizara hii kwa kweli ni ndogo mno kiasi cha kusikitisha hasa. Mimi nilisema katika kipindi hichi hichi cha bajeti kwamba kuipa uzito kilimo ndivyo inavyostahiki, lakini sasa hivi kilimo kina *risk* nyingi. Kuna hali ya hewa kama mvua ipo au hapana itaathiri harakati za kilimo, kuna wadudu waharibifu wanaathiri harakati za kilimo. Lakini tungelianza kwenye uvuvi ambao shamba lake liko bivu kabisa tungeliweza kukitononesha kilimo chetu kidogo kidogo.

Kwa hivyo, mimi nahisi kwamba hata kama tumeteleza mwaka huu lakini tunaiagiza serikali mwakani tukijaaliwa wizara hii ipewe uzito wa aina yake.

La pili tuanze na ufugaji wa kuku. Mhe. Mwenyekiti, kumegawika sasa hivi baada ya matatizo mengi wanayopata wananchi wetu kufuga wale kuku ambao si mazoea ya nchi hii, tunawaita sio kuku wa kienyeji. Watu wengi wameanzisha ufugaji wa kuku wa kienyeji na kwa sababu wananchi bado wanawapenda hawa kuku wa kienyeji naomba sasa wizara iangalie uwezekano kama Mhe. Waziri alivyosema katika hotuba yake kumuelekeza mwekezaji kuweka katika kuku wa mayai na wengineo. Basi waweke kituo kwa njia yoyote ile ikiwa ni mwekezaji au vyenginevyo kuzalisha hao kuku wa kienyeji ili watu wakawachukue kirahisi, waweze kununua vifaranga wa kuku wa kienyeji kwa bei nyepesi na kwa urahisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wengi wanaotaka kufuga mimi binafsi nimetembelea sehemu nyingi za jimbo langu lakini tatizo ni kupata hao vifaranga. Kwa sababu tayari mtu anataka auze kuku ambaye atapata faida, hayuko tayari kuuza vifaranga wakati hajapata bei nzuri. Kwa hivyo, hata huu ufugaji wa kuku wa kienyeji umeshaanza kuwa na matatizo ya kupata hao kuku wa kufuga.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri tulitazame hili kwamba wale ambao wanataka kuendeleza kuku wa kienyeji basi kuwe na mpango wa kupata wale vifaranga kwa njia nyepesi ili ufugaji wao uwe mwepesi na kuendelea.
Lakini nilimwambia hapa rafiki yangu muwezeshaji kwamba tunategemea wizara yake itashirikiana na wizara nyengine na hii Wizara ya Mifugo na Uvuvi niliitaja, ili kuwe na mtandao mzuri wa kuwawezesha wale wananchi isiwe kila mmoja anafanya lake. Kuna wengine wanatazamwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, kuna wengine

wanatazamwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, wanatazamwa na wizara yako, lakini wengine hawatazamwi kabisa.

Kwa hivyo, naomba katika kipindi kijacho tuone kwamba kuna ushirikiano wa kutosha baina ya wizara hizi mbili, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nchi yoyote haiwezi kwenda bila ya kuwa na takwimu halisi ya mahitaji na kile ambacho kinazalishwa. Sasa mimi nafikiri kama tunaangalia kiasi gani juu ya uzalishaji tutoe takwimu kwamba kwa kuku tulionao kama kila mtu atapata kula kuku basi tuwe na kuku kiasi fulani kwa wiki mara moja au mara mbili. Sasa lengo hilo ndio tulielekee tutawezaje kufika hapo. Hivi tunavyokwenda kwa kweli tunakwenda katika hali ngumu sana. Kwa hivyo, hao maafisa wetu waweze kuweka takwimu za usahihi ili tuweze kujua uzalishaji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, suala jengine liko kwenye ufugaji wa ng'ombe. Hebu wizara sasa iamue ni nani aliyekuwa na mamlaka ya kuweza kuona kwamba ni ng'ombe wa aina gani tunafuga. Kwa sababu hii mitandao ya miradi ni mizuri lakini matokeo yake kwa sababu wakati mwengine wizara haiingizwi kati, kunatokezea miradi kama ya *TASAF* na mengineyo wanaagiza ng'ombe ambao pengine wizara haina taarifa nao. Sasa matokeo yake inakuwa hawana tija.

Mhe. Mwenyekiti, mfano huo umetokezea kwa mbuzi watu wengi wanasema mbuzi ambao wameagizwa hawakuweza kukaa katika mazingira yetu. Kwa sababu sasa hivi Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko peke yake basi ingefanya utaratibu wowote lakini miradi ambayo itaingiza uagizaji wa wanyama wawe na udhibiti nayo. Ni kitu muhimu sana kwa sababu wengine wanapata tabu sana na wanaingia gharama kubwa ya ufugaji lakini matokeo yake tija hakuna.
Kwa sababu kipo kitengo cha Idara ya Mipango, Sera na Utafiti mimi nafikiri wizara ingekaa kitako ika-*define* sasa utafiti katika wizara hii ni upi. Nasema hili Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kila wizara sasa hivi imeundiwa idara hii, lakini tulipopita katika kamati bado baada ya miezi saba ya kuundwa wizara hazijajipanga idara hii itafanya utafiti wa aina gani. Sasa ndio nasema kwamba kwa sababu ipo idara hii basi tayari ijipangie malengo ni utafiti wa aina gani ambao idara hii itaufanya kwa sababu huu ni utafiti wa kisera.

Kwa mfano, kama kuna *research institute* ya mambo ya mifugo labda maradhi ile ni mbali. Sasa huu unatarajiwa vile vile uingize utafiti wa kisera. Je, sera tunayokwenda nayo kuhusu huu ufugaji utatupelekea wapi. Kwa hivyo, mimi nafikiri twende *beyond the scope* ambayo ukiona tu utafiti unakwenda, twende

kwenye *scope* yake hasa kuona kwamba ni utafiti wa aina gani ambao unawezekana.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye ufugaji wa ng'ombe wa maziwa wananchi wengi wamejitokeza kufuga ng'ombe wa maziwa lakini kunakuwa na kupanda na kushuka. Ukiwa na aina fulani ya mradi ambao wananchi hao wanasaidiwa ile biashara inakua, lakini mradi ule ukiondoka tu inashuka. Sasa je, hatuwezi kuweka mikakati ambayo tutapata wataalam wanaoita *sustainable environment* ya ufugaji ambayo itawafanya hata kama mradi utaondoka basi ufugaji utakuwa unapata nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala la uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyopata taaluma juzi mimi nafikiri kwamba pamoja na yote tunayoyajua lakini tuamue kufanya kazi hilo ndio jambo muhimu. Maneno sasa yameshakuwa mengi tuamue kufanya kazi ya uvuvi kwa sababu nchi yetu ni ya visiwa. Wenzetu wengi wanajiendesha kwa shughuli za uvuvi kwa nini sisi tushindwe kujiendesha. Mpaka hivi leo hatuna rekodi ya kusafirisha hata samaki mmoja wakati walio Bara huko wanazungukwa na ziwa tu ambalo lina mipaka, halafu ziwa moja hilo hilo limegaiwa kwa nchi karibu sita na bado wanasafirisha minofu.

Sasa sisi bahari yetu haina hata mpaka ni kwenda tu ukavua lakini miaka yote hiyo inayokwenda hata kolekole hatujasafirisha. Mhe. Mwenyekiti, tujiulize tunakosea wapi. Lakini Waswahili wanasema usiangalie ulipojikwaa angalia ulipoangukia. Tumeshakosea tulipokosea hebu tuseme sasa basi mwaka fulani tuanze kusafirisha na sisi, yaani watu wetu wameshatoshelezeka na samaki wao na hawa wengine tunasafirisha kutafuta mambo mengine hilo ndio la kufanya. Lakini kwa kweli ukimwambia mtu yeyote kwamba sisi tumezungukwa hapa na bahari ikawa hatuna samaki wala hatusafirishi.

Mhe. Mwenyekiti, wewe ulikuwa hai mzima mwaka uliovuliwa samaki ikakamatwa meli hapo Dar es Salaam. Sisi tulipata habari kupitia gazeti fulani ambalo lilichapishwa siku moja tu kwamba wale walishindwa kuwashtaki kwa sababu bahari waliyovua ni mamlaka ya Zanzibar na Mahakama waliyowapeleka ni ya Tanzania Bara. Wakili alipokuja akawaambia nyinyi hamna haki ya kushtaki hapa ilikuwa kesi yenu muipeleke Mahakama Kuu ya Zanzibar. Wakenda chini kwa chini wagaiwe sijui wafanywe hivi lakini ukweli ni kwamba kesi ilifeli.

Sasa angalia samaki wale matani kwa matani meli moja tu hatuzijui hizo nyengine zinazokuja kila siku. Mhe. Mwenyekiti, tutakaa mpaka lini sisi tusubiri tu. Basi bora ikiwa hatuna uwezo tutafute meli moja ambayo na sisi

tutaingia ndani yake tutakuwa na ubia. Meli nyengine hujifanya zinatekwa nyara huko na Wasomali kumbe zinavua samaki.

Kwa hivyo, kitaifa tuna kazi kubwa ya kufanya ya kufikia kuvua samaki wetu. Mimi sidhani vile vile kwamba ofisi itatusaidia sana katika kuvua samaki. Jambo la muhimu na la mara moja ni kupigania kupata *facility* ambayo itaweza ku-*process* samaki wetu. Tunaishukuru sana wizara kwa kuharakisha kupata ofisi nzuri na ambayo itatuunganisha kimataifa, lakini tusitosheke na ofisi lazima tupate nyenzo za kuweza kusafirisha. Masuala haya ya kugombaniana ardhi tunaiomba serikali iwaachie taasisi zipate ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, sisi ni mashuhuda kwa sababu tulikuwamo ndani ya kamati fedha zilikuwa zimeshaletwa zimo mikononi za kuanzisha kujenga soko na sehemu ya kuwatengeneza wale samaki watakaovuliwa yaani *processing unit.* Kukiwa na migogoro ya ardhi, ardhi hii sio, hii imeshachukuliwa, matokeo yake fedha zikapitwa na muda.

Mhe. Mwenyekiti, tumekwenda sisi Mwanza kwa kazi hizo hizo za kamati tumeoneshwa soko lililojengwa kwa pesa hizo zilizorudishwa kwenye *World Bank.* Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana tusije tukachelewa tena halafu tukaja tukakosa na mambo mengine makubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye jimbo. Mhe. Mwenyekiti, Jimbo langu la Ziwani karibu sehemu kubwa ni ya wavuvi. Kwa kweli hawajafaidika sana na misaada ambayo inatolewa na hii wizara. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aiangalie sana, yeye mwenyewe ameshatembelea ni sehemu ambayo inatoa kile kitoweo nilichokitaja cha kimaskini ambacho kila siku kipo sokoni ikiwa kuna mvua kuna upepo kitu kinachoitwa dagaa. Kwa hivyo, tunawaomba sana wawasaidie hawa kama ambavyo dalili aliionesha.

Lakini kuna kitoweo kimoja cha diko kinaitwa kichuwani bahati nzuri hata katika kitabu chao kile walichotupa kwenye semina siku ile nilishukuru sana kwamba kwa jina kimetajwa kichuwani. Hili diko liko kati kati baina ya Chake Chake na Wesha na upande huu Mtambwe. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ikiwa kuna aina yoyote ya msaada wa kujengwa kijisoko kidogo kwa kiasi chao aweze kutufanyia hivyo ili wale wavuvi pale waweze kufaidika na hii misaada ya *MANCEP* na mengineyo inayotoka.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wale huko nyuma walikuwa wanaendesha diko wao wenyewe wavuvi waliweza kumudu hata kununua kifusi cha njia yao nzima ya kilomita zaidi ya tatu bila ya kutegemea Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa wakati ule. Ni wananchi ambao wana uwezo wa kujiendeleza na wana uwezo wa kuendeleza. Namuomba sana Mhe. Waziri atazame kujenga

soko kule la kiasi chao ili na wao waweze kujitanua katika shughuli zao na waweze kujiondolea umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo namuomba sana Mhe. Waziri ayazingatie yatakayochangiwa na wajumbe wote kwa sababu hii wizara ina *nickname* ya kitoweo kama nilivyosema ni muhimu sana kwa kuongeza lishe katika kiwiliwili. Mhe. Mwenyekiti, nasema kwamba kama itashughulikiwa kweli, mbona hayo mafuta tunaweza kughairi yasichimbwe kwanza tukangoja tukajipanga vizuri. Bahari ina utajiri bwana.

Mhe. Mwenyekiti, kilikuwepo kimeli kidogo hapo tulichokipata sisi kwa *East African Community* ilipovunjika, kilikuwa na vitu vingi ndani yake mle. Mimi nilikuwa na jirani yangu na mzee wangu wakati huo alikuwa Afisa Mdhamini wa Wizara ya Uvuvi wakati huo na alikuwa yeye mwenyewe ni *gogler*, sio hii ya kuingia kwenye mtandao hapana ni ile ya kuzamia. Walikwenda katika kipindi kile wakawa wanawatazama wale samaki, ile meli ilikuwa na uwezo wa kuona mwahali ambamo mna samaki na halafu ukawapiga picha kwa sababu ilikuwa ni ya *Marine Services*. Mtaalam aliyekuja mara moja aliwaambia samaki waliokuwemo wengine wana umri wa miaka 400.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tuone kwamba na sisi tuko baharini tukavue. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hapa anatuletea bajeti *deficit* lakini haileti hata meli moja ikenda ikavua tukapata samaki kwanza. Namuomba Mhe. Waziri ajikaze kidogo tukavue.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja lakini nangojea samaki wangu, kuula mtupu siwezi. Ahsante.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuichangia Wizara hii ambayo ni muhimu katika kujenga afya kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuona kwamba kuna haja ya Wizara ya Kilimo na Maliasili ambayo ina mambo yote haya lakini kuigawa. Amefanya hivi kwa sababu tuweze kupata utendaji na ufanisi mzuri zaidi katika kila wizara.

Lakini pia nichukue nafasi hii nimpongeze sana tena Mhe. Rais kwa kuona kwamba Mhe. Said Ali Mbarouk ndio anaweza kumpa wizara hii na kutoa imani yake. Ni imani yangu kwamba kwa Mhe. Said ninavyomuelewa pamoja na watendaji ambao amewapata basi wizara hii itafanikisha shughuli zake zote. Isipokuwa tu na mimi kabla sijasahau nimuombe sana Mhe. Waziri wa Nchi

(OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa kweli wizara hii imepata fedha kidogo sana. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha pale ambapo wizara hii itahitajia fedha basi aitupie jicho la huruma ili aweze kuisaidia wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna visiwa na visiwa ambavyo Mwenyezi Mungu amevibariki kwa bahari, amevibariki kwa ardhi nzuri. Kwa hivyo, mimi niseme kwamba hili suala la uvuvi tumepitwa na wakati kidogo kwa sababu tumejua kwamba sisi ni visiwa lakini huko nyuma tumejisahau. Kwa vile sasa hivi ni wizara maalum ambayo imeundwa ya Mifugo na Uvuvi basi naomba kwanza tupitie upya sera, tupitie upya sheria, kama kuna sera ambazo zimepitwa na wakati na kama kuna sheria zimepitwa na wakati basi tuzirekebishe ili tuweze kupata ufanisi zaidi na mzuri wa kutekeleza wizara hii.

Lakini pia niseme tu kwamba ni vyema tukahakikisha tunapitia upya miradi yote ya uvuvi, miradi yote ya mifugo, ili kuhakikisha ni wapi ambapo tumekwama katika miradi yetu ya uvuvi. Ni sababu zipi ambazo zimesababisha miradi yetu ya uvuvi ikakwama.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nije kwenye mifugo. Ni sababu zipi ambazo zimesababisha kukwama katika mifugo, ni kwa nini tumekwama. Iwe mifugo ya ng'ombe, kuku, mbuzi na mifugo ya kila aina ambayo kwa kweli haikuleta tija nzuri katika visiwa vyetu. Naiomba sana wizara na kwa jinsi ninavyowaelewa watendaji wa wizara hii, suala hilo kwao ni ndogo mno. Wanaweza wakalifanyia utafiti ili kuweza kuboresha miradi yetu na kufikia malengo ambayo tunayahitaji.

Jengine niseme kwamba katika kutembea kwetu kwenye Kamati yetu wizara hii ina rasilimali nyingi sana na ni rasilimali ambazo zinaweza zikasaidia katika hili. Kwa hivyo, naiomba sana serikali, zile sehemu ambazo zinamiliki basi ni haraka mno kupatiwa hatimiliki kwa sababu zinavamiwa bila ya kiasi.

Tumetembelea sehemu nyingi sana Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyingi sana zimevamiwa na wakaazi mbali mbali. Naomba sana kutia uzio katika sehemu ni kitu muhimu. Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia wizara hii tuhakikishe na kwa sababu hatimiliki ni wizara kwa wizara na ni wizara zote za serikali hii hii, naomba twende katika zile *proper channel* ambazo tutasaidiana wizara kwa wizara, ili kuhakikisha wizara zote za serikali zinapata hatimiliki, ili kuweza kuhakikisha kutokuelewana na wananchi wetu ambao tunawaongoza sisi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, niombe kwamba Afisi ya Pemba kwa kweli ilitupwa sana huko nyuma, ni lazima nikubali na ni lazima tukubali. Naiombe sana afisi

hii itizamwe kwa jicho la huruma, kwa sababu ni aibu tumekwenda katika kugawanyagawanya kila wizara imepelekwa huku, hata gari afisi hii haina. Ilikuwa imeazima katika afisi nyengine, basi naomba sana pamoja na yote lakini afisi hii nayo itizamwe kwa jicho la huruma, ili nao wafanye ufanisi mzuri zaidi katika kutekeleza shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulipata semina, tulipata somo ambalo kwa kweli ni somo zuri sana. Nasema bado kama tulivyoambiwa kwamba tufanye mapinduzi ya uvuvi, tutayafanyaje mapinduzi haya ya uvuvi. Kama nilivyosema mwanzo kwamba tufanye utafiti wa miradi yetu upya ili tuangalie ni sehemu ipi na ipi ambayo hatukuitendea vizuri, kuanzia vifaa, vitendea kazi na mambo yote ambayo yanapaswa wizara hii kuyatekeleza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, niseme hivi, nitowe wito kwa mikoa pamoja na wilaya tuhakikishe tunaisaidia wizara hii, ili kuipa msukumo na hasa kwa sababu wizara hii itaweza kuwajiri vijana wetu, itaweza kuwasaidia akina mama wetu kwa sababu akina mama popote unapokwenda wewe utawakuta. Wakisikia mradi fulani basi waanzilishi ni wanawake wa Zanzibar ndio wanaochukua majukumu ya kufanyakazi nzito sana. Niziombe wizara husika, Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana Wanawake na Watoto zishirikiane wizara hizi waelewane namna gani ya kuweza kuwasaidia vijana wetu, kina mama wetu pamoja na vikundivyote ambavyo vimeanzishwa. Hapo vikishirikiana kwa udhati kabisa ni imani yangu kubwa kwamba umaskini utatoweka.

Jengine ambalo nilizungumze Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba nitowe wito kwa wafanyabiashara wetu wa Zanzibar. Nitowe wito kwa wafanyabiashara wetu wa Zanzibar, kwamba wawekezi katika uvuvi. Nadhani akitokea mfanyabiashara mmoja tu akawekeza katika shughuli hii ya uvuvi na akaiona faida yake, basi ninahakikisha kwamba wafanyabiashara wengine wataiga.

Kwa hivyo, naomba sana wale wenzetu ambao wanauwezo na kwa Zanzibar pesa tunazo, Wazanzibari pesa tunazo. Wale watu ambao wana uwezo, kama wanavyonunua vyombo vya usafiri vya kutusaidia usafiri wa kwenda Dar es Salaam, Unguja au Dar es Salaam Pemba basi wajitokeze kuwekeza katika sekta hii ya uvuvi. Ni imani yangu kwamba wizara hii itaweza kulenga majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe serikali pamoja na wizara kwamba tuna vikundi vingi sana ambavyo vimekopeshwa mbuzi kulipa mbuzi, vimekopeshwa ng'ombe kulipa ng'ombe na mifugo ya kuku, lakini bado taaluma ni finyu. Naiomba sana wizara izidishe taaluma kwa watu wetu ambao wana mifugo ya

namna hiyo. Lakini si hivyo tu, niungane na kamati yangu kama ilivyosema kwenye ripoti yetu ni kwamba utamkopesha mtu mbuzi mmoja, kwa kweli haileti tija ni vyema kama tutamkopesha mtu basi tumpe kitu mbacho kitazalisha na tija yake itaonekana sio vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ilipokuwa inachangiwa Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi hapa kulikuwa na mifuko hii ya JK na AK mtu anakopeshwa Shs. 50,000. utamuwezeshaje mtu kumpa Shs.50,000 kisha ukamwambia afanye biashara, haiwezekani, Shs. 50,000 imepitwa na wakati, si lolote si chochote sasa hivi Shs.50,000. naomba sana wizara ambazo zitawezesha Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tukawa na kitu kidogo lakini kikaleta tija na manufaa kwa wananchi wetu, kuliko kuwa na mambo msururu matokeo yake yakawa hayaonekani ni ziro pesa hazilipwi, faida haionekani, mtu anatapatapa.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe wito kwamba tuna matatizo. Tunapopewa kitu ambacho tuendeshee maisha, mawili au matatu yameshajitokeza. Kwanza unajisahau kama umekopeshwa na wenzako wanataka ulipe wewe ili na wao wakopeshwe, unasema pesa ni za serikali lakini serikali hiyo hiyo ndio inayokuangalia wewe kuhakikisha kwamba unajiondoa katika umaskini.

Mhe. Mwenyekiti, nitowe wito kwa wanavikundi. Maana na wizara hii ina vikundi vile vile. Nitowe wito kwa kweli umefika wakati wa kubadilika na kuisaidia serikali. Watu wanasema ukisaidiwa na wewe ujisaidie. Kwa hivyo, nawaomba wananchi wa Zanzibar wale wote ambao wamepewa mikopo kwa ajili ya kujinasua katika umaskini, nawaomba sana kwamba serikali imewaamini basi na wao wajiaminishe kwa serikali yao, ili waweze kulipa na wenzao waweze kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba ni imani yangu wizara hii kwa mashirikiano yetu sote Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kwa sababu wizara hii ni wizara ambayo ina tija ya vijana wetu na kina mama pamoja na wizara ya uwezeshaji, pamoja na wizara ya wanawake na vijana tutaipa mashirikiano makubwa ili kuhakikisha kwamba pale ambapo tunapotaka kwenda tuweze kufika japo hatua mbili japo sio zote.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kusema kwamba naitakia kila la heri wizara hii na nitilie mkazo kwa Mhe. Waziri wa Fedha, chondeee chonde. Kwa kweli wizara hii uisaidie kwa sababu ni wizara muhimu na ni wizara nyeti. Zote ni wizara muhimu, lakini hii ina tija kwa binadamu na afya na kama binadamu hana afya basi chochote kile hakiwezi kikatendeka.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia juu ya mia, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Kwanza nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu na kwa michango mizuri. Hadi kufikia hapa tunaahirisha Baraza letu tukufu hadi kesho siku ya Ijumaa saa 3:00 za asubuhi, ahsanteni.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 22/07/2011 saa 3:00 asubuhi)